# Nipashe

Jumatatu Agosti 26, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580006

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Aua mke kwa shoka, wenye hasira kali wamchoma moto

UKURASA 3


Nipashe Spotika

NYOTA EPL WANAOWEZA KUWAHI DIRISHA KUTIMKA UK.20

ISIKUPITE

MTIFUANO...

UKURASA 13

SAKATA LA ATCL

# Jopo la wanasheria latua Afrika Kusini

• **Ni** kuifuatilia ndege iliyokamatwa nchini humo kwa amri ya mahakama kisa... *Endelea uk. 2*




WAZIRI WA UCHUKUZI, ISACK KAMWELWE

## Wakimbizi 2,000 sasa kurejeshwa kila wiki

UKURASA 4

## Vyama vyaeleza hofu kanuni za uchaguzi Serikali za Mitaa

UK. 2

**MICHEZO** NI VITA MTOANO SPRITE BBALL KINGS UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kushoto) na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Burundi, Pascal Barandagiye, wakisaini maazimio ya makubaliano ya kuwarejesha wakimbizi 2000 katika nchi yao, kila wiki kuanzia Oktoba Mosi, mkoani Kigoma jana. **PICHA: WMNN**

SAKATA LA ATCL

# Jopo la wanasheria latua Afrika Kusini

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwelwe, amesema jopo la wanasheria limeondoka nchini kwenda Afrika Kusini kufuatilia sababu ya kuzuiwa kwa ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL).

Waziri Kamwelwe alitoa taarifa hiyo jana wakati akihojiwa na waandishi wa habari kwenye ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa kivuko kipya cha Mafia - Nyamisati.

Alisema tayari kuna wanasheria wameondoka juzi na wengine wameondoka jana kushughulikia suala hilo kwa kuwa ni suala la kimahakama.

Alisema ndege hiyo ilikamatwa kwa amri ya mahakama na kwamba hawakutoa taarifa kwa Tanzania mpaka ilivyozuiliwa ndipo wakapeleka taarifa kwa balozi Tanzania nchini Afrika Kusini na tayari muda ulikuwa umeshakwenda.

Ndege hiyo aina ya Airbus A220-300 ilizuiwa mwishoni mwa wiki kwa amri ya Mahakama Kuu ya nchini humo kwenye Uwanja wa Ndege wa Oliver Tambo, jijini Johanessburg na abiria waliokuwamo ndani ya ndege hiyo walitafutiwa ndege nyingine ya kurudi nchini.

"Sina cha kueleza chochote kuhusu ndege iliyokamatwa maana mpaka sasa hatujajulishwa ni kwa nini inashikiliwa na mahakama, sisi kama serikali tunalishughulikia suala hilo na tayari tumekaa vikao na nimezungumza na Mwanasheria Mkuu akaniambia jana wamepeleka wanasheria na leo wamepeleka wengine kushughulikia suala hilo, hivyo wanasheria wetu watatueleza na taarifa tutaitoa kwa umma," alisema.

"Kama mnavyojua Jumamosi na Jumapili hakuna kazi duniani kote na muhimili wa mahakama haufanyi kazi siku hizo ndio maana hatujajua kwani mahakama imezuia hiyo ndege, taarifa tumeipata Ijumaa muda umeshaenda hatukuweza kulishughulikia suala hilo," alisema.

Alisema sababu zitajulikana baada ya wanasheria hao kufika mahakamani na umma utajulishwa.

### SERIKALI YASIKITISHWA

Vile vile, Kamwelwe alisema kukamatwa kwa ndege hiyo kumewasikitisha watu wengi na serikali inafanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha ndege hiyo inaachiwa mara moja.

"Ile ndege ni yetu, ni kodi zetu, serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha ndege hiyo inarudi nchini," alisema.

Alisema hakuna mgogoro wowote wa kibiashara na nchi ya Afrika Kusini kwa kuwa hata wao ndege zao zinakuja nchini na kufanya biashara.

"Hatuna mgogoro wowote na Afrika Kusini mbona ndege zao zinatua mara mbili mbili nchini sasa na sisi si tungewakamata tumewaacha kiustaarabu tumewaacha waendelee kuja."

Alifafanua kuwa hata taarifa za kuzuia ndege hiyo hazikufika kwa wakati kwa kuwa ilikuwa inajiandaa kuruka ndipo ikazuiliwa.

Kuhusu abiria waliokuwamo ndani ya ndege, Waziri Kamwelwe alisema tayari wamerudishwa nchini kwa ndege ya South Africa Airways juzi na wengine wamewasili jana.

Alisema kampuni ya ndege ya Rwanda Airline na Ethiopia Airline, walikataa kuwabeba abiria hao.

Ijumaa serikali ilipatiwa taarifa kutoka kwa balozi wetu wa nchini Afrika Kusini kuwa ndege ya ATCL imezuiliwa kwa amri ya Mahakama Kuu Gauteng bila kueleza sababu ya kukamatwa kwa ndege hiyo.

### KUJENGWA KWA KIVUKO

Wakati huo huo, Waziri Kamwelwe amesema ujenzi wa kivuko kipya cha Mafia - Nyamisati utakamilika Februari, mwakani na utagharimu Sh. bilioni 5.3.

Kamwelwe aliyasema hayo baada ya kukagua eneo hilo la ujenzi na kwamba utagharimiwa na fedha za serikali ambazo zimetokana na kodi ya wananchi. Alisema kukamilika kwa ujenzi wa kivuko hicho kutasaidia kuondoa adha ya usafiri kwa wananchi wa Mafia na pia kushuka kwa bei ya mafuta ya petroli wanayouziwa kwa sasa lita moja Sh. 3,000.

Alisema mkandarasi wa ujenzi wa kituo hicho ambaye ni Kampuni ya Songoro Marine Transport Boat Yard LTD, atahakikisha anapatiwa fedha zake kwa wakati ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Alisema kampuni hiyo ambayo ni ya wazawa inasifa ya kufanya vizuri katika ujenzi wa vivuko na kwamba mkakati wao ni kuhakikisha kodi za wananchi zinatumika na wazawa na sio kuwaleta makandarasi nje ya nchi.

Mbunge wa Jimbo la Mafia, Mbaraka Dau, alishukuru kuanza kwa ujenzi huo na kueleza kuwa utasaidia kutatua changamoto ya usafiri.

Dau alimwomba waziri kuhakikisha pasiwapo na ucheleweshaji wa fedha ambao unaweza kusababisha kukwamisha mradi huo kumalizika kwa wakati.

Mhandisi wa Wakala wa Ufundi na Umeme (Tamesa), Japhet Maselle, alisema kukamilika kwa kivuko hicho kutafanya jumla ya vivuko kuwa 31 na kwamba kukamilika kwa ujenzi huo ni jitihada za serikali kuboresha huduma kwa wananchi na kuhakikisha maeneo mengi ya nchi yanafikika kirahisi ili kuinua uchumi wa Tanzania.

Maselle alisema kivuko hicho kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 100, abiria 200, magari madogo sita na mizigo.

# Upinzani watilia shaka kanuni za uchaguzi S/Mitaa

**Na Enock Charles**

VYAMA vya siasa nchini vimeeleza kushangazwa na kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa zilizotangazwa wiki iliyopita na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, kwa madai kuwa zina kasoro nyingi zinazotia shaka katika uchaguzi huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mrema, amedai kushangazwa na kanuni hizo kwa maelezo si rafiki kwa vyama vya upinzani.

"Kwanza niseme haijawahi kutokea ni kwa mara ya kwanza tunakuwa na kanuni za aina hii zenye kiwango kikubwa kabisa cha ukandamizaji kwa vyama vya upinzani," alisema na kuongeza:

"Kwa mfano kuna 'gape' kubwa kati ya siku ya mgombea kurejesha fomu tarehe 4 Novemba na siku ya kuanza kampeni tarehe 17 Novemba, kitu ambacho kinaleta shaka kubwa."

Alisema kutokana na muda mrefu kati ya siku ya kurejesha fomu na kampeni, ni rahisi kwa wagombea kuingia katika makosa ya kujisahau na kutoa kauli zinazoashiria kuwa wanafanya kampeni, hivyo kuwa katika hatari ya kuenguliwa.

Licha ya kuwapo kwa muda mrefu kati ya siku ya kurudisha fomu na siku ya kuanza kampeni, kiongozi huyo wa Chadema pia ameelezea kusikitishwa na namna serikali ilivyoweka muda mfupi wa siku 7 tu za kampeni tofauti na miaka iliyopita, akieleza kuwa muda huo hautoshi hasa kwa kuwa vyama vimezuiwa kufanya shughuli za siasa kwa miaka minne sasa.

### ACT YAFUNGUKA

Katibu Mwenezi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alidai serikali imetupilia mbali mapendekezo yao yote 21 waliyoyatoa katika uchaguzi huo, ikiwamo kuongezwa kwa muda wa kampeni kuwa mwezi mmoja badala ya siku saba kama ilivyo sasa na kudai siku hizo ni chache.

"Tulitoa mapendekezo 21 yote yametupwa hii inaonyesha kwamba vyama vya upinzani huwa vinatoa maoni ili kuonekana kwamba tumetoa maoni, lakini hayachukuliwi haiwezekani maoni yote hayo yakawa mabaya kwa serikali," Ado alisema.

Alidai zaidi kuwa serikali imeendelea na msimamo wake kuwatumia makatibu tawala kusikiliza rufani zote katika uchaguzi, jambo ambalo linaweza kuleta upendeleo katika rufani hizo kwa kuwa Makatibu Tawala hao ni wateule wa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi.

### KAULI YA CUF

Mkurugenzi wa Habari wa Chama cha Wananchi (CUF), Abdul Kambaya, amelalamikia kuwekwa kwa wakuu wa mikoa na wilaya katika uratibu na usimamizi wa shughuli za uchaguzi kwa madai kuwa viongozi hao ni wateule wa Rais, kwa hiyo upo uwezekano mkubwa wa kupendelea chama tawala.

Pia amelalamikia sharti la mgombea kuwa na kitambulisho cha Nida kama mbadala wa cheti cha kuzaliwa kwa madai kuwa kwa sasa watu wengi hawana vitambulisho hivyo, hivyo sharti hilo linawakwamisha wagombea wengi wa upinzani.

"Kuweka sharti la mgombea kuwa na kitambulisho cha Nida ni mpango wa kukwamisha wagombea wetu, kwa kuwa kwa sasa watu wengi hawana vitambulisho hivyo," Kambaya alisema.

### JAJI MUTUNGI

Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, amevitaka vyama vyote vya siasa kutii sheria zote na maelekezo ya uchaguzi huo ili kuendelea kudumisha amani nchini.

"Jukumu la vyama ni kutekeleza sheria na kuwa mawakala wa amani na amani inatakiwa kuendelea kutawala nchini kama ilivyo sifa ya nchi yetu, nina watakia uchaguzi wa amani," Jaji Mutungi alisema.

Akitoa tangazo la uchaguzi huo, wiki iliyopita Waziri Jafo alisema waangalizi wa uchaguzi huo wataruhusiwa baada ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Tamisemi siku 21 baada ya tangazo la uchaguzi kutoka.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




# Aua mke kwa shoka, wenye hasira kali wamchoma moto

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKAZI wa Kijiji cha Chiwata Kata ya Chiwata wilayani Masasi mkoani Mtwara, Juma Lugomba (61), ameuawa kikatili kwa kupigwa na mwili wake kuchomwa moto na wananchi wenye hasira kali baada ya kumuua mkewe kwa shoka.

Kutokana na kitendo hicho, wananchi hao walipandwa na hasira na kuamua kumkamata Lugomba kisha kumchoma moto hadi kufa.

Tukio hilo lilitokea katika kijiji cha Chiwata mwishoni mwa wiki na kuthibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee.

Mzee alisema inadaiwa kuwa majira ya saa 3:00 usiku, Lugomba alimshambulia mkewe, Yolenda Milanzi (59) kwa kitu chenye ncha mkali na kumsababishia majeraha ambaye yamemsababishia umauti baada ya kumjeruhi vibaya kichwani.

Alisema baada ya Lugomba kufanya mauji hayo, kundi la wananchi wenye hasira kali waliamua kumsaka na walipomkamata walimjeruhi kisha kumchoma moto hadi kufa.

"Ni kweli tukio hilo limetokea mume kumshambulia mkewe na kumuua, lakini baada ya yeye kufanya mauaji hayo asubuhi yake wananchi waliamua kumsaka mkazi huyo na walipomkamata walimjeruhi kisha kumchoma moto hadi kufa," alisema Mzee.

Alisema bado sababu za mauaji hayo hazijafahamika, lakini Polisi wanaendelea na uchunguzi juu ya tukio hilo licha mume huyo naye kuuawa na kundi la wananchi wenye hasira.

Aidha mkuu huyo wa wilaya ametoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia hatua mkononi badala yake wafuate sheria na kanuni na kwamba watuhumiwa lazima wafikishwe kwenye vyombo vinavyohusika.

Mtendaji wa kijiji cha Chiwata, Thawabu Mturi, Lugomba baada ya kufanya mauji hayo aliamua kukimbia na kwenda kijiji cha jirani cha Pemba kujificha ili kukwepa ushahidi.

Alisema wananchi walipogundua kuwa amemuua mkewe, walipandwa na hasira ndipo walipoamua kumtafuta wakiwa wamebeba silaha za jadi na walipogundua kuwa amejificha katika kijiji cha jirani, walimfuata huko na walifanikiwa kumkamata kisha walimchoma moto hadi kufa.

"Tukio kama hili ni la pili kutokea katika familia hii leo tumeambiwa na baadhi ya wanafamilia wa mke huyu kuwa miaka ya nyuma pia kuna mwanamke aliuawa na mumewe," alisema Mturi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, akizungumza na Nipashe jana baada ya kutopatikana kwa siku mbili, aliiambia Nipashe kuwa hadi jana hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kuhusiana na mauaji ya Lugomba.



Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Juu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Kennedy Hosea (wa pili kushoto), akikabidhi bendera ya taifa kwa baadhi ya Watanzania 30 waliopata ufadhili wa masomo ya shahada mbalimbali zikiwamo za umahiri na uzamivu nchini Hungary, chini ya ufadhili wa serikali ya nchi hiyo, wakati wa hafla ya kuwaaga iliyofanyika nyumbani kwa Balozi wa Heshima wa Hungary hapa nchini, Obedie Kimaro (kushoto), Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam juzi, usiku. **PICHA: JOHN BADI**

# 30 wapata ufadhili wa masomo

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA 30 wamepata ufadhili wa masomo ya shahada mbalimbali zikiwamo za umahiri na uzamivu nchini Hungary chini ya ufadhili wa serikali ya nchi hiyo.

Akizungumza wakati wa sherehe ya kuwaaga iliyofanyika juzi nyumbani kwa Balozi wa Heshima wa Hungary nchini, Obedie Kimaro, jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Juu nchini, Dk. Kennedy Hosea, alisema ufadhili huo ni hatua muhimu katika maendeleo ya elimu na rasilimali watu.

Dk. Obeid alisema wanafunzi hao wakiwamo wawili ambao watasomea shahada za uzamivu (Ph.D) watakuwa chachu katika maendeleo ya elimu na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Miongoni mwa fani zitakazosomewa na wanafunzi hao ni uhandisi umeme, uhandisi usalama na ubora wa chakula, utalii, udaktari wa binadamu na mifugo, mazingira na utalii.

Mkurugenzi huyo alisema fani hizo ambazo Watanzania wanakwenda kuzisomea, zina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi hasa viwanda na sekta ya utalii ambayo inapewa kipaumbele katika kuchangia pato la taifa.

"Kipekee tuwakumbushe Watanzania kuwa Hungary imechangia katika kuzalisha wasomi nchini na pia imepiga hatua katika masuala ya uhandisi na sayansi na teknolojia. Kama mtakumbuka kulikuwa na magari ya 'Icarus' ambayo yalikuwa maarufu sana nchini enzi za UDA. Magari haya yalitoka Hungary na hata sasa haya magari ya mwendokasi injini zake zimetoka Hungary," alibainisha.

# Sheria za barabarani kuangaliwa upya

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesema wizara ipo kwenye mchakato wa kuangalia upya sheria za usalama barabarani kwa lengo la kuziongezea makali ili kukabiliana na tatizo la ajali nchini.

Alisema lengo ni kukabiliana na watumiaji wa vyombo vya moto wakiwamo madereva wa pikipiki ambao wengi wao wamekuwa wakivunja sheria mara kwa mara na kusababisha ajali zinazoweza kuepukika.

Masauni aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akitoa zawadi kwa wanafunzi na shule za msingi zilizoshinda michoro yenye ujumbe wa usalama barabarani visiwani Zanzibar kwa mwaka 2019 katika mafunzo yaliyofadhiwa na Kampuni ya Mafuta ya Puma na Shule ya Msingi Mkunazini kushika nafasi ya kwanza na kukabidhiwa Sh. milioni nne.

"Ajali za barabarani zimeendelea kupungua siku hadi siku, lakini bado kuna changamoto ya baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto na hasa waendesha bodaboda wanavunja sana sheria za barabarani hawa tumeshawaundia mkakati.

"Tumeamua atakeyakamatwa kwa kuvunja sheria za usalama barabarani kwanza awekwe mahabusu na kisha apelekwe mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Wanavunja sheria kwa kuamini sheria sio kali sana, sasa tumeamua na tutawadhibiti ipasavyo kwa watakaoendelea kutoheshimu sheria zilizopo," Masauni alisema.

Alisema kuna umuhimu jamii ya Watanzania kwa upande wa Bara na Visiwani kuendelea kupatiwa elimu inayohusu usalama barabarani pamoja na matumizi sahihi ya barabara.

"Hivyo nitumie nafasi hii kuipongeza Kampuni ya Puma Tanzania kwa uamuzi wake wa kutoa elimu hii, kwa hapa Zanzibar shule tano za msingi zimepata elimu hiyo na tunaamini itasaidia kupunguza ajali ambazo zinaweza kuepukika," Masauni alisema.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




TAIFA STARS vs BURUNDI
SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA
HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# 2,000 kurejeshwa Burundi kila wiki

**Na Felix Mwagara,** KIGOMA

TANZANIA na Burundi zimesaini makubaliano ya kuwarejesha wakimbizi 2,000 kila wiki nchini mwao kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu.

Wakimbizi hao waliopo katika Kambi ya Nduta na Mtendeli, wanatarajiwa kusafirishwa nchi yao ya asili kutokana na kuwapo kwa amani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Waziri wa Mambo ya Ndani wa nchini Burundi, Pascal Barandagiye, wamesaini makubaliano hayo ambayo watahakikisha wakimbizi wote waliopo katika kambi hizo wanarejeshwa nchini mwao bila kukwamishwa na mtu au shirika lolote.

Akizungumza na waandishi wa habari, mjini Kigoma , Waziri Lugola alisema makubaliano hayo yataanza rasmi Oktoba Mosi na wakimbizi hao watakuwa wanarejeshwa nchini mwao na kupata mapokezi makubwa na serikali ya Burundi.

"Tuna taarifa wapo baadhi ya watu, mashirika ya kimataifa wanawarubuni wakimbizi wakiwatangazia kuwa Burundi haina amani, jambo ambalo si la kweli, nchi hiyo ina amani na wakimbizi wanapaswa kurejea nchini mwao," alisema Lugola.

Alionya kuwa, atawachukulia hatua kwa watakaokwamisha usafirishaji wa wakimbizi hao kwa kuwa Serikali ya Burundi inataka watu wao na Tanzania imeamua kuwapa ili waende wakaijenge nchi.

"Natoa kauli hii sio kuwatisha au kutishia nyau, bali nasema, serikali ya Magufuli haiwezi kuchezewa na mtu yeyote, hivyo tutawakamata wanaowarubuni, wanaowashawishi wakimbizi wasiende nchini mwao," alisema Lugola.

Wiki iliyopita, katika mkutano wa hadhara kambi ya Nduta, baadhi ya wakimbizi walisema wanawekewa vikwazo na kucheleweshwa na baadhi ya watendaji wa mashirika ya wakimbizi kambini humo wakati wanapoomba kujiandikisha kurejeshwa kwao.

Mkimbizi wa kambi hiyo, Nzoisa Bhainoje, alisema yupo tayari kurejea Burundi, lakini amefanya juhudi za kwenda eneo la kujiandikisha kambini hapo na hajafanikiwa kutokana na kusumbuliwa akiambiwa kuwa idadi wanaotakiwa kuondoka imekamilika.

"Nakumbuka nilifika eneo la kuondoka siku ya Jumanne, lakini ilishindikana kujiandikisha kutokana na kukwamishwa, wengi tunataka kuondoka tunashindwa kwa sababu tunakwamishwa," alisema Bhainoje.

Bhainoje alisema, wanaomba watendaji hao wawaruhusu wanaotaka kurejea nchini mwao kwa hiari, lakini kwa wale ambao

INENDELEA UK. 8

## Kuanzishwa safari ATCL China sasa kukuza utalii

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, amesema kuanzishwa kwa safari za ndege kutoka Dar es Salaam hadi China kutasaidia kuongeza utalii kwa kiwango kikubwa kwa kuwa Wachina wanasubiri kwa hamu.

Kairuki aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuzinduliwa kwa mitandao miwili ya China ambao utakuwa unatangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii (TTB).

Alisema bila ya kuwa na ndege ya uhakika, kuutangaza utalii ni changamoto kwa kuwa Wachina wanapenda kwenda katika nchi ambazo zina ndege za moja kwa moja kutokana na tatizo la lugha.

"Wakipita katika nchi nyingine inawalazimu wakae waanze kuzungumza, hii inakuwa ni changamoto, lakini shirika letu la ndege likianza safari zake kama kuanzia Kilimanjaro kwenda China au Dar es Salaam kwenda China itawavutia Wachina wengi na wanasubiri kuanza kwa ndege hiyo," alisema.

INENDELEA UK. 8




Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole (katikati), akikata utepe kuzindua majengo ya Shule ya Msingi Busisi, yaliyokarabatiwa kwa msaada wa benki ya TPB kwa gharama ya Sh. milioni 10.4, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, mkoani Mwanza juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Dk. Edmund Mndolwa (wa pili kushoto), Meneja wa benki hiyo, Sengerema, Joseph Fumbo (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPB, Sabasaba Moshingi (kulia), Mkuu wa Shule hiyo, Marco Dominic na Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Salum Kalli. **NA MPIGAPICHA WETU**


BANK OF TANZANIA

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MAGARI NA VIFAA VYA OFISI CHAKAVU – BENKI KUU TAWI LA ARUSHA TAREHE 31-08-2019**

Benki Kuu ya Tanzania Tawi la Arusha, imetoa idhini kwa **TAMBAZA AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kuuza kwa mnada wa hadhara Magari na Samani mbalimbali zikiwemo Samani za Ofisini na Majumbani zilizoorodheshwa hapa chini. Mnada utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 31/08/2019 kuanzia saa 03:00 asubuhi katika majengo ya Benki Kuu yaliyopo KIBLA Kitalu namba 565 Jiji la Arusha.

| NA. | AINA | NAMBA ZA USAJILI | AINA YA GARI | MWAKA ILIYOTENGENEZWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | GARI | SU 35970 | Land Cruiser | 2003 |
| 2. | GARI | SU 36506 | Land Cruiser | 2005 |
| 3. | SAMANI MBALIMBALI ZA OFISINI NA MAJUMBANI | | | |

**MASHARTI YA MNADA**

**A. MAGARI**

- Magari, yatauzwa kama yalivyo na mahali yalipo.
- Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer) na salio litalipwa katika kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada.
- Kiasi cha asilimia ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
- Mshindi atatakiwa kulipia ushuru na kodi nyingine ikiwa atanunua gari ambalo halikulipiwa ushuru/kodi kabla ya kuchukua gari hilo kutoka Benki Kuu ya Tanzania.
- Jukumu la kubadilisha umiliki wa Gari litakuwa ni la Mnunuzi mwenyewe.

**B. VIFAA VYA OFISI, VIYOYOZI, VITI, MEZA NA MASHINE ZA OFISI**

Vifaa hivi vitauzwa tarehe ya mnada kama ifuatavyo:

- Mnunuzi atatakiwa kulipa pesa yote mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the harmer). Mshindi akishindwa kulipa, kifaa hicho kitapigwa mnada upya mara moja
- Mnunuzi atatakiwa kuchukua kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo (cash and carry)
- Vifaa hivyo vitauzwa kama vilivyo na mahali vilipo.
- Haitaruhusiwa kwa kifaa/vifaa/samani yoyote iliyonunuliwa kubaki eneo la mnada

Magari pamoja na samani mbalimbali vinaweza kukaguliwa katika majengo ya Benki Kuu ya Tanzania yaliyopo Kitalu Na. 565 maeneo ya KIBLA Jijini Arusha. Ukaguzi utafanyika kuanzia tarehe 28 hadi 30 Agasti 2019 muda wa saa za kazi kuanzia saa 3 asubuhi mpaka saa 9 mchana.

**Mkurugenzi wa Tawi**
**Benki Kuu ya Tanzania - Tawi la Arusha**
**S. L. P. 3043**
**Arusha**


## Madiwani wacharukia 20%

**Na Gurian Adolf,** NKASI

SERIKALI wilayani Nkasi mkoani Rukwa imetoa siku 14 kwa halmashauri ya wilaya hiyo, iwe imetekeleza sheria ya kurejesha asilimia 20 ya makusanyo ya vijiji vyote katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Said Mtanda, alitoa agizo hilo jana baada ya madiwani wa halmashauri hiyo kulalamikia katika baraza lao kuwa fedha hizo hazijarejeshwa katika vijiji hivyo kwa muda mrefu hali inayosababisha ugumu wa utendaji kazi kwa viongozi wa serikali za vijiji na vitongoji.

Akitoa agizo hilo Mtanda alisema haoni sababu kwa nini halmashauri hiyo, iwe inavunja sheria na iachwe tu ikiendelea kufanya hivyo na ikizingatiwa fedha hizo zinatolewa ili ziwezeshe viongozi hao wa ngazi za vijiji na vitongoji kutekeleza majukumu yao ikiwamo kufanikisha ukusanywaji wa mapato zaidi.

Akizungumzia suala hilo hivi karibuni katika baraza hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki, Diwani wa Chala, Michael Mwanalinze, alisema asilimia 20 zimekuwa na mchango mkubwa katika shughuli za maendeleo katika vijiji vyao na kuwa kitendo cha fedha hizo kutorudishwa katika vijiji vyao kama ambavyo sheria inaelekeza, kunasababisha baadhi ya miradi inayotekelezwa na wananchi kutokamilika kwa wakati kwa kuwa wasimamizi hawana fedha za kufanya hivyo.

Philipo Kapembwa, Diwani wa Majengo alisema fedha hizo ni haki yao ya msingi kuzipata na haoni sababu yoyote ya kuziomba kama hisani kwani ni haki ya msingi ya wanaosimamia mapato hayo na yanapatikana kutokana na juhudi zao.

Diwani wa Nkomolo, Egid Ngomeni, alisema amekuwa akikerwa na kitendo cha fedha hizo kutorudi kwa wakati na kuwa wao kama madiwani wanataka fedha hizo zirudi haraka vinginevyo hawataelewana na halmashauri yao, kwani inawapa wakati mgumu wanapoulizwa na viongozi wa serikali za vijiji.

Kutokana na malalamiko hayo ndipo mkuu huyo wa wilaya alipoamua kuagiza kuwa fedha hizo zirudishwe mara moja katika vijiji na kutoa siku 14 ziwe zimevifikia vijiji vyote vya wilaya hiyo.

Awali Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Mhandisi Emmanuel Sekwao, alisema miongoni mwa mipango ya robo ya kwanza ya halmashauri hiyo ni kurejesha fedha hizo asilimia 20 za vijiji pamoja na kulipa madeni yote ya halmashauri, hivyo madiwani wasiwe na wasiwasi juu ya fedha hizo zitarejeshwa kwa wakati.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Zeno Mwanakulya, aliitaka halmashauri kutekeleza maagizo yote hasa hilo la kurejesha asilimia 20 katika vijiji haraka sana, vinginevyo baraza la madiwani halitaielewa halmashauri hiyo kama hali itakuwa hivyo na kuahidi kuwa katika kikao kijacho hapatakalika kama fedha hizo zitakuwa hazijarejeshwa.

TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

## TAARIFA KWA UMMA

## KUITWA KUANZA MAFUNZO YA STADI ZA KAZI KATIKA VYUO VYA DON BOSCO TANZANIA NA VYUO SHIRIKI

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu (OWM-KVAU) kwa kushirikiana na Taasisi ya Don Bosco Net Tanzania na vyuo Shiriki inapenda kuutaarifu umma wa Watanzania kuwa, vijana 5,875 wamechaguliwa kuanza mafunzo ya stadi za kazi kwa awamu ya kwanza kwa lengo la kukuza ujuzi, na kukidhi mahitaji ya soko la ajira nchini katika fani za useremala, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, uashi, utengenezaji wa kompyuta, uchongaji wa vipuri, kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji, ufundi magari, ufungaji wa umeme majumbani na viwandani, ufungaji umeme wa jua, mapishi na usindikaji wa chakula, uwekaji wa terazo na marumaru, ufugaji, kilimo cha matunda na mbogamboga, utengenezaji wa samani kwa kutumia aluminiam, ushonaji na uchapaji nyaraka.

Vyuo vitakavyotoa mafunzo ni Dar es salaam (Oysterbay VTC, Don Bosco Upanga na Don Bosco Temeke), Morogoro (Holy Cross Social Training Center), Kilimanjaro (Don Bosco Moshi), Shinyanga (Ola Sisters na St. Francis de Sales Technical Institute)), Dodoma (Don Bosco Institute), Arusha (Don Bosco KII- TECH), Mafinga (Don Bosco Seminary na Mafinga Parish), Musoma (St. Anthony VTC), Iringa (Don Bosco YTC), Singida (RC Mission VTC), Kagera (Kashozi Homecraft VTC), Geita (Geita VTC), Ruvuma (Peramio VTC), Lindi (Lindi RVTC).

Mafunzo yataanza rasmi katika vyuo vyote tarehe **02 Septemba, 2019** na yatatolewa kwa kipindi cha miezi sita. Vijana wote waliochaguliwa wanatakiwa kufika katika vyuo hivyo kuanzia tarehe 27 hadi 31 Agosti, 2019 kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kuanza mafunzo. Majina ya Vijana waliochaguliwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo za vyuo vilivyoainishwa na katika Tovuti ya www.kazi.go.tz na www.dbtz.org. Serikali itagharamia ada ya mafunzo pamoja na nauli wakati wa mafunzo ya shilingi 100,000/= (Laki Moja tu) kwa kijana kwa mwezi. Aidha, gharama nyingine za kujikimu zikiwemo malazi, chakula n.k zitagharamiwa na mwombaji au Mzazi/Mlezi. Aidha, tunapenda kuwataarifu vijana ambao waliomba na hawakufanikiwa kupata nafasi ya kuchaguliwa awamu ya kwanza kuwa watazingatiwa katika awamu ya pili ya mafunzo itakayoanza Machi, 2020. Orodha ya idadi ya vijana waliochaguliwa kwa fani kwa kila chuo ni ilivyoainishwa hapa chini :-

**ORODHA YA IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA KUANZA MAFUNZO KWA FANI NA KWA CHUO**

| NA. | CHUO | FANI | IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Don Bosco Oysterbay | Ufundi magari | 70 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 70 |
| | | Uchorongaji vipuri | 70 |
| | | terazo | 80 |
| | | Utengenezaji wa kompyuta | 80 |
| | | Useremala | 70 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 70 |
| | | Umeme wa jua | 90 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 160 |
| | | **Jumla Ndogo** | **760** |
| 2 | Don Bosco Upanga | Kutengeneza Kompyuta | 120 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 120 |
| | | **Jumla Ndogo** | **240** |
| 3 | Don Bosco Temeke | Utengenezaji wa kompyuta | 80 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 140 |
| | | Mapishi | 60 |
| | | **Jumla Ndogo** | **280** |
| 4 | Don Bosco Iringa | Utengenezaji wa kompyuta | 80 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 100 |
| | | Ufundi Bomba | 50 |
| | | Useremala | 50 |
| | | Terrazo na marumaru | 80 |
| | | Kutengeneza samani kwa aluminum | 80 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 50 |
| | | Uashi | 50 |
| | | Ufundi magari | 50 |
| | | Ufungaji umeme wa jua | 60 |
| | | Ufungaji umeme wa majumbani | 50 |
| | | **Jumla Ndogo** | **700** |
| 5 | Don Bosco Mafinga | Utengenezaji wa kompyuta | 100 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 80 |
| | | **Jumla Ndogo** | **180** |
| 6 | Don Bosco Dodoma | Uchorongaji Vipuri | 60 |
| | | ufundi magari | 60 |
| | | Ufundi bomba | 60 |
| | | Useremala | 60 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 60 |
| | | Uashi | 60 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 60 |
| | | Ufundi umeme wa jua | 90 |
| | | Mapishi ya vyakula na uhudumu | 180 |
| | | Terazo na marumaru | 90 |
| | | Utengenezaji wa kompyuta | 80 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 160 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1020** |
| 7 | Don Bosco Moshi | Utengenezaji wa kompyuta | 160 |
| | | ufugaji | 80 |
| | | Kilio cha matunda na mbogamboga | 80 |
| | | **Jumla Ndogo** | **320** |

**ORODHA YA IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA KUANZA MAFUNZO KWA FANI NA KWA CHUO**

| NA. | CHUO | FANI | IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA |
|---|---|---|---|
| 8 | Don Bosco Shinyanga (Ola Sisters) | Utengenezaji wa kompyuta | 60 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 50 |
| | | Usindikaji vyakula | 40 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 35 |
| | | **Jumla Ndogo** | **185** |
| 9 | Don Bosco KII TECH | Ufundi Komputa | 40 |
| | | Ufundi umeme wa jua | 40 |
| | | Ufundi Umeme wa majumbani | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **120** |
| 10 | St Franscis De Sales technical Institute | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 40 |
| | | Ufungaji umeme wa majumbani | 30 |
| | | Utengenezaji magari | 20 |
| | | **Jumla Ndogo** | **90** |
| 11 | Kashozi Home Craft VTC | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 40 |
| | | Mapishi | 40 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 40 |
| | | Utengenezaji kompyuta | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **160** |
| 12 | RC Mission VTC | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 30 |
| | | Mapishi | 30 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 40 |
| | | Utengenezaji kompyuta | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **140** |
| 13 | St. Anthony VTC | Ufundi umeme wa majumbani | 40 |
| | | Ufundi Magari | 40 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 80 |
| | | uashi | 40 |
| | | mapishi | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **240** |
| 14 | Holy Cross Social Training Centre | Ushonaji | 80 |
| | | Utengenezaji wa kompyuta | 60 |
| | | mapishi | 60 |
| | | **Jumla Ndogo** | **200** |
| 15 | Geita VTC | Ufundi umeme wa magari | 40 |
| | | ufundi wa magari | 40 |
| | | Ufundi bomba | 40 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 40 |
| | | Useremala | 40 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 40 |
| | | Uashi | 40 |
| | | Terazo na marumaru | 60 |
| | | Ufundi wa kompyuta | 40 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 60 |
| | | **Jumla Ndogo** | **440** |
| 16 | Peramio VTC | Uchapaji wa nyaraka (printing) | 40 |
| | | ufundi magari | 40 |
| | | Ufundi bomba | 40 |
| | | Useremala | 40 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 40 |
| | | Uashi | 40 |
| | | ufugaji | 40 |
| | | Ufundi wa kompyuta | 40 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **360** |

**ORODHA YA IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA KUANZA MAFUNZO KWA FANI NA KWA CHUO**

| NA. | CHUO | FANI | IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA |
|---|---|---|---|
| 17 | Lindi RVTSC | ufundi magari | 80 |
| | | Useremala | 40 |
| | | Ufundi umeme wa majumbani | 80 |
| | | Uchomeleaji na uungaji vyuma | 80 |
| | | Mapishi | 50 |
| | | Uashi | 60 |
| | | Ubunifu wa mitindo ya mavazi na Ushonaji | 50 |
| | | **Jumla Ndogo** | **440** |
| | | **JUMLA KUU** | **5875** |

**IMETOLEWA NA:**
**KATIBU MKUU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadhamini wanahitajika zaidi klabu Ligi Kuu Bara

**JUZI**, Jumamosi pazia la Ligi Kuu Bara lilifunguliwa rasmi kwa kuchezwa mechi tano katika viwanja tofauti nchini huku timu tatu kati ya hizo zikianza vizuri kwa kuvuna pointi tatu muhimu.

Katika Uwanja wa Kassim Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Namungo FC iliyopanda Ligi Kuu msimu huu ilianza vizuri kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ndanda FC, wakati miamba mingine inayoshiriki ligi hiyo kwa mara ya kwanza, Polisi Tanzania wakiwa uwanja wao wa nyumbani wa Ushirika wakishinda kwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union.

Biashara United ikiwa nyumbani Musomo ikakubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, wakati Mbeya City wakishindwa kutambiana na majirani zao Tanzania Prisons kwa kutoka suluhu.

Jijini Mwanza, majirani wengine Mbao FC walitoka sare dhidi ya 'Wapiga Kitabu', Alliance FC, hayo yakiwa matokeo ya juzi kabla ya ligi hiyo kuendelea hapo jana kwa Mwadui FC kuikaribisha Singida United.

Tofauti na msimu uliopita, ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imeanza ikiwa na Mdhamini Mkuu, Kampuni ya Vodacom.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilimtangaza rasmi mdhamini huyo siku moja kabla ya ligi hiyo kuanza rasmi juzi na kuleta matumaini mapya ya kwa bingwa sasa kuondoka na zawadi nono mbali na kombe.

Kutokana na kukosekana kwa mdhamini mkuu, msimu uliopita tumeshuhudia hadi sasa haijajulikana rasmi mabingwa, Simba watapewa zawadi gani mbali na kombe walilokabidhiwa.

Vodacom ambayo imekubali kuidhamini ligi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kwa gharama ya Sh. bilioni tisa, hakika ni ukombozi mkubwa kwa klabu zetu na soka la Tanzania kwa ujumla, kwa sababu si tu kutaongeza ushindani katika ligi hiyo, bali pia kutazipunguzia klabu gharama kubwa za kujiendesha hususan suala la nauli na hata mishahara kwa wachezaji.

Hivyo, Nipashe tunaipongeza Kampuni ya Vodacom kwa kuitika wito wa TFF kudhamini ligi hiyo, lakini pia tunaomba kampuni nyingine kujitokeza zaidi kwani milango bado ipo wazi kwa wadhamini wenza kuungana na kampuni hiyo.

Hata hivyo, si kwa kudhamini ligi hiyo tu, kwani wigo ni mpana zaidi hasa kwa kujitokeza moja kwa moja kuzidhamini klabu mojawapo ama hata zaidi ya moja kati ya 20 zinazoshiriki kinyang'anyiro hicho msimu huu.

Aidha, klabu nazo hazina budi kuingia sokoni kutafuta wadhamini wao binafsi jambo ambalo litaufanya huu wa jumla wa TFF kuwa kipato cha ziada kwao.

Lengo letu ni kuona ushindani ukiongezeka katika Ligi Kuu na ligi hiyo ikiendelea kuwa bora zaidi, na hilo litawezekana tu kama klabu zetu zitakuwa na wadhamini wenye nguvu za kuziondolea njaa wachezaji.


Tunaamini bado zipo kampuni nyingi hapa nchini na nje ya nchi zenye nia ya kudhamini Ligi Kuu ama klabu, hivyo ni suala la idara za masoko TFF na zile za klabu kujipambanunua zaidi kwa kuingia sokoni kusaka wadhamini.

Kadhalika, tunataka sasa kuona ushindani wa tija ukiongezeka katika ligi hiyo kwani kwa asilimia kubwa kero hususan kwa upande wa nauli kwa klabu, itakuwa imepungua kama si kumalizika.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Yanga, Azam, lengo liwe kulinda nafasi kwanza

Na Adam Fungamwango

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga na Azam FC zimefanikiwa kutinga hatua za raundi ya kwanza kwenye michuano hiyo.

Yanga imefanikiwa kutinga hatua ya Ligi ya Mabingwa kwa kuitoa Township Rollers kwa jumla ya mabao 2-1, ikitoka sare nyumbani na kushinda ugenini bao 1-0.

Azam yenyewe imetinga raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuisukumiza nje Fasil Kenema ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 3-2, ikifungwa bao 1-0 ugenini na kushinda mabao 3-1 nyumbani.

Huu ni mwanzo mzuri kwa timu za Tanzania ambazo ni mara ya kwanza kuwa na idadi ya timu nne kwenye michuano ya kimataifa.

Shirikisho la Soka Afrika (Caf), liliipa Tanzania nafasi nne badala ya mbili, hii ikichagizwa na Simba kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

Kwa kuanzia angalau timu mbili zimeshafanikiwa kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo na hii imekuwa ni faraja kwani kama timu za Tanzania zingetolewa ingekuwa ni kilio kikubwa.

Nasema kilio kwa sababu pamoja na kwamba Tanzania imeingiza timu nne, lakini haina pointi nyingi, hivyo inaweza kuengulia mwakani kuingiza idadi hiyo kama klabu hizo zikifanya vibaya.

Nyuma ya Tanzania kuna nchi kama Kenya na nyingine ambazo zinaifukuza nafasi hiyo, na kama klabu zao zikifanikiwa kufanya vema na sisi kufanya vibaya, tunaweza kuzidiwa pointi na mwakani kujikuta tukirudi kwenye idadi ya timu zilezile mbili.

Kuna baadhi ya nchi Afrika kama Misri, Congo DR, Algeria, Tunisia na nyingine timu za klabu zimekuwa zikifanya vema karibuni kila mwaka tangu zamani, hivyo hizi zina pointi nyingi mno na hata kama timu zao zote nne zitatolewa kwenye michuano kwa miaka mitatu, bado zitaendelea kupeleka wawakilishi wanne.

Tanzania ni moja kati ya timu ambazo ndizo za chini, zikiwa na pointi chache, hivyo kinachotakiwa ni klabu zetu kujituma na kujitahidi kusonga mbele ili kujazia pointi ambazo zitafanya nafasi ya timu nne kuendelea kuwa salama.

Nitoe pongeza kwa Yanga ambayo pamoja na matatizo kadhaa, kutofanya vema nyumbani na kuchukuliwa kuwa ndiyo kama vile imetoka, lakini ilipigana kufa kupona ugenini na kufanikiwa kusonga mbele, kuihakikishia Tanzania kuwa imo bado kwenye michuano hiyo.

Azam nayo baada ya miaka michache na kusuasusa imeonekana imerudi kivingine, nayo kwa jinsi ilivyo, pamoja na matunzo inayoyapata ina wajibu wa kufanya vema ili kuhakikisha mwakani Tanzania inapeleka tena timu nne.

Tukubaliane kuwa kutwaa Kombe la Afrika, au Kombe la Shirikisho kwa timu hizi si kazi rahisi, lakini sasa malengo yao yawe ni kutinga hatua ya makundi tu.

Lengo la hatua hiyo, si tu kuzifanya timu hizo kujiingizia kitita cha pesa kutoka Caf, lakini pia kuikusanyia nchi pointi ili mwakani Tanzania ipeleke kwa mara nyingine tena timu nne, lakini pia kuzifanya hata zile nchi ambazo zinatukaribia kuziacha kwa mbali.

Tanzania ikishakuwa na uhakika wa kuwa inaingiza timu nne karibuni kila mwaka ni faida kubwa kwani hata Ligi Kuu ya Tanzania inakuwa na ushindani, kwa kuwa timu hazigombei tu kuwa bingwa, lakini pia zinagombea nafasi nne za juu. Pamoja na pongezi, nitoe pia angalizo kuwa mechi za raundi ya kwanza hazitokuwa rahisi kama hizi.

Kwa hali hiyo kutakuwa hakuna timu inayokubali kufungwa kizembezembe, kwani kila moja itakuwa ikitafuta kuwamo kwenye nafasi nne za juu. Pamoja na pongezi, nitoe pia angalizo kuwa mechi za raundi ya kwanza hazitokuwa rahisi kama hizi.

Kwenye michuano hii kila raundi timu inayoingia inakuwa ngumu kuliko ya kwanza. Kwa maana hiyo timu za Yanga na Azam zisibweteke na badala yake zianze maandalizi ya mechi zinazofuata za raundi ya kwanza

# BARUA & MJADALA

## Tujengeeni daraja hili tulilolichangia

***Mhariri***

*MIMI ni mmoja kati ya wananchi wanaozikubali sana jitihada za Rais John Pombe Magufuli ya kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo kama mtu mmoja mmoja, lakini na kwa ustawi wa taifa la Tanzania kwa ujumla wake.*

*Aidha, ni mmoja miongoni mwa Watanzania walio wengi ambao wanaikubali sana dhana ya wananchi kuchangia maendeleo ya eneo lao pale walipo, kwa kushiriki kwenye miradi mbalimbali ya kujitolea nguvu kazi ama kuchangia fedha.*

*Ninafanya hivyo kwa sababu michango kama hiyo huwa ina faida za moja kwa moja kwetu sisi wananchi au hata kama si ya moja kwa moja, ina faida zake kwa mgongo wa nyuma kwa maana ya ama watoto na wajukuu wetu, kama siyo kwa jirani zetu.*

*Kunapokuwa na changamoto kwa mfano ya barabara ambayo wananchi wana uwezo wa kuilima au ya daraja ambalo wananchi wanaweza kubeba mawe au kuchangia kidogo fedha ili daraja la kuwasaidia liweze kujengwa, basi mimi huwa niko mstari wa mbele kushiriki.*

*Na ndiyo maana nimeshiriki kwa mapana sana katika kutoa michango mbalimbali iliyohusu kuchangia ujenzi wa zahanati katika kijiji chetu au ujenzi wa madarasa, nikielewa fika kuwa huo ni wajibu wa msingi kufanya.*

*Hata hivyo, Mhariri ninapokuja kupinga au kutokubaliana na aina hii ya uchangiaji wa nguvu kazi ama fedha kutoka kwa mwananchi ni pale ambapo michango hiyo inapoishia hewani, bila kutekeleza kilichokusudiwa.*

*Na ndicho kilichonifanya leo hii niandike barua hii kwako Mhariri, nikiwa mkazi wa Kinondo Mashariki, Kata ya Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.*

*Mimi pamoja na wakazi wenzangu wa wa Kinondo Mashariki, tulichangia shilingi 70,000 kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa daraja litakalorahisisha usafiri katika eneo la Mji Mpya.*

*Sasa hadi miaka imepita, na daraja hatuoni likijengwa huku viongozi wetu, kwa maana ya Mwenyekiti wetu wa Mtaa pamoja na diwani wetu wa Kata ya Mabwepande, wakiwa kimya kama vile hakuna kitu kilichofanyika.*

*Mhariri, hapa ndipo ninapokuja kupingana na aina hii ya uchangiaji kwa sababu tunapochanga kwa ajili ya maendeleo yetu, inapaswa tulichochangia kionekane na si vinginevyo.*

*Ninaomba basi kupitia kwako wahusika watueleze fedha zetu zilipo kwa kuwa hatuoni daraja likijengwa na tatizo bado lipo.*

***Mkazi Kinondo Mashariki, Dar***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# TFF katu isikubali rangi nembo ya mdhamini kuchakachuliwa

**Na Adam Fungamwango**

**SOKA** la Tanzania bado linapitia kwenye hatua ngumu sana. Nadhani huko mbele hata wajukuu wetu watakuja kujiuliza hivi hawa babu zetu kwa nini walikuwa wanafikiria vitu kama hivi.

Wakati dunia ya soka inatoka nyuma na kwenda mbele, Wabongo huwa tunapenda kurudi nyuma kule walikotoka wenzetu.

Klabu nyingi kwa sasa duniani zinasaka matajiri wawekezaji ili kuzifanya kuwa bora na kujiendesha, bado mpaka sasa kwenye karne hii ya 21, kuna watu wanaamini kuwa soka linaweza tu kuendeshwa na michango ya kawaida, na si kutafuta wawekezaji.

Ukishangaa ya Mussa utaona ya Firauni, leo hii bado timu zinaamini kuwa kuweka nembo yenye rangi tofauti na rangi rasmi ya klabu ni kosa kubwa. Ni uchuro.

Hizi ni fikra za kihafidhina. Wahafidhina ni watu ambao mara nyingi hawataki mabadiliko. Wao wanaamini kuwa kitu chochote kilivyo, kama walikikuta hivyo, basi kibaki hivyo hivyo. Hata siku moja huwa hawana fikra ya kufanya mabadiliko hata kama yana tija.

Nimemsikia Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, akisema hakuna timu yoyote itakayoruhusiwa kubadili rangi ya nembo ya mdhamini katika jezi.

Kauli hiyo imekuja kufuatia sintofahamu ya nembo ya mdhamini mkuu ambayo klabu ya Yanga imekuwa ikibadilisha kwa madai kuwa haiendani na utamaduni ya rangi rasmi ya klabu yake.

Kwa sasa Karia anasema kwa msimu huu, rangi ambayo itatumika kwa timu zote itasalia kuwa ileile nyekundu ambayo ndiyo nembo ya Kampuni ya Vodacom inayodhamini ligi hiyo. Akaongeza kuwa hatua za kisheria kwa atakayebadili rangi ya mdhamini zitachukuliwa.

"Mkataba wetu wa udhamini una masharti yake ambayo tunatakiwa kuyafuata na hatoruhusu yeyote kwenda kinyume nayo. Masharti hayo ni kama kitabu cha msahafu na kila mmoja anapaswa kuyafuata. Yeyote ambaye hatoyafuata tutamtoa kwenye familia yetu," anasema Karia.

Klabu zimelia sana msimu uliopita kuwa hazikuwa na mdhamini, lakini sasa amepatikana, hivyo haitakiwi tena kumletea masharti ambayo mengine hayana msingi wowote.

Kibiashara nembo ya kampuni yoyote au ya bidhaa yoyote huwa haibadilishwi chochote. Iwe rangi au kuifanya vyovyote vile.

Klabu ya Yanga mara nyingi imekuwa kwenye mizozo ya kubadili nembo za kampuni mbalimbali kwani si kampuni hii ya simu tu, hata miaka kadhaa nyuma ilitokea kwa kampuni moja ya bia.

Kwa bahati mbaya sana, TFF na kampuni hizo zote huko nyuma zilikubali siasa hizo na kuruhusu Yanga kubadilisha rangi kwenye nembo zake, kitu ambacho kwa kweli hakileti uhalisia.

Lakini sasa naona ni kama vile wameshtuka. Hawataki tena siasa, moja ya masharti ni kwamba nembo yake ibaki kama ilivyo kwa klabu zote. Imefika wakati viongozi wa klabu, wanachama na mashabiki wa klabu hizi kongwe wabadilike kifikra. Hivi majuzi niliwasikia baadhi ya wazee wa Simba wakipinga rangi ya jezi ya klabu hiyo.

Shirikisho la Soka Afrika (Caf) liliitaka Simba kuwa na rangi tatu tofauti, ya nyumbani, ugenini na nyingine huru ya akiba. Hili limelalamikiwa sana na wazee kwa madai utamaduni wa Simba ni kuwa na rangi mbili tu na si vinginevyo.

Ninavyojua mimi ni kwamba rangi zilianza duniani na klabu zikaanzishwa baadaye, hakuna klabu yenye hakimiliki ya rangi.

Lakini pamoja na hayo, nembo ya mdhamini haihusiani lolote na hili la rangi ya klabu, kinachowekwa pale ni tangazo tu la mdhamini na si vinginevyo.

Klabu za wenzetu Ulaya zinapiga hatua kubwa kwa sababu ya mambo kama haya. Wao wanachoangalia ni fursa tu ya kuingiza pesa na hawaangalii rangi au 'visababu' vingi vya ajabu ajabu vya kukwamisha maendeleo.

Wachezaji wa Yanga kuweka nembo ya mdhamini mkononi au begani, hakuwafanyi washindwe kucheza mpira. Na wala rangi ya nembo ya mdhamini haiifanyi klabu hiyo kuonekana kuwa imebadilisha rangi ya klabu.

Viongozi wa klabu ya Yanga wanapaswa waanze kutoa elimu kwa mashabiki wao ili kusiwe na malalamiko yasiyo ya lazima na kumfanya mdhamini akasirike na kujiondoa.

Natumaini viongozi wa Yanga watalifanyia kazi hilo kwani wao wakisema, wanachama na mashabiki hawatowapinga na hata ukiangalia huko nyuma, tatizo kubwa lilianza kwa viongozi wenyewe wa Yanga ndiyo walikuwa wakipinga na kuwafanya wapenzi wao kuwaunga mkono.

Kwa sasa kwenye soka cha kuangalia ni faida zaidi na si masuala yasiyo na msingi, kwani wakati mtu anapinga rangi ya mdhamini kuvaliwa, lakini wachezaji wa timu yake hiyo hiyo wanakuwa wamevaa viatu vya rangi hiyo hiyo, na hawawakatazi tofauti ya nembo iko wapi? Tuacheni uswahili usio na maana, soka letu lichanje mbuga.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**



# Mpina afagilia kampuni kwa zana bora za kilimo

Na Enock Charles

SERIKALI imeipongeza kampuni ya zana za kisasa za kilimo ya Agricom Africa, Tanzania Limited, kutokana na kuibuka na ushindi wa kwanza kitaifa katika eneo la zana bora na za kisasa za kilimo.

Iliibuka mshindi kwa kuleta zana za kisasa za kutengeneza vtakula vya mifugo katika maonyesho ya Nanenane hivi karibuni mkoani Simiyu.

Pongezi hizo zilitolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Luhaga Mpina, alipotembelea kampuni hiyo kujionea zana hizo, baada ya kumalizika kwa maonyesho ya Nanenane.

Waziri Mpina alisisitiza kuwa mapinduzi ya kweli ya kilimo yataletwa na kilimo kinachotumia zana bora na za kisasa, mbegu bora, pembejeo za kilimo na utaalamu wa kisasa wa kilimo, hivyo kubadili kilimo kutoka cha kujikimu hadi kilimo biashara.

Alisema hata katika sekta ya mifugo, ufike wakati chakula cha mifugo nacho kitayarishwe kama ilivyo kwa vyakula vya binadamu, hivyo kampuni hiyo imeleta vifaa vya kukata majani na kuyafunga kwa ajili ya chakula cha mifugo.

Waziri Mpina alitoa wito kwa halmashauri zote nchini, kununua mashine za kisasa za kilimo na malisho ya mifugo na kutayarisha mashamba darasa ya kuwafundishia wakulima kwa mifano, ili wakulima waone faida za matumizi ya zana bora na za kisasa za kilimo, na kwa upande wa mifugo.

Alisema mashine kama hizo, zinaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya wakulima na wafugaji, kwa wafugaji kuandaa malisho ya mifugo yao zaidi ya kuiachia ikizagaa zagaa na hatimaye kula mazao ya wakulima.

Aliitaka kampuni hiyo kusambaza zana hizo kuwafikia wakulima na wafugaji nchi nzima na kuleta vipuri, kushauri halmashauri zote nchini kuwahamasisha wakulima na wafugaji kujiunga katika vikundi ili kuweza kukopesheka, wakopeshwe hizo zana bora na za kisasa ili kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo chetu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Agricom, Angelina Ngalula, aliahidi kampuni yake kuendelea kushirikiana na serikali katika kuunga mkono juhudi za serikali kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kutumia zana bora, na katika kutimiza hilo, tayari kampuni hiyo imeishafungua ofisi katika kanda mbalimbali nchini.

Ili kuwafikia wakulima, kampuni hiyo imeshiriki maonyesho ya Nanenane katika kanda tano tofauti, wakianzia Arusha, Mbeya, Dodoma, Morogoro na Nanenane Kitaifa Nyakabindi, Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, ambapo kampuni hiyo imetwaa zawadi ya kwanza kitaifa katika kampuni za zana za kisasa za kilimo.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya zana za kilimo ya Agricom, Angelina Ngalula, akizungumzia kauli mbiu ya Agricom ambayo ni 'Toboa utokee shamba'. Kampuni hiyo ilitwaa ushindi wa kwanza kitaifa kwa kampuni za zana za kilimo mwezi huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kutumia ardhi ya bandari

Na Enock Charles

DIWANI wa Kata ya Zinga iliyopo Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, Mohamed Mwinyigogo, ameiomba serikali kuwaruhusu wananchi pamoja na mamlaka za serikali za mitaa na vijiji kuitumia ardhi iliyokuwa itumike kwa ajili ya mradi wa Bandari ya Bagamoyo katika shughuli za maendeleo kwa kuwa sasa mradi huo umeahirishwa.

Akizungumza katika mahafali ya kwanza ya Shule ya Msingi Mazzoldi, diwani huyo amebainisha kuwa licha ya mradi huo kuahirishwa, lakini bado ardhi iliyokuwa itumike katika mradi huo imeshikiliwa na mamlaka ya ardhi kwa maelezo kwamba ni kwa ajili ya matumizi ya mradi huo.

"Ardhi yetu ya Zinga ina changamoto kubwa sana kwa sababu imetwapini... wafadhili wanaotaka kutujengea shule wakienda katika mamlaka ya ardhi wanaambiwa ni eneo la mradi na tunauhitaji wa maeneo kwa sababu kata ya Zinga ina wageni wengi," Mwinyigogo alisema.

Diwani huyo alibainisha kuwa mradi huo ulitarajiwa kuhusisha vijiji vinne vya kata hiyo ambavyo ni Kijiji cha Zinga, Pande, Kondo na Mlingotini na kwamba kushikiliwa kwa ardhi hiyo kunakwamisha kufanyika kwa shughuli za kimaendeleo ikiwamo ujenzi wa shule.

"Kwa mfano kuna bwana mmoja anaitwa Luta ana heka 15 anataka kujenga shule kubwa ya vipaji, lakini akienda ardhi anaambiwa nenda eneo la mradi kwa hiyo ana rudi nyuma," Mwinyigogo alisema.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Sister Aquila Tarimo, akizungumza katika mahafali hayo alisema shule hiyo ilianza mwaka 2009 kwa kutoa elimu ya awali pekee na kwa sasa ina uwezo wa kupokea wanafunzi zaidi ya 700 wa elimu ya darasa la kwanza mpaka la saba na wanafunzi 300 wa elimu ya awali.

"Shule hii ilianza kwa hatua ya chekechea mwaka 2009 na miaka minne baadaye ilianza kutolewa elimu ya msingi na tuna mpango wa baadaye kuongeza madarasa ya sekondari," Tarimo alisema.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Sister Eutropia Shirima, aliwataka wadau kujitokeza kuchangia shule hiyo ili kuongeza madarasa ya sekondari kwa kuwa tayari imeonyesha mfano mzuri kwa elimu ya msingi na ya awali.

# 2,000 kurejeshwa Burundi kila wiki

INATOKA UK. 4

hawataki kuondoka wanaweza kubaki kwa mipango yao.

Baada ya wakimbizi hao kutoa kero zao kwa Lugola na Waziri Barandagiye, Lugola aliagiza kufanyika uchunguzi katika kambi hiyo kuwakamata wote ambao wanaokwamisha wakimbizi hao kurejea nchini kwao kwa hiari.

"Naagiza uchunguzi ufanyike haraka iwezekanavyo kwa yeyote atakayehusika anakwamisha kuwarejesha wakimbizi hawa ambao wapo tayari kuondoka nchini kwao kutokana na amani iliyopo, awe ofisa kutoka wizarani, awe ofisa wa shirika lolote, awe yupo hapa kambini, lazima tutamkamata na kumpeleka mahakamani," alisema Lugola.

Aliongeza kuwa, muda umefika kwa wakimbizi wa Burundi kurudi nchini mwao, kwa kuwa sababu zilizokuwa zinazuia kuwarudisha kwa sasa hazipo na nchi hiyo ina amani.

"Wanaosema Burundi haina amani wanaipaka matope nchi hiyo kwa kuwa jambo hilo halina ukweli wowote na Tanzania imefanya uchunguzi wa kutosha na kujiridhisha kuwa amani ya kudumu ipo nchini humo, Oktoba Mosi tutaanza kutekeleza mkataba wa pande tatu wa kurudishwa kwa wakimbizi 2000 kila wiki wa Burundi kwenda nchini mwao," alisema Lugola.

# Kuanzishwa safari ATCL

INATOKA UK. 4

Kairuki alisema watakapoona matangazo wawe na uelewa jinsi ya kufika Tanzania, hivyo ikiwapo ndege ya kufika hadi China itawasaidia.

Kairuki alisema Tanzania inafahamika katika masuala ya utalii kwa upande wa Serengeti na Ngorongoro bado kuna maeneo mengine hayajafahamika na yanahitajika kutangazwa.

Alisema mtandao wa Baidu unatumika China pamoja na nchi nyingine duniani, hivyo itaitangaza nchi na watu wengi kuona utalii wa Tanzania.

"Hii ni fursa ya kujitangaza lengo letu ifikapo mwakani kuongeza idadi hadi kufikia watalii 50,000 na ifikapo mwaka 2025 tuwe tunapokea watalii zaidi ya 100,000 kutoka nchini China na hii inawezekana kwa kuwa serikali imefanya jitihada kubwa katika masuala ya utalii," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya TTB, Richard Rugimbana, alisema tukio la kampuni mbili za China kuamua kuja kuitangaza Tanzania ili waweze kupata vitu vya utalii vizuri wakavitangazwe nchini kwao ni la kihistoria.

Alisema kutangazwa kwa vivutio vya Tanzania katika mitandao hiyo itawawezesha Wachina kufahamu vitu vilivyopo nchini na kuongeza utalii.

Mhadhiri wa Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Mawasiliano ya Habari ya China, Maria Lee, alisema kutangaza vivutio katika mtandao huo wa Baidu kutasaidia kufahamika kwa utalii uliopo Tanzania ili Wachina wahamasike kuja kuvitembelea.

Alisema kuna timu ya wafanyakazi 12 wa mtandao huo wamewasili nchini kwa ajili ya kupiga picha za maeneo ya vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kwa ajili ya kuwaonyesha Wachina.

# Simbachawene azitaka mamlaka kupanga matumizi bora ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, ameliagiza Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kushirikiana na mamlaka zinazohusika na ardhi kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuepuka uharibifu wa mazingira unaotokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu.

Waziri Simbachawene alitoa agizo hilo alipokutana na wataalamu wa mkoa wa Iringa kujadili namna mkoa ulivyojipanga katika suala la utunzaji wa mazingira na kuagiza mamlaka husika kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi utakaosaidia kuondoa tatizo la uharibifu wa mazingira.

"Halmashauri zote nchini zijielekeze kwenye kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi utakaosaidia usimamizi mzuri wa ardhi kulifanya zoezi la usimamizi wa mazingira hapa nchini kuwa rahisi kutokana na mpango wa kila eneo kukamilika na kutekelezwa," alisisitiza.

**Nguvu kubwa inatumika na wasimamizi wa sheria na kanuni za mazingira kuadhibu jamii ijapokuwa miundombinu ya matumizi ya ardhi haijawekwa sawa.**

Alisema mazingira yanagusa maisha ya kila mtu katika eneo lake, hivyo ni muhimu kutenga maeneo kulingana na mahitaji jambo litakalosaidia kutoa mwongozo kwa jamii juu ya utunzaji wa mazingira kinyume na ilivyo sasa.

"Nguvu kubwa inatumika na wasimamizi wa sheria na kanuni za mazingira kuadhibu jamii ijapokuwa miundombinu ya matumizi ya ardhi haijawekwa sawa," alisema Simbachawene.

Aliongezea kuwa NEMC ishirikiane na halmashauri na mamlaka zilizopo nchini kuandaa na kufanya utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuwaweka wananchi katika ya kujisimamia katika utunzaji wa mazingira kulingana na mpango utakavyokuwa.

Aliwataka watendaji wa NEMC na taasisi zote nchini kupitia sheria zinaongoza mamlaka nyingine ili kuepuka mwingiliano wa majukumu na pia zitawasaidia katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisema elimu ya mazingira hasa kwa wakati huu, ambapo serikali imejielekeza kwenye ujenzi wa viwanda ni muhimu ikaendelea kutolewa zaidi.

"Ili kutekeleza azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 ni lazima kushirikiana katika kutelekeza majukumu hasa katika usimamizi wa matumizi bora ya ardhi na utunzaji wa vyanzo vya maji ili utekelezaji wa miradi mbalimbali isikwamishwe," alisema Hapi.

Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu, alisema maagizo na mapendekezo yote wameyapokea na wataisimamia menejimenti kuyatekeleza ili suala la mpango wa matumizi bora ya ardhi liweze kutekelezwa.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri, jijini Dar es Salaam, Gladius Ndyetabura, akikabidhi cheti cha pongezi kwa Alex Matata ambaye ni mmoja wa wanafunzi wa darasa saba waliofanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya mtihani wa majaribio (Mock), katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, mwishoni mwa wiki, ambapo shule hiyo, imeongoza kwa Wilaya ya Ubungo na kutoa wanafunzi sita katika 10 bora. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapigiwa debe nafasi uongozi

**Na Joseph Mwendapole**

MATOKEO ya utafiti mbalimbali yanaonyesha wanawake wakipewa nafasi za uongozi huleta matokeo chanya kwa sababu ya uchapakazi wao, lakini changamoto ni utayari wao wa kujitokeza katika mapambano ya kisiasa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Wakili Clarence Kipobota wakati akiwasilisha mada ya nafasi ya wanawake katika uongozi na ngazi za maamuzi kwenye mkutano ulioandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF).

Kipobota alisema kuna umuhimu kwa serikali na wadau wote kuangalia uwezekano wa kutengeneza mfumo maalum wa kuwawezesha wanawake kiuchumi ili waweze kushiriki kwenye nafasi za uamuzi na uongozi kwani wanazimudu.

Alisema katika vyama vya siasa mifumo ya upatikanaji wa nafasi za uongozi wa kisiasa bado ni changamoto kubwa, na kwamba bado ni vigumu kwa wanawake kuweza kupenya na kupata nafasi za uongozi.

Alisema kwa takwimu za kisiasa kwenye chaguzi za mwaka 2015, ni asilimia 23.3 tu ya wanawake walioshinda kwenye majimbo ya uchaguzi nchini, na kusema kuwa: "Hii inathibitisha kuwa wanawake wakipewa nafasi wanaweza kuleta matokeo chanya kwenye jamii na uongozi wa nchi kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna kulaya, alisema mchango wa wanawake katika harakati za uhuru na ukombozi Afrika ni kubwa na ni muhimu kuendelea kudumishwa.

"Sote tunajua jinsi gani hapa nchini mwanamke kama Bi Titi Mohammed alivyoshiriki kikamilifu katika harakati za uhuru wa nchi yetu na ni mwanamke wa kuigwa kwa kusimama imara katika kutetea ukombozi wa mtu mweusi na kukomesha ukoloni hapa nchini," alisema Kulaya.

## Teknolojia yapaisha uzalishaji ndizi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya wakulima wa ndizi Kata ya Izimbya Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera wameeleza mafanikio ya ongezeko la mavuno kutokana na kutumia teknolojia iliyotolewa na watafiti.

Watafiti hao ni kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Kituo cha TARI Maruku kwa kushirikana na wilaya hiyo.

Wakizungumza mwaka mmoja tangu kupokea elimu ya kilimo tija, Yazid Salum, alisema mafanikio ya mavuno ni kutokana na ufuatiliaji wa elimu ya kitaalamu katika kutunza shamba kwa kuongeza uboreshaji.

Winfrida Jonas, alisema, aliweza kutumia mbinu za kitaalamu zenye kutega wadudu waharibifu na kujipatia mabadiliko ya ustawi wa migomba yake hadi kuzalisha mikungu ya ndizi kuanzia 15 hadi 20 kwa wiki.

Ofisa kilimo wa Wilaya ya Bukoba, Muganyizi Kasige, alisema baada ya wakulima kutambua umuhimu wa teknolojia ya ongezeko la ndizi lilifikia tani 25 kutoka 10.

Kagise alisema, kata zilizofikiwa ni Kyaitoke, Kaibanja, Ruhunga, Rubare, Kikomero, Muganjwale na Izimbya, ambazo zilikuwa zimeathiriwa na changamoto ya mnyauko.

## Wakazi Mwanza wapata fursa maji

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (Mwauwasa), imeanza kutekeleza mradi mdogo wa maji ya bomba katika kata za Kisesa na Bujora wilayani Magu mkoani Mwanza.

Meneja msaidizi miundombinu, Stanley William, amesema jana jijini Mwanza, kuwa mradi huo unakadiriwa kugharimu kisi cha Sh. milioni 460, unaotarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa.

"Tayari tumeshaanza kutekeleza mradi mdogo wa maji katika kata za Kisesa na Bujora mwezi huu, ili kupunguza changamoto kubwa ya maji inayowakabili wananchi hao, unaokadiriwa kugharimu kiasi cha Sh. milioni 460 ambao utatokea Butimba kupitia Igoma na Nyamhongolo jijini hadi Kisesa," alisema William.

Meneja huyo alisema utekelezaji wa mradi huo kwa haraka ni kufuatia agizo la Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alilolitoa hivi karibuni katika kata hizo alipokuwa kwenye ziara yake mkoani Mwanza.

Sarah Mathias, mkazi wa Kata ya Kisesa, alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya maji, na wanalazimika kuamka usiku wa manane kwenda kusaka maji kwa kupanga foleni jambo ambalo linawaumiza kulingana na mahitaji ya maji.

# Jukata yashinikiza kanuni Sheria ya Vyama vya Siasa

**Enock Charles na Maria Magili**

JUKWAA la Katiba Tanzania (JUKATA) limeiomba serikali kutangaza kanuni zitakazotumika katika Sheria ya Vyama vya Siasa iliyopitishwa Februari 2, mwaka huu ili kuwezesha vyama kuzielewa vizuri kanuni hizo kabla ya uchaguzi mkuu mwakani.

Akizungumza na waandishi wa habari na wadau jijini Dar es Salaam, mwenyekiti mstaafu wa jukwaa hilo, Deus Kibamba, alisema mabadiliko waliyopendekeza katika sheria hiyo, mengi yamepitishwa na kuwa kinachosubiriwa sasa ni kanuni zitakazitumika katika sheria hiyo.

"Sheria tayari ipo, lakini bado hatuna kanuni maana baada ya kutungwa sheria kinachofuata ni kanuni ndio kinachosubiriwa sasa na imekuwa muda mrefu kweli," Kibamba alisema.

**Sheria tayari ipo, lakini bado hatuna kanuni maana baada ya kutungwa sheria kinachofuata ni kanuni ndio kinachosubiriwa sasa na imekuwa muda mrefu kweli.**

Akizungumza na Nipashe kwa simu jana kuhusu wito huo wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata) Msajili wa Vyama vya Siasa nchini , Jaji Francis Mutungi, amesema ni kama mchezo wa kuigiza kwa kuwa jukwaa hilo lilishapeleka kesi mahakamani kuhusiana na sheria hiyo.

"Ni kama mchezo wa kuigiza kwa sababu wao walishafungua kesi mahakamani, halafu bado wananialika tuijadili," Jaji Mutungi alisema.

Katika mkutano huo uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, jukwaa hilo lilimtangaza Bob Wangwe kuwa mkurugenzi mtendaji wake, akichukua nafasi ya Diana Kidala. Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Hebron Mwakagenda, alimtaka mkurugenzi huyo kuzingatia maadili na uzalendo katika kuongoza jukwaa hilo.

"Tuna imani naye sana kwa kuwa yeye ni kijana zaidi, hivyo jukwaa litakimbia na kuzidi kuimarika zaidi kwa kupata mawazo bora," Hebron alisema.

Akizungumza baada ya kutangazwa, Wangwe alisema lengo kubwa la jukwaa hilo kwa sasa ni kuhakikisha wanatetea makundi ya vijana, walemavu na kinamama katika ushiriki wa shughuli za kisiasa.

"Tunataka utetezi wa makundi ya watu wenye ulemavu, vijana na wanawake kushiriki katika shughuli za kisiasa," Wangwe alisema.

Kibamba alitaja baadhi ya vipengele vilivyobadilika katika sheria hiyo kutokana na maoni na mapendekezo yao ikiwamo vyama kuzingatia makundi ya vijana, walemavu na wanawake katika uteuzi wa wagombea.

Pia kuruhusiwa kwa ushirikiano wa vyama vya upinzani kabla na baada ya uchaguzi vyenye malengo yanayofanana kama vile Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) katika kufanya shughuli za siasa.

Mdau, Stella Jailos kutoka Sauti ya Wanawake wenye ulemavu Tanzania (SWAUMA), alisema walemavu hawapatiwi kipaumbele kwenye uteuzi wa wagombea katika vyama na badala yake wanasubiri kupewa nafasi maalumu bungeni.

"Vyama vya siasa vinatakiwa kuwaamini walemavu na kuwapatia nafasi ya kugombea kama watu wa kawaida," Stella alisema.

Aliiomba serikali kuwapatia kipaumbele walemavu kwa kuwapatia vifaa mbadala na rafiki wakati wa kupiga kura ili wachague mtu ambaye wamemchagua wao na sio kusaidiwa kupiga kura kama ilivyo sasa.

# Wito masheha kuwasimamia wasioona

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MASHEHA wa Wilaya ya mkoani Pemba, wametakiwa kuwasimamia watu wenye ulemavu kupata haki zao za msingi sawa na wananchi wengine katika jamii.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa Jumuiya ya Wasioona Wilaya ya Mkoani utakaosimamia umiliki wa ardhi kwa wasioona, Mkuu wa Wilaya hiyo, Issa Juma Ali, alisema, si vyema watu wenye ulemavu kudharauliwa na kutengwa kwa sababu ya hali zao.

Alisema kuwa watu wenye ulemavu wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kukosa mahitaji yao muhimu, hivyo ni vyema kwa masheha wa shehia za wilaya hiyo, kusimamia upatikanaji wa haki zao za msingi ambazo wamekuwa wakizikosa ndani ya jamii.

Aidha, aliwataka wanachama wa Jumuiya ya Wasioona na jamii kwa ujumla kutuumia mradi huo kama ufunguo wa kutatulia matatizo kadhaa yanayowakabili watu wasioona.

"Hii ni fursa muhimu kwenu, tubadilike ili kuleta maendeleo zaidi, tuendeleze vikundi vyetu baada ya miradi kumaliza muda wake na sio kuivunja," alisema.

Meneja wa mradi huo, Massoud Suleiman Daud, alisema mradi huo utatekelezwa katika shehia zote 36 za Wilaya ya Mkoani, hivyo ni jukumu la masheha kuwahamasisha wenye ulemavu kuunda vikundi katika shehia zao, ili wanufaike na mradi huo.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Wilaya ya Mkoani, Ali Hemed Khalifa, alisema ushirikiano wa dhati unahitajika kwa serikali na jamii kwa ujumla, ili kufanikisha lengo walilokusudia wanajumuiya hao.

Mradi huo wa miezi nane (8) unatekelezwa na Jumuiya ya Wasioona Wilaya ya Mkoani Pemba, chini ya ufadhili wa Foundation for Civil Society.



Mchuuzi wa sambusa akisubiri wateja bila kuzifumika katika kituo cha mabasi cha Uwanja wa Karume, Ilala jijini Dar es Salaam wikiendi, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: JOHN BADI**

# Kampeni mpya kulinda watoto

**Na Yasmine Protac**

TGNP Mtandao imetambulisha kwa vyombo vya habari kampeni yake ya 1_5_5 ambayo inalengo la kumlinda mtoto dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia na wa kingono.

Hayo yalisemwa na mwezeshaji wa Mtandao huo, Gema Akilimali, wakati alipokuwa anaitambulisha kampeni hiyo kwa vyombo vya habari. Alisema malengo ya kampeni ya '1_5_5 namlinda', itasaidia kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto katika matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Mtakuwa ni mpango wa serikali ambapo lengo lake ni kupunguza ukatili kwa watoto ifikapo mwaka 2020 kwa kupunguza kwa asilimia 50," alisema.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo ya 1_5_5 namlinda inaipa nafasi jamii kutengeneza ulinzi kwa watoto ndani ya nyumba na nje ya shule. Alisema kampeni hiyo inaongeza uelewa wa ulinzi kwa wasichana na wavulana kuelewa bayana taratibu za kutoa taarifa za kingono.

Alisema takwimu za utafiti ya afya ya uzazi na mtoto zinaonyesha ukatili wa kingono unaongezeka. "Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu zinaonyesha takwimu za mwaka 2018 wastani wa watoto 394 kila mwaka wanabakwa," alisema.

# Viongozi dini waombwa kukemea mmomonyoko

**Na Sabato Kasika**

VIONGOZI wa dini wameombwa kusaidia kukemea mmomonyoko wa maadili katika jamii, ili kusaidia kupunguza vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikiendelwea kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Wito huo ulitolewa na Ofisa Elimu ya Msingi wa Wilaya ya Temeke, Mectilda Rukoijo, kwenye warsha ya kujifunza mkakati wa mawasiliano ili kuzuia ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Alisema mmomonyoko wa maadili kwa vijana, hasa wanafunzi wa shule za msingi usipothibitiwa kikamilifu utasababisha madhara makubwa ikiwamo kuwa taifa la baadaye lisilo na maadili.

"Pamoja na kwamba juhudi mbalimbali za kukomesha vitendo vya ukatili zimekuwa zikifanyika kwa kufikisha kwenye vyombo vya dola, lakini ninawaomba viongozi wa dini wasaidie sana," alisema Rukoijo.

Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Temeke, Bridgeter Pilla, alisema wazazi na walezi hawawezi kukwepa lawama yanapojitokeza matatizo kama hayo ya watoto kulawitiana. Aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao ili kujua mienendo yao na kuwakemea au kuwachukulia hatua pale wanapobaini kwamba wanafanya mambo yasiyotakiwa.

# Wataalamu wa macho wafundwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATAALAMU wa macho nchini wametakiwa kwenda maeneo ya pembezoni ili kutoa huduma kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo, hususan jamii za kifugaji ambazo zinakabiliwa na ukosefu wa lishe bora pamoja na wadudu aina ya nzi na mbung'o kutokana na mazingira wanayoishi.

**Naamini endapo ugonjwa huu ukidhibitiwa asilimia 80 ya upofu hutibika, kulingana na takwimu za Shirika la Afya ulimwenguni (WHO).**

Akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa kongamano la 20 la kisayansi la wataalamu wa macho (Optometria), Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini wanakabiliwa na changamoto kubwa ya matatizo ya macho, kutokana na mazingira wanayoishi hivyo ni vyema sasa madaktari wa macho kwenda maeneo ya pembezoni kuwatibu wagonjwa hao.

Muro alisema wataalamu hao wa macho wanatakiwa kuweka mikakati itakayowezesha kada hiyo kutambuliwa kwa utoaji wa huduma za macho na kufanya upasuaji kwa kutambulika kitengo chao.

Alisisitiza kuwa endapo wataalamu hao watazifuata jamii hizo vijijini zaidi na kutibu matatizo ya macho ikiwamo uono hafifu unaotokana na maeneo wanayoishi, itawasaidia wananchi hao ambao wengi wao wanakumbwa na tatizo hilo.

"Lazima sasa muende vijijini ili kutatua changamoto za magonjwa ya macho, kwa kuwa wananchi wa vijiji wanateseka sana na matatizo ya macho," alisema.

Pia alisema lazima waangalie jinsi ya kudhibiti wanaouza miwani ya jua au ya macho ambayo haijathibitishwa na madaktari, kwa kuwa imekuwa tatizo kubwa kwa watu kuvaa bila ushauri wa daktari wala kununua sehemu sahihi.

"Ukimuuliza mtu hii miwani ya jua au ya kusomea hupati jibu tena inauzwa Sh. 700 hadi Sh. 1,500 kwa wafanyabiashara ndogo ndogo, hivyo ni lazima mdhibiti suala hilo," alisema.

Naye Rais wa Chama cha Wataalamu wa macho nchini, Anna Germanus, alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaa tiba, kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa macho kutokana na hospitali nyingi kuwa na wataalamu wa macho bila vifaa tiba.

Pia alitoa rai kwa serikali kuangalia suala hilo, ili waweze kutoa huduma hiyo za macho badala ya kukaa hospitali bila wagonjwa wa macho.

"Naamini endapo ugonjwa huu ukidhibitiwa asilimia 80 ya upofu hutibika, kulingana na takwimu za Shirika la Afya ulimwenguni (WHO)," alisema.

Aliomba wananchi kuwa na utaratibu wa kupima macho mara moja kwa mwaka ili kupata huduma bora za macho endapo watagundulika kuwa na matatizo hayo macho ikiwamo mtoto wa jicho ambao huwakumba zaidi watu wenye umri mkubwa.

## Barabara mbovu zawakera wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI wa Kijiji cha Sokoni 2 katika Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, wameomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) kukarabati kipande cha barabara kutoka Kimandolu kuelekea kijiji hicho, baada ya kuwa tishio la usalama wa wananchi na magari.

Ombi hilo limetolewa jana na Mwenyekiti wa kijiji hicho, Obedi Melami, baada ya barabara kutoka eneo la Kimandolu mita 200 katika halmashauri ya jiji, kuelekea kijiji cha Sokon2 wilayani Arumeru, kutopitika na kusababisha usumbufu kwa madereva wa magari na watembea kwa miguu hasa nyakati za usiku.

Melami alisema, eneo hilo kutoka usawa wa barabara limesahaulika kwa muda mrefu, baada ya kuharibiwa na mvua na kutengeneza korongo refu ambalo limekuwa tishio.

"Eneo hilo limekuwa korofi na tumewahi kulalamika kwenye mamlaka husika ikiwamo Tarura, lakini hatukuwahi kupewa majibu ya kueleweka badala yake eneo hili, limezidi kusababisha madhara kwa magari na pikipiki zinatumbukia kwenye korongo hili, tunaomba tusaidiwe, kipande hiki kimetelekezwa kwa muda mrefu sana," alisema Melami.

Baadhi ya madereva wa bodaboda, Robert Paulo na Issa Kimweri, wakazi wa kijiji cha Sokon2, walisema eneo hilo limekuwa ni tishio kwa vyombo vya moto kwa kuwa baadhi ya madereva wanapata ajali kutokana na uharibifu wa barabara hiyo.

Kimweri alisema pamoja na kujichanga na wananchi wengine kwa ajili ya kurekebisha barabara hiyo, lakini inaendelea kuharibika kutokana na kuhitaji nguvu za kutumia magreda. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, akizungumzia malalamiko ya wananchi hao alisema, tayari kiasi cha Sh. milioni 140 kimekabidhiwa kwa Tarura, kwa ajili ya kukarabati maeneo yote ambayo ni korofi na yaliyoharibiwa na mavua.

Dk. Madeni aliwataka wananchi kuwa na moyo wa subira wakati barabara hizo zikiendelea kushughulikiwa, kwa kuwa halmashauri ya jiji imeshakabidhiwa kiasi hicho cha fedha kwa Tarura kwa ajili ya kushughulikia kero kama hizo na kupatiwa ufumbuzi wa haraka.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso (wa pili kulia), alipofanya ziara wilayani humo, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## TAEC yaagiza wamiliki X-ray kutoa mafunzo

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

TUME ya Nguvu za Atomic Tanzania (TAEC), imezitaka taasisi zinazomiliki vifaa vya 'X-ray' nchini kwa ajili ya ugakuzi wa mizigo, uhakiki wa usalama na matumizi mengine ya kibinadamu kuwapatia mafunzo wanaofanya kazi kwa kutumia vifaa hivyo ili kuepuka madhara kama saratani.

Dk. Remigius Kawala, Msimamizi Mwandamizi na msimamizi wa utafiti na mafunzo wa TAEC, aliyasema hayo jana wakati akitoa mafunzo ya siku tano kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Makao Makuu Dar es Salaam na hoteli ambao kwa pamoja wanahudumu kila siku na vifaa (mashine) vya X-ray kwa ajili ya usalama.

Dk. Kawala alisema taasisi za serikali na za watu binafsi wanaomiliki vifaa hivyo washirikiane na Tume ya Nguvu za Atomiki kuwapatia elimu ya matumizi sahihi ya mashine hizo za mionzi wakati wa ukaguzi wa mizigo, matibabu, vipimo na ukaguzi wa binadamu ili kuepuka madhara ya mionzi yanayoweza kusababisha kupata saratani, ulemavu na hata vifo.

"Wasipopata mafunzo sahihi, mionzi ikavuja au hitilafu za mashine, zikatoa mionzi ambayo haina kiwango kinachotakiwa kiusahihi, wafanyakazi wao na wateja kwa pamoja watapata madhara yatokanayo na mionzi kwenye chembe hai za binadamu na kuzifanya kuzaliana kwa wingi bila mpangilio hali inayoweza kusababisha ukuaji wa saratani, pia kuleta matatizo mengine ya kibaiolojia," alisema Dk. Kawala.

Alitaja baadhi ya faida za mafunzo hayo kuwa ni kuongeza uelewa kuhusu mionzi na pia kuongeza ujuzi wa namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa usalama na kwa usahihi kwa kutumia vifaa vya mionzi vinavyotumika kukagua mizigo na watu ili kurahisisha uelewa kwa washiriki.

Alisema Tume ya Atomiki inatarajia baada ya mafunzo hayo washiriki wataongeza tija katika maeneo yao ya kazi na mashine zitatumika kukagua mizigo.

Alitaja matarajio mengine kuwa ni kuimarisha usalama kwa kudhibiti madhara ya mionzi kwa watu na mazingira wakati vifaa vya mionzi vinapotumika kukagua mizigo na pia kuimarisha uhusiano kati ya TAEC na taasisi zingine ili kuimarisha ulinzi na usalama kwenye vifaa vya mionzi ili kuthibiti madhara yake.

Alisema TAEC na wadau wa sekta hiyo watafanya majadiliano ili kusisitiza umuhimu wa kuwa na vifaa maalumu vya kupimia mionzi waagizapo mashine hiyo ili kujua kama inavuja au kama mbovu.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bruno Nyalifa ambaye ni ofisa usalama wa hoteli aliishukuru TAEC kwa kuwa mafunzo hayo yamemfungua macho kwa kufahamu matumizi sahihi ya mashine za X-Ray zinazokagua mizigo na binadamu.

Naye Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Teknolojia na Huduma za Ufundi, Dk. Firmi Banzi, aliwataka washiriki kutuma orodha ya wafanyakazi wanaofanya kazi na mashine za mionzi ambao hawajabahatika kupata mafunzo kuwafikia kwa ajili ya elimu.

Akifunga mafunzo hayo Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Prof. Lazaro Busagala, alisema bila mafunzo wananchi watakuwa hawako salama.

"Siku moja nilikuwa nimerudi kutoka safari na nilipofika uwanja wa ndege tukiwa tunasubiri mizigo kwenye mashine ya x-ray mtoto mmoja alirukia mzigo na kuushika wakati mashine ikiwa inafanya kazi huku taa nyekundu ikiwaka, nilimuwahi na kumnasua pale ili asipate madhara ya mionzi, wakati huo mfanyakazi wa mashine na mzazi walikuwa wanamwangalia bila kujua madhara yake," alisema Prof. Busagala.

# SGR kurahisisha usafiri Kanda ya Kaskazini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Reli nchini, Masanja Kadogosa, amesema awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR utakaojengwa kwenye mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha, utawezesha abiria kutumia saa 3:30 hadi 4:00 kutoka Dar es Salaam hadi Moshi.

Juzi, wakati wa kongamano la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) la kumpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kufanikiwa kutekeleza ilani ya uchaguzi kati ya mwaka 2015 hadi 2019, Kadogosa aliwaeleza wananchi wa Moshi, kwamba reli hiyo itakuwa suluhisho la kero ya usafiri katika mikoa hiyo ambayo hufurika abiria wanaokwenda kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

**Katika kipindi hicho cha utekelezaji wa ilani, Rais Magufuli amesimamia misingi ya uchumi pamoja na changamoto kadhaa zinanazoikumba uchumi wa dunia na hata ukanda wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.**

"Nyie ni mashahidi kwamba Rais Magufuli mwezi uliopita alishafungua fursa nyingine za kiuchumi kwa kuifufua reli ya Kaskazini hapa Moshi ambayo ilikufa miaka 12 iliyopita, ile ya Arusha/Moshi iliyokufa tangu mwaka 1983, nayo Rais Magufuli ataifungua tena mwezi Desemba, mwaka huu.

"Habari njema zaidi ni kwamba reli ya kisasa inakuja Moshi na tathmini tuliyofanya inaonyesha kwamba treni ya umeme ambayo itachukua abiria wanaotoka Dar es Salaam kuja Moshi, itatumia saa 3:00 hadi 3:30, lakini Dar hadi Arusha itatumia saa 4:00 na Mheshimiwa Rais, ameahidi utekelezaji wake uko tayari," alisema Mkurugenzi huyo wa TRC.

Maelfu ya abiria kutoka mikoa mbalimbali nchini, hukwama kupata usafiri wa kurudi na kwenda katika miji ya Moshi na wilaya za Hai, Siha na Rombo, kila mwisho wa mwaka na mwanzoni mwa mwezi Januari, kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kutokana na mabasi ya abiria kutotosheleza mahitaji ya wakati huo.

Julai 20, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua safari za treni ya mizigo kwa reli ya Kaskazini katika mji wa Moshi.

Moja ya miradi mikubwa nchini inayompa heshima Rais Magufuli ya kukumbukwa ni utekelezaji wa mradi wa umeme wa maporomoko ya maji ya Mto Rufiji (RHPP) uliojengwa na Kampuni ya Arab Contractors kwa pamoja na Elsewedy Electric zote kutoka nchini Misri. Mradi una uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Mingine ni mradi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), ununuzi wa ndege mpya za Shirika la Ndege nchini (ATCL), ufufuaji wa reli ya Kaskazini iliyokufa miaka 12 iliyopita, ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami, madaraja makubwa na elimu bure.

Katika kipindi hicho cha utekelezaji wa ilani, Rais Magufuli amesimamia misingi ya uchumi pamoja na changamoto kadhaa zinanazoikumba uchumi wa dunia na hata ukanda wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akieleza kuhusu mafanikio hayo ya kiuchumi alisema, "huwezi kuongelea kukua kwa uchumi, bila ya kuangalia vijenzi muhimu vya kuashiria ukuaji wa uchumi, mambo ambayo Rais Magufuli ameyafanya zaidi ni kuhahakikisha mapato ya serikali yanakua, ameziba mianya ya upotevu wa mapato na kuongeza ukusanyaji wa kodi ya serikali, hivyo ni lazima apongezwe."

Pia katika kuhakikisha anapambana na rushwa na ufisadi nchini, Rais Magufuli alianzisha Mahakama ya Mafisadi (makosa ya uhujumu uchumi) ambayo ilianza kazi rasmi Julai mwaka 2017.




Mbunge wa Viti Maalum kupitia Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoani Kilimanjaro, Shally Raymond (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni saba, kwa Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ikiwa ni mchango wake wa mashuka kwa vituo vya afya vya mkoa huo, wakati wa kongamano la kumpongeza Rais John Pombe Magufuli kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2015, lilioandandaliwa na UWT mkoani humo jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Kinamama waonyeshana ubabe mbio za ubunge

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SASA ni rasmi vita ya ushawishi katika mbio za ubunge mkoani Kilimanjaro, imehamia kwa wanawake baada ya wabunge wake wawili kuonyeshana 'umwamba' wa kuchangia kiasi cha Sh. milioni 75 za ukarabati wa jengo la ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro pamoja na uimarishaji wa huduma za afya.

Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, ambaye alimwakilisha Spika wa Bunge, Job Ndugai, katika kongamano la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT) la kumpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi kwa mwaka 2015 hadi 2019, alilazimika kutumia dakika 10 kuwaelezea wabunge hao, namna wanavyoitendea haki falsafa ya Rais John Magufuli.

Aliyetia fora katika kongamano hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki ni Mbunge wa Viti Maalum, Esther Mmasi, anayewakilisha vyuo vikuu nchini ambaye alichangia kiasi cha Sh. milioni 65.

Katika mchango wake, Mmasi alitoa saruji mifuko 1,000 yenye thamani ya Sh. milioni 14, tiles (vigae) masanduku 500 sawa na Sh. milioni 11.5 na ndoo za rangi 60 za Sh. milioni 5.1.

Pia aliahidi kukabidhi miradi mbalimbali ya kinamama kwenye wilaya sita za Mkoa wa Kilimanjaro, yenye thamani ya Sh. milioni 35.

Wakati Mbunge wa Viti Maalum, Shally Raymond, yeye alikabidhi hundi ya Sh. milioni 10 na kuahidi kutoa mashuka kwa ajili ya Hospitali za Mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungumza katika kongamano hilo, Dk. Tulia, alisema msukumo wa wabunge hao wanawake unachagizwa zaidi na kazi nzuri aliyoifanya Rais Magufuli, kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 na katika bajeti ya serikali ya mwaka 2019/2020 ameondoa kero 57 zilizokuwa zikiwaumiza Watanzania.

"Leo tumekuja hapa kumpongeza Rais, Dk. John Magufuli kwa kutekeleza ilani ya CCM kwa mafanikio makubwa katika kipindi chake cha utawala, lakini ninyi ni mashahidi kwamba katika bajeti kuu ya serikali ya mwaka huu wa fedha, serikali yake imeondoa jumla ya kero 57. Uteuzi wa majaji, mawaziri wanawake, wakuu wa mkoa na wilaya ni taswira ya mtu anayejali usawa wa kijinsia, lazima apongezwe," alisema.

# Uhamiaji kupambana na wahamiaji haramu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

IDARA ya Uhamiaji imesema tatizo la wahamiaji haramu kutoka mataifa mbalimbali na kuufanya Mkoa wa Kilimanjaro kama uchochoro wa kupita kwenda Afrika ya Kusini kutafuta maisha, litakuwa historia muda mfupi ujao.

Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Tunu Ng'ondya, aliyasema hayo jana wakati wa hafla fupi ya kuwavisha vyeo vipya maofisa wa idara hiyo waliotunukiwa na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala.

"Tunamshukuru Kamishna Jenerali wa Uhamiaji kwa kuthamini mchango wetu katika utekelezaji wa majukumu ya idara na kuona umuhimu kutupandisha vyeo na hii ni heshima kubwa kwetu, hivyo ni lazima tujitume zaidi.

"Najua mkoa huu upo mpakani na wahamiaji haramu walio wengi wamekuwa wakiutumia kwenda Afrika Kusini kutafuta maisha na hasa ajira, leo nimeongezewa timu ya viongozi hawa kwa ajili ya udhibiti, naamini mtakwenda kuleta mabadiliko chanya na uhamiaji haramu utageuka kuwa historia katika Mkoa wa Kilimanjaro."

Kuhusu udhibiti wa rushwa, Tunu ameeleza: "Serikali tayari imeanzisha utaratibu wa kufanya kwa njia ya mtandao ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anayeshawishika kuomba au kutoa rushwa, wakati wa kupewa huduma katika Idara ya Uhamiaji."

Alitoa rai kwa wananchi ambao bado hawajajua namna ya kutumia mtandao kama uombaji wa viza kielektroniki (e-visa), vibali vya ukaazi kielektroniki (e-residence permit) na utoaji wa hati za kusafiria za kielektroniki (e-passport), ni vyema wakafika katika ofisi za Uhamiaji kwa ajili ya maelekezo kwa kuwa elimu hiyo ni bure.

Baadhi ya maofisa Uhamiaji walioandishwa vyeo akiwamo Innocent Bazobonankira, alimshukuru Kamishna Jenerali wa Uhamiaji kwa cheo hicho, huku akihidi kutekeleza majukumu yake kwa weledi katika nafasi hiyo.

Nipashe

# Spotika



NYOTA EPL WANAOWEZA KUWAHI DIRISHA KUTIMKA UK.20




# MTIFUANO....

Kiungo wa Arsenal, Dani Ceballos, akimiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield na Liver kushinda 3-1 juzi. **PICHA: HABARI UK. 28**

## ISIKUPITE

TANGU Kocha Jurgen Klopp alipoanza kuinoa Liverpool Oktoba 2015, ameiongoza kuifunga Arsenal jumla ya mabao 26 kwenye Ligi Kuu England, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko aliyozifunga timu nyingine katika ligi hiyo. Na ni Everton pekee nyumbani kwa Arsenal (64) iliyoruhusu mabao mengi zaidi ugenini dhidi ya mpinzani mmoja kwenye Ligi Kuu zaidi ya Arsenal nyuma kwa Liverpool (62).

# MAKOSA MATATU YA LAMPARD CHELSEA



Frank Lampard

**LONDON, England**

MCHEZO wa ufunguzi wa kipigo na sare ya nyumbani uliiacha Klabu ya Chelsea katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England (kabla ya mechi za juzi Jumamosi kushinda 3-2 dhidi ya Nowich na kukwea hadi nafasi ya 12).

Kumekuwa na mitazamo chanya na hasi, lakini licha ya ukweli huo, Chelsea wanaweza kuwa na matumaini mapya chini ya kocha wao huyo mpya na gwiji wa timu hiyo, Frank Lampard.

Chelsea ilianza ligi kwa kucheza na Manchester United pale kwenye dimba la Old Trafford, ambapo 'Mashetani Wekundu' hao waliibuka na ushindi wa mabao 4-0.

Wakiwa wametoka kufungwa kwenye mchezo wa Uefa Super Cup na Liverpool ambako timu hiyo ilicheza vizuri zaidi ikilinganishwa kwenye mchezo dhidi ya United.

Na baada ya hapo waliwakaribisha Leicester kwenye Uwanja wa Stamford Bridge, huku Lampard akiwa na matumaini ya kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo, akalazimishwa sare ya kufungana bao 1-1.

Chelsea ilitawala mchezo baada ya kufunga bao la mapema, lakini walijikuta kwenye wakati mgumu wakati Mbweha hao waliposawazisha kipindi cha pili.

Katika mechi mbili za mwanzo za ligi hiyo, makala haya yanakuchambulia vitu vitatu alivyokosea Lampard hapo Chelsea...

**3. Kushindwa kutengeneza mipango**

Kitu cha kwanza ambacho wachambuzi wengi walikizungumzia kwenye mechi hizo za Chelsea ni udhaifu wa kushindwa kutengeneza mipango kwa safu yake ya ushambuliaji. Hata kama Blues walishindwa kufunga wakati wakichapwa 4-0 pale Man United, ilikuwa pengine kwa sababu kila shambulio la United lilitengenezwa na wao Chelsea.

Chelsea ilikosa kujiamini kwenye mipango ya kulinda lango lake. Kwenye mchezo wa Super Cup, mashabiki walimchagua N'Golo Kante kama mtu aliyemsumbua zaidi Virgil van Dijk.

Mason Mount amepewa jukumu la kuwa kwenye kona wakati timu ikishambulia, lakini chipukizi huyo alishindwa kufanya lolote.

Lampard anahitaji kufumua mfumo wake wa ushambuliaji ambao unatakiwa kuwa na madhara na kutengeneza mikakati ya safu yake ya ushambuliaji kuwa bora.

**2. Kuwaamini wachezaji chipukizi**

Chelsea inaweza kuwa imeathirika kwa kufungiwa kutokutosajili, na kwa vyovyote vile Lampard anakuwa na wakati mgumu wa kuchagua kikosi chake.

Lampard aliwachezesha kwa pamoja Mount na Tammy Abraham mbele dhidi ya Manchester United na wachezaji hawa walishindwa kufanya lolote pale mbele hasa kutokana na uzoefu wao mdogo. Kulikuwa na Christian Pulisic au Ross Barkley na Olivier Giroud ambao walikuwa fiti kwa mchezo, ambao wana uzoefu wa kutosha kwenye Ligi Kuu.

Umuhimu wa kuwaanzisha wachezaji wenye uzoefu kwenye kikosi na sio vijana waliotoka moja kwa moja kwenye akademi, ulidhihirika katika mchezo dhidi ya Liverpool, wakati Giroud na Pulisic walipocheza kwa kiwango cha juu kabisa hapo Chelsea.

Lampard anatakiwa kuthamini mchango wa wachezaji wenye uzoefu wakati wa uchaguzi wa wachezaji wake, kuliko kuendelea kuwaanzisha vijana ambao hawakuwa na lolote kwenye matokeo mabaya katika mechi mbili. Kila mchezo wanatakiwa kuchukulia kama fainali.

**1. Udhaifu wa kipindi cha pili**

Limekuwa tatizo la muda mrefu kwa Chelsea kwa kipindi cha misimu michache iliyiopita, wakiwa wanaanza kwa kasi na hata kuongoza kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili kimekuwa kibaya kwao kwa kushindwa kuhimili presha.

Kocha wa Blues hao alikiri mwenyewe baada ya mchezo dhidi ya Leicester. Alisema, "Tunatakiwa kuwa tayari wakati mchezo unapotuacha na kupigana kuurudisha."

Chelsea ilishutumiwa kwa kukaa nyuma na kulinda bao baada ya kuongoza. Hilo linaipa nafasi timu pinzani kuwa na nafasi ya kushambulia kwa kasi na kufunga mabao muhimu ambayo ndio yanaamua hatima ya mchezo. Mbinu hizi zilikuwa zinatumika enzi za Jose Mourinho wakati akiwa kocha hapo Blues, lakini la muhimu ni kwamba wakati huo Chelsea ilikuwa na wachezaji wenye uzoefu na safu yake ya ulinzi iliundwa na mabeki bora duniani.

Sasa zama za John Terry, Alex, David Luiz na Gary Cahill zimemalizika, Chelsea si tena timu inayotoa mabeki muhimu kwa kikosi cha timu ya taifa ya England. Njia bora ya Chelsea kwa sasa ni kushambulia na kupata nafasi ya kutawala mpira kwa muda mrefu.

Kurt Zouma na Andreas Christensen wameonyesha ishara ya kuimarika baada ya mchezo wa United lakini bado wana safari ndefu ya kwenda. Kurudi kwa Antonio Rudiger kunaweza kurudisha angalau uimara wa safu ya beki ya Chelsea.

Haya mambo matatu ndio yanaweza kuwa suluhisho kwa Lampard kuitengenezea Chelsea kuwa timu yenye kiwango bora na ushindani kwenye Ligi Kuu ya England.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER United ni timu pekee ya pili kuweza kuzawadiwa penalti katika kila mechi kati ya tatu za mwanzoni mwa msimu wa Ligi Kuu England, baada ya Chelsea msimu wa 2012-13. Hata hivyo, 'Blues' walizamisha zote kimyani wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakikosa mbili.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA

# Benzema na rekodi ya Ufaransa La Liga

Karim Benzema amekuwa mchezaji wa kwanza kutoka Ufaransa kuweza kutupia mabao 150 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Real Madrid walilazimishwa sare nyumbani ya bao 1-1 dhidi ya Real Valladolid juzi, Jumamosi, shukrani kwa Benzema aliyewapa tabasamu kwa kufunga bao hilo la kwanza dakika ya 82 kwa shuti kali akiwa umbali wa yadi 18.

Hata hivyo, halikutosha kuwapa pointi tatu kufuatia Sergi Guardiola kuisawazishia Valladolid zikiwa zimebaki dakika mbili mpira kumalizika.

Benzema ametumia miaka 10 kuweza kutimiza idadi hiyo ya mabao 150.

Straika huyo wa zamani wa Lyon, msimu mbaya wa 2017-18 ulizua hofu kwake, lakini sasa amerejea kwenye ubora wake.

Na kwa bao lake hilo la juzi, linamrudisha katika mstari, huku pia likimfanya kuwa mchezaji wa saba kuweza kutimiza mabao 150 kwenye La Liga katika klabu ya Real Madrid.






Beki wa KMC FC, Amos Charles (kushoto), akimiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa AS Kigali, Uwanja wa Taifa Ijumaa iliyopita. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# SABABU 5 KMC KUTOLEWA CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, timu ya KMC FC Ijumaa iliyopita iliyaaga mashindano hayo kwa kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya AS Kigali ya Rwanda kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa nchini Rwanda, KMC inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni ililazimisha sare ya bila kufungana.

Matarajio makubwa kwa timu hiyo yalikuwa ni kushinda mechi ya nyumbani, lakini haikuwa hivyo, kwani ilijikuta ikishindwa kufua dafu mbele ya mashabiki wachache waliojitokeza kuishangilia.

Kwa matokeo hayo, KMC iliyopanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu uliomalizika, imeshindwa kuvuka hatua ya awali ya michuano hiyo.

Ilipata zali baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuongeza timu kwa klabu za Tanzania kutoka mbili hadi nne na kwa kuwa Azam iliyoshika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu ilikuwa bingwa wa Kombe la FA na kupata tiketi moja kwa moja, mshindi wa nne kwenye Ligi Kuu ambaye ni KMC ikapata nafasi hiyo. Zifuatazo ni sababu tano zinazoonyesha kwa nini KMC ilifungwa kwenye mechi ya Ijumaa.

**1. Kutokuwa na uzoefu**

Ni mara ya kwanza kucheza Ligi Kuu Tanzania. Ni kama ya kwanza pia kucheza michuano ya kimataifa. Ni timu ambayo pia haijaanzishwa muda mrefu sana. Hii ni sababu tosha ya timu hiyo kutolewa mapema kwa sababu haina uzoefu wa mechi za kimataifa.

Mechi kama hizi mara nyingi ni za kutafuta matokeo zaidi na si kuangalia timu inachezaje. Ukiangalia kwenye mechi ya Ijumaa ni kama vile KMC ilikuwa ikitafuta sare zaidi kwa kutegemea kwenda kwenye mikwaju ya penalti kwa matarajio kuwa wana kipa mzoefu na mwenye uwezo wa kuokoa mikwaju hiyo, Juma Kaseja, hivyo walicheza kwa taratibu mno kwenye dakika za awali.

AS Kigali walicheza kwa nguvu kana kwamba wao wako nyumbani na walikosa bao dakika za mwanzo, kabla ya kupachika bao dakika ya 29 kupitia kwa Rashid Kalisa na baada ya kufungwa ndipo KMC ilionekana kuzinduka na kuanza kufanya mashambulizi, wakati wenzao tayari walikuwa wamebadilisha mfumo kwa kuweka watu wengi zaidi nyuma na straika mmoja mbele, huku wakishambulia kwa kushtukiza.

Hata bao la pili lililofungwa dakika ya 63 na Erick Nsabimana lilitokana na KMC kushambulia zaidi na kusahau kulinda, mpira mmoja mrefu uliopigwa mbele ulisababisha kuzaa kwa bao la pili. Bao la mkwaju wa penalti walilopata KMC lilikuja dakika za mwisho wakiwa wameshachelewa na mechi ikaishia hapo.

**2. Kutokuwa na wachezaji wa kimataifa**

KMC ilicheza ikiwa haina wachezaji wenye uwezo mkubwa, hasa wa mechi za kimataifa. Mchezaji pekee aliyeonekana kumudu vizuri mechi hiyo ni Mrundi Yusuph Ndikumana ambaye licha ya kuokoa bao la wazi, lakini alifunga kwa mkwaju wa penalti, pia alionekana kung'ara, tofauti na wachezaji wengi wa Kitanzania.

Kutokuwapo kwa baadhi ya wachezaji ambao wamesajiliwa na klabu hiyo, lakini bado hawajapata uhamisho wa kimataifa ITC, kumeigharimu pia timu hiyo.

Baadhi ya wachezaji ambao iliwakosa ni Janvier Bokungu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na wengineo hawakuwa sehemu ya kikosi kutokana na ITC zao kuchelewa kufika na hii inatokana na kuchelewa kusajiliwa.

Ingawa AS Kigali ilimkosa Haruna Niyonzima kwa sababu kama hizo, lakini yenyewe ilionekana angalau ina afadhali kwani ilikuwa na baadhi ya wachezaji walioonekana wana uzoefu wa michuano hiyo.

**3. Kucheza mechi jua kali**

Haijajulikana kama muda huo ulipangwa na Caf au wao wenyewe KMC, lakini kucheza mechi muda wa saa tisa ulionekana pia kuiathiri mno timu hiyo kuliko wageni. Ilifika wakati wachezaji wa KMC walionekana kuchoka mno na kushindwa kufanya chochote kile, pale wanapolazimika kutumia nguvu au mbio.

Kama ilivyoainisha mwanzo kuwa KMC ilionekana kucheza taratibu mwanzo wakati wachezaji wao wana pumzi na nguvu, lakini walipofungwa walianza kuhaha uwanja mzima na hapo ndipo walipojichosha zaidi juani.

**4. Kucheza kwenye Uwanja wa Taifa**

Kucheza kwenye uwanja mkubwa kama wa Taifa, halafu timu haina mashabiki wa kutosha nalo ni tatizo.

Kwa kawaida Uwanja wa Taifa ni mkubwa mno, kuanzia kwenye vipimo vya ndani ya uwanja na hata kuzunguka majukwaa, KMC hilo nalo hawakuliangalia. KMC angalau ingeamua kucheza mechi yao kwenye Uwanja wa Uhuru, au Chamazi Complex ingeweza kuwasaidia.

Watu walijitokeza kuishangilia, na idadi ile kama ingekuwa viwanja nilivyoviainisha ingeweza kuwasaidia, lakini Taifa mpaka uonekane mdogo na kuwachanganya wapinzani inahitaji kazi ya ziada.

**5. Kubweteka na sare ya ugenini**

KMC ingeweza kupata matokeo mazuri kama mechi ile ingekuwa ya kwanza. Kitendo cha kwenda ugenini na kutoka sare ya bila kufungana, inawezekana kabisa kuwa baadhi ya wachezaji wao waliona ni kana kwamba tayari wamemaliza kazi.

Wachezaji wa KMC inaonekana hawakujengwa kisaikolojia na kuambiwa kuwa bado hawajamaliza mechi, hivyo kuonekana kucheza kana kwamba tayari wameshasonga mbele na kilichobaki ni dakika 90 tu zitimie.

Hata hivyo, pamoja na matokeo hayo na sababu zote hizo, hawana cha kupoteza na huwezi kuwalaumu kwani kote walipofikia si haba na wanahitaji kupambana na kupata nafasi moja kati ya zile tatu za juu, ili kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa mwakani.

# MASTAA WA5 WALIOSHINDWA KUUZIKA ULAYA MAJIRA HAYA

**PARIS, Ufaransa**

KUMEKUWA na wachezaji wengi ambao kipindi hiki cha dirisha la usajili wa majira ya joto barani Ulaya walikuwa na ndoto ya kuhama au kuhamia katika klabu za ndoto zao, lakini wengine wamefanikiwa na wengine imeshindikana.

Kwa Harry Maguire, Tanguy Ndombele au Antoine Griezmann wamefanikisha kile kilichoonekana kuwa ndoto zao.

Pia klabu nazo zilikuwa na ndoto ya kuwauza wachezaji ambao walionekana kutokuwa na nafasi kwenye vikosi vyao, lakini mshahara mkubwa na kutohitaji kwa wachezaji wenyewe kumesababisha usajili wao kuwa mgumu.

Hapa tunakuchambulia wachezaji watano ambao wameshindwa kuuzika katika kipindi hiki cha majira ya joto, teremka nayo...

**Mesut Ozil**

Kila uvumi uliokuwa unaenea kuhusu usajili wa mchezaji huyo wa Arsenal kipindi hiki cha majira ya joto mwishoe ulishindikana, kwa maelezo kwamba: "Mshahara wake ni kikwazo kikubwa cha Mesut Ozil kununulika na klabu nyingine."

Bahati nzuri kwa Ozil ni kwamba alikubali dili zuri zaidi wakati akisajiliwa pale Arsenal na mashabiki kwa wakati ule hawakuwa na tatizo naye lolote.

Hata hivyo, matatizo yake na timu ya Taifa ya Ujerumani pamoja na kushuka kiwango kukawashawishi mashabiki na kocha Unai Emery, kuhitaji kumuuza kiungo huyo.

Licha ya hilo, usajili wa Ozil umeonekana kuwa mgumu, licha ya kuhusishwa na klabu mbalimbali. Kwa sasa alikuwa akihusishwa na klabu za Uturuki pamoja na D.C United ya Marekani, lakini bado hakuna kilichofanyika hadi sasa na mkataba wake unamalizika mwaka 2021. Na hii maana yake ni kwamba, anaweza kubakia hapo jijini London kwa muda mrefu.

**Gareth Bale**

Mara tu baada ya Zinedine Zidane kurudi tena kuchukua mikoba pale Santiago Bernabéu, Gareth Bale alikuwa anajua kwamba siku zake zinahesabika.

Wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alibainisha wazi kuhusu uhusiano wa mteja wake na kocha huyo mapema Julai, kwa kusema: "Ni rahisi: Zidane hamtaki Gareth. Hakuna uhusiano mzuri kati yao, na hayajawahi kuwa mazuri."

Manchester United, Liverpool na klabu nyingine Ulaya zilikuwa zikihusishwa na mpango wa kumtaka Bale, lakini mshahara wake mkubwa umeonekana kuwa kikwazo kikubwa cha kuuzika.

Alitumaini amepata wokovu wa soka, wakati klabu tajiri ya Ligi Kuu ya China, Jiangsu Suning ilipotangaza nia ya kumchukua, uhamisho huo ulisitishwa na Real Madrid dakika za mwisho baada ya klabu hiyo, kutaka wamchukue bila kulipa ada kwa raia huyo wa Wales. Bale kwa vyovyote ataendelea kubakia hapo.


**Shkodran Mustafi**

Mashabiki wa Arsenal hawamtaki kabisa Shkodran Mustafi na wameonyesha wazi. Kwa mujibu wa mashabiki wa 'Washika Bunduki' hao wa London, makosa ambayo amekuwa akifanya Mjerumani huyo hayavumiliki.

Kocha Unai Emery naye hana 'mahaba' na beki huyo wa kati, huku hivi karibuni alinukuliwa akisema kwamba, alijaribu kumuuza Mjerumani huyo katika madirisha matatu ya usajili, lakini ilishindikana.

Na hali hiyo pia imejitokeza kipindi hiki cha majira ya joto na hivyo kwa vyovyote Emery ataendelea kubakia na mchezaji huyo na Mustafi anaonekana kama ambaye haelewi kinachoendelea, ingawa alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Monaco na Valencia.

Matumaini pekee kwa Emery ni kama AS Roma wataendelea na mpango wao wa kutaka kumsajili beki huyo kwa mkopo, lakini kwa kuwa mkataba wake unamalizika mwaka 2021, hakuna cha kumzuia Mustafi kurudi tena hapo London baada ya kucheza kwa mkopo kule Italia.




Mesut Ozil

**Adrien Silva**

Wakati anatua kwenye viunga vya Leicester City, Adrien Silva, alionekana kama mchezaji muhimu zaidi kwao. Alitia saini ya mshahara mzuri Januari mwaka 2018, lakini ameshindwa kufikia matarajio ya wengi tangu kutua hapo Midlands.

Ameshindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza, alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita akicheza kwa mkopo pale Monaco, kwenye dili ambalo lilimuhusisha Youri Tielemans kutua kwenye Uwanja wa King Power.

Wakati Tielemans alipotia saini ya mkataba wa kudumu kubakia hapo kipindi hiki cha majira ya joto, ilionekana wazi kuwa Silva atakuwa mrithi wake pale kwenye Uwanja wa Louis II. Hata hivyo, mpango huo ukashindika.

Kocha Brendan Rodgers hivi karibuni alimshauri hadharani Silva kuondoka, lakini hata hilo nalo limeonekana kushindikana kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno. Nafasi yake ya kucheza msimu huu kwa vyovyote itakuwa ndogo na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Rennes au AC Milan.

**Mauro Icardi**

Tangu kuwasili klabuni hapo, kocha, Antonio Conte alibainisha wazi kwamba Mauro Icardi hayupo katika sehemu ya mipango yake. Amekuwa mtukutu si tu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, lakini pia mshambuliaji huyo 'utata' wake ameshindwa kabisa kuuficha. Na bila shaka yoyote zama hizi za Conte klabuni hapo ndio zitamfanya kutopata kabisa nafasi ya kucheza.

Uhamisho wake kipindi hiki cha majira ya joto umekuwa mgumu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina ataendelea kukaa hapo kwenye Uwanja wa San Siro, lakini bila kuwa na nafasi ya kucheza.

Juventus, Napoli, Roma na Monaco zote zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Icardi hivi karibuni, lakini wapi anakwenda, imebakiwa kuwa ni swali lisilo na majibu.

Kama ataendelea kubakia hapo Inter, kwa uhakika kabisa Conte atajaribu kuponya matatizo yaliyopo kati ya klabu na Icardi, kwani mshambuliaji huyo ni mmoja ya wachezaji bora zaidi ambao wana jicho la kuzifumania nyavu na hivyo hatakuwa na namna ya kumwachia.

## Nukuu

"Labda ninaweza kustaafu kazi yangu mwaka ujao ... lakini ninaweza kucheza hadi nikiwa na miaka 40 ama 41. Sijui. Ninachoweza kusema mara zote ni kufurahia wakati wangu. Zawadi hiyo ni bora na lazima niendelee kuifurahia," **ristinao Ronaldo.**



"Mara zote unaweka ulizo kuhusu Paul, siyo?" Solskjaer aliwauliza wanahabari waliokusanyika katika mkutano wa waandishi wa habari. Tunajua kuna mambo yanazungumzwa. Muda utazungumza. Bado tunabaki na swali kubwa. Sina wasiwasi juu ya Paul, kwangu mimi, atabaki," **Kocha wa Manchester United Ole Gunnar Solskjaer**.



"Anapaswa kuwa mvumilivu katika njia sahihi, na pia kila kitu kitakuwa sawa kwa asilimia 100, tunazungumza tu kuhusu Ox kwa sababu kila mmoja anajua ni kwa namna gani alivyo mzuri, lakini tunataka kuhakikisha kwamba anaweza kuonyesha hilo uwanjani pia. Huo ni uamuzi wangu, na wakati ninapofanya uamuzi kuwa sasa yupo tayari ni wajibu wangu bila shaka na kijana anapaswa kujaribu kuonyesha ubora wake," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akizungumzia kuhusu Alex Oxlade-Chamberlain kupewa nafasi kikosi cha kwanza.**





Beki wa Yanga, Lamine Moro (kushoto), akijiandaa kumdhibiti straika wa Township Rollers asileta madhara kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, zilipokutana Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam.

# YANGA ILIVYOSHINDA UGENINI TANGU 2016, AZAM USIPIME

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni Jumamosi safi kwa Watanzania baada ya timu zake mbili, Yanga na Azam FC kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza ya michuano ya kimataifa.

Mjini Gaborone, Botwana, Yanga iliichapa Township Rollers mbele ya mashabiki wake kwa bao 1-0, ikiwa ni mechi ya hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bao la Mganda Juma Balinya aliyepiga faulo kali dakika ya 42, lilitosha kuifanya Yanga kupita hatua hiyo ya awali na sasa itacheza mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Zesco ya Zambia.

Baada ya kushinda mabao 2-0 ugenini dhidi ya Green Mamba ya Eswatini, Zesco ilishinda tena nyumbani bao 1-0 na kutinga raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 3-0, hivyo itakutana uso kwa uso na Yanga mwezi ujao.

Ushindi wa Yanga ugenini ni wa kwanza tangu 2016 kwenye mechi za kimataifa.

Ilikuwa ni Februari 13, 2016 nchini Mauritius iliposhinda bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Cercle de Joachim ya nchini humo.

Lilikuwa pia ni bao la mchezaji wa kigeni, Donald Ngoma dakika ya 17, Mzimbabwe aliyekuwa akiichezea Yanga wakati huo, lakini kwa sasa anakipiga Azam FC na alicheza Jumamosi kwenye mechi ya Azam FC dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia.

Tofauti ndogo ni kwamba mechi ya mwaka 2016 ilikuwa ni ya kwanza na marudiano ikawa nchini Tanzania, Yanga ikishinda mabao 2-0, ya wachezaji Mzimbabwe Thabani Kamusoko na Mrundi Amissi Tambwe ambao kwa sasa hawapo tena na timu hiyo.

Ya Jumamosi iliyopita ilikuwa ni ya pili baada ya ile ya kwanza nchini Tanzania, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, kabla ya Yanga kwenda kupindua meza ugenini.

Mechi nyingine ilichezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Azam FC ikiiwakilisha Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia.

Azam FC iliachilia kipigo cha mabao 3-1 na kutinga moja kwa moja raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Mabao ya Azam yalifungwa na straika mpya kutoka Ivory Coast, Richard Djodi dakika ya 23 na 31, huku Mzambia Obrey Chirwa akipiga bao la tatu dakika ya 59, Mujib Kassim akiifungia Fasil Kenema bao la kufutia machozi.

Ulikuwa ni mchezo wa kulipa kisasi kwani katika mechi ya kwanza wiki mbili zilizopita nchini Ethiopia, Azam ilifungwa bao 1-0, hivyo kutinga raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 3-2.

Kwa upande wa Azam FC si jambo la ajabu kupata ushindi kwenye uwanja wao, kwani imekuwa ni kawaida yao kuufanya uwanja wao kuwa machinjio.

Hata kama ilipokuwa ikitolewa, lakini mara nyingi Azam imekuwa kwanza ikiutumia vema uwanja wake wa Azam Complex vizuri kwenye michuano ya kimataifa.


Timu ambazo zinaufahamu vema uwanja huo si wa kuingia kichwa kichwa na Feriaviario de Nampula ilipochapwa bao 1-0 Kombe la Shirikisho 2014, lakini Azam ikakubali kipigo cha mabao 2-0 ugenini na kutolewa.

Mwaka unaofuata Azam iliisasambua El Merreikh ya Sudan mabao 2-0 kwenye uwanja huo, lakini ikaenda kupoteza kwa mabao 3-0 ugenini na kutolewa kwa jumla ya mabao 3-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mwaka 2016, mabingwa wa sasa wa Afrika, Esperance ya Tunisia nao walikiona cha moto walipokanyaga Uwanja wa Azam Complex na kuchapwa mabao 2-1, ingawa ilipokwenda ugenini Azam ikapoteza kwa mabao 3-0.

Timu ya Bidvest ya Afrika Kusini nayo haikusalimika Chamazi, ikafungwa mabao 2-1, wakati kwenye mechi ya kwanza nchini Afrika Kusini, Azam ilishindiliwa mabao 3-0.

**NAJUA WAJUA**



MOHAMED Salah ameifungia Liverpool katika kila mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England kwenye misimu mitatu aliyoichezea (msimu wa 2017-18, 2018-19 na 2019-20).

Nipashe
Spotika



KUMEKUWA na wachezaji wengi ambao kipindi hiki cha dirisha la usajili wa majira ya joto barani Ulaya walikuwa na ndoto ya kuhama au kuhamia katika klabu za ndoto zao, lakini wengine wamefanikiwa na wengine...

Uk. 16-17

# NYOTA EPL WANAOWEZA KUWAHI DIRISHA KUTIMKA

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili kwa Ligi Kuu ya England limefungwa wiki mbili zilizopita, na siku ya mwisho walisajiliwa wachezaji kama Alex Iwobi, Giovani Lo Celso na Dennis Praet na kujiunga na klabu zao mpya. Na usajili bado haujafungwa kwa ligi nyingine nne barani Ulaya.

Huku pazia la dirisha la usajili likifungwa Agosti 8 nchini England, ligi nyingine Ulaya linafungwa Septemba 2, mwaka huu.

Na hii inamaanisha nini kwa klabu za Ligi Kuu England? Hata kwa klabu kubwa inamaanisha kwamba wachezaji bado wanaweza kununuliwa na miamba wengine wa Ulaya.

Na hapa tunaawangalia wachezaji wanne ambao wanaweza kuondoka kwenye ligi hiyo na kutua katika klabu nyingine, twende...

**1. Alexis Sanchez**

Labda tunaweza kusema kwamba, usajili mkubwa wa Alexis Sanchez kutoka Arsenal na kujiunga na Manchester United, huku akipishana na Henrikh Mkhitaryan Januari mwaka jana haujazaa matunda yaliyotegemewa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile ambaye ndiye anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye ligi hiyo wa pauni 500 kwa wiki, ameshindwa kabisa kuonyesha cheche zake alizokuwa nazo kule Arsenal hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Klabu kadhaa zimetajwa kutaka kumsajili, lakini kikwazo kikubwa ni mshahara wake, ila bado Man United wanamatumaini wanaweza kumuuza mchezaji huyo kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili kwa ligi nyingine.

**2. Christian Eriksen**

Ingawa Tottenham imeanza msimu wa 2019/20 vizuri kwa kupata ushindi dhidi ya Aston Villa na kutoka sare na Manchester City, lakini kocha Mauricio Pochettino tayari amepaza sauti kuwa kikosi chake bado hakipo imara.

Hiyo ni kutokana na wao kutofanya usajili katika kipindi cha majira ya joto na tatizo kubwa kwake ni kiungo wake, Christian Eriksen. Mkataba wa sasa wa Eriksen hapo Tottenham unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2020, na licha ya jitihada kubwa za klabu hiyo kumshawishi kusaini mkataba mpya ambao utamfanya alipwe pauni 200 kwa wiki, lakini hajakubali kusaini.

Mapema Juni mwaka huu, Eriksen alibainisha kwamba, "nataka changamoto mpya" katika maisha yake ya soka, lakini ukiacha usajili ulioshindikana kwenda Barcelona au Real Madrid, hakuna klabu iliyoonyesha nia ya kutaka kumsajili.

Spurs wana hofu kwamba wanaweza kumpoteza mchezaji huyo kwa usajili huru na thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 100. Hivyo, Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy anatakiwa kukamilisha uhamisho wake mapema kwa mchezaji huyo raia wa Denmark.

Atletico Madrid imekuwa ikitajwa kwamba ndio sehemu ambayo anaweza kutua mchezaji huyo, lakini ada yake ya pauni milioni 50 wanayotaka kutoa inaonekana kuwa ni ndogo.



Wilfried Zaha

**3. Wilfried Zaha**

Nyota wa Crystal Palace, Wilfried Zaha alikaribia kuondoka katika klabu hiyo, wakati Arsenal na Everton walipotuma ofa za kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, huku ofa yake ikifikia hadi pauni milioni 80. Lakini Zaha ambaye ana mkataba wa muda mrefu hapo kwenye dimba la Selhurst Park, Palace wakakataa kumuuza.

Pamoja na yote, Zaha ana uwezekano mkubwa wa kuondoka kwenye ligi hiyo ya England kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili Ulaya. Klabu za Borussia Dortmund na Napoli zimetajwa kuwa na nia ya kutaka kumsajili.

**4. Toby Alderweireld**

Tayari tumezungumzia kuhusu kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino na woga wake kwa kikosi chake, kwa sababu Christian Eriksen ameshaonyesha nia ya kutaka kuondoka. Tatizo jingine kwake ni beki wa kimataifa wa Ubelgiji, Toby Alderweireld ambaye anaingia kwenye miezi ya mwisho ya mkataba wake na haonyeshi nia ya kutaka kusaini mkataba mpya.

Klabu ya AS Roma ya Italia inatajwa kwamba inataka kumsajili mchezaji huyo kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili. Hivyo kuna uwezekano mkubwa kwa mchezaji huyo akatimkia nchini Italia.

**USILOLIJUA**



Nicolas Pepe amekuwa mchezaji wa kwanza kufanikiwa kumzidi ujanja, huku akikokota mpira kwa kumpita beki wa Liverpool, Virgil van Dijk hiyo ikiwa ni mara ya kwanza hilo kutokea kwa Mholanzi huyo katika mechi zake 50 alizocheza Ligi Kuu England, tangu Mikel Merino alipofanya hivyo dhidi yake Machi 2018 akiichezea Newcastle.



# Wazazi waagizwa kupeleka watoto hosteli

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WILAYA ya Songwe imegiza wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma kidato cha pili na nne kuhakikisha wanahamia hosteli ili kujiandaa na mitihani ya kitaifa mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samwel Jeremiah, alisema hayo alipokuwa akizungumza na wazazi, walezi pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Galula.

Alisema hatamvumilia mzazi yeyote atakayekaidi agizo la kuwapeleka watoto hosteli kwa sababu ambazo hazina msingi.

Alisema lengo la kuhimiza wanafunzi kuhamia hosteli ni kuwasaidia kujiandaa vyema na mitihani ya kitaifa iliyopo mbele yao kwa sababu watapata nafasi ya kujindaa.

"Kuanzia leo nataka wanafunzi wote wa kidato cha pili na nne wahamie hosteli ili wapate muda wa kujisomea jioni na usiku, kuliko kubaki nyumbani ambako kuna majukumu mengi na kukosa muda wa kujisomea na kusababisha kufanya vibaya kwenye mitihani," alisema Jeremiah.

Alisema katika kutekeleza hilo, ofisi yake itapeleka birika za chai 25 kuboresha ofisi ya walimu pamoja na kuanzisha mfuko wa motisha na yeye amechangia Sh. 100,000 na kuahidi kwenye mitihani kutoa chakula na magodoro ili kuhakikisha ziro hakuna wilayani humo.

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Songwe, Rowllens Kabuje, alisema kwa miaka mingi wilaya hiyo imekua ikifanya vibaya kwenye mitihani ya kitaifa sababu ikiwa wazazi wa eneo hilo ambao wengi ni jamii ya wafugaji na wachimbaji madini wakiwapeleka watoto kufanya shughuli hizo badala ya kwenda shuleni.

"Ni wakati sasa wa kuondoa ziro wilayani kwetu, tunashukuru tumempata mkuu wa wilaya ambaye anapenda elimu hivyo ni jukumu letu sisi wakuu wa idara kuandaa mitihani ya mara kwa mara kuwapima wanafunzi wetu, ili kuwajengea uwezo zaidi wa kukabiliana na mitihani itakayofanyika mwezi Novemba," alisema Kabuje.

Aliongeza kuwa halmashauri imeanza kugawa vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari nne ili kuhakikisha wanatekeleza kaulimbiu ya ondoa ziro Songwe.

Naye Diwani wa Viti Maalum wa Kata ya Galula, Bertha Chifupa, alisema atahakikisha anashiriki ipasavyo kuhamasisha wazazi na walezi walio ndani ya kata yake kutowazuia watoto wao kuhamia hosteli ili kuondoa aibu ambayo ilikuwapo kwa miaka mingi na kufikia malengo waliyojiwekea katika vikao vya halmashauri kuhusu elimu.

# Mkulima kuuza kahawa kielektroniki

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WIZARA ya Kilimo imeanzisha mfumo rahisi wa kielektroniki utakaomuunganisha mkulima kuuza kahawa kwenye soko la moja kwa moja na kumwezesha mkulima kuuza kahawa kwa bei ya soko la dunia, kupitia utaratibu maalumu utakaowekwa na serikali.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga, wakati akizindua mnada wa kahawa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema mfumo wa uuzaji wa kahawa moja kwa moja katika Soko la Dunia utamsaidia mkulima kunufaika na kilimo chake kwa kuwa na uhakika wa kuuza ikilinganishwa na sasa wanavyouza kupitia vyama vya ushirika.

**Walikuwa na malalamiko ya mara kwa mara yakielekeza Bodi ya Kahawa kuvunjwa wakidai imeshindwa kuwatetea wakulima, hivyo mfumo huo utawasaidia kuuza mazao yao kwa uhakika.**

"Serikali yenu ni sikivu imeendelea na jitihada za kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo chao tunazungukia mataifa mbalimbali kuangalia uhitaji wao, ili tuweze kuwauzia mazao yetu, tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa mpaka sasa maana tayari kuna uhakika kwa soko la kahawa na mahindi na mazao mengine nayo yametafutiwa ufumbuzi," alisema Hasunga.

Aliwataka wakulima kuongeza tija kwenye uzalishaji wa kahawa ili waweze kushindana kwenye soko la dunia ambalo linahitaji bidhaa bora.

Aliwataka wakulima kuzingatia kanuni na ushauri wa kitaalamu unaotolewa na maofisa ugani namna ya kulima kilimo cha kisasa ambacho kitawanufaisha.

Baadhi ya wakulima walioshiriki kwenye uzinduzi wa mnada huo, Gervas Mwangoka, alisema utaratibu huo utaongeza uwazi kwenye mauzo ya zao hilo.

Alisema walikuwa na malalamiko ya mara kwa mara yakielekeza Bodi ya Kahawa kuvunjwa wakidai imeshindwa kuwatetea wakulima, hivyo mfumo huo utawasaidia kuuza mazao yao kwa uhakika.

Mwangoka alisema mfumo wa kielektroniki ambao utawaunganisha wakulima moja kwa moja kwenye soko la dunia, utasaidia kuziba mianya ya udanganyifu iliyokuwa inafanywa na madalali kwenye vyama vya ushirika kupitia soko la pamoja.

Katika taarifa yake Waziri Hasunga alisema wafanyabiashara wa mazao mbalimbali hawahitaji tena kufuata vibali wizarani ili kusafirisha mazao nje ya nchi bali vibali hivyo kwa sasa vinapatikana kwa njia kielektroniki.



Wajane waishio katika mazingira magumu wilayani Masasi, mkoani Mtwara, wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa timu ya injili kwa watu wasiofikiwa kutoka Dodoma, baada ya kupokea misaada mbalimbali ikiwamo shuka, vyandarua, doti za khanga na vitenge, katika hafla iliyofanyika mjini Masasi jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Wafugaji wanufaika elimu upangaji bajeti

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Shibolya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamenufaika na elimu ya upangaji bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia ambayo imetolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Elimisha.

Mmoja wa wafugaji waliopata elimu hiyo, Rehema Nsolo alisema, wanawake wamekosa kipaumbele cha kushirikishwa kwenye utoaji wa uamuzi, jambo linalosababisha familia nyingi kutokuwa na bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

Nsolo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Shilolya, wakati Shirika la Elimisha likitoa elimu ya upangaji bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia uliokuwa na lengo la kuweka usawa katika matumizi ya rasilimali fedha.

Alisema wanawake wengi wanajukumu la kuhakikisha mazao na mifugo linakuwa salama, lakini unapofika muda wa mauzo wanaume ndiyo wanahusika na shughuli zote za uuzaji na kupanga matumizi ya fedha hizo bila kuwahusisha wake zao.

"Asilimia 80 ya wanawake vijijini ndiyo wazalishaji, lakini wengi hatuna uamuzi wakati wa mauzo tulichozalisha, elimu hii imetusaidia kutambua haki zetu hivyo ni wakati wetu kupigania bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia," alisema Nsolo.

Aliwataka wanawake wote wanaojihusisha na kilimo pamoja na ufugaji kuhakikisha hawako nyuma unapofika wakati wa mavuno na upangaji wa bajeti kushiriki kama wazalishaji wakubwa badala ya kuwaachia wanaume ambao wakati mwingine fedha za mavuno huzitumia kuhonga michepuko na ulevi.

Akieleza lengo la utoaji wa elimu hiyo, Ofisa Habari wa Shirika la Elimisha, Elizabeth Nyivambe, alisema upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia utasaidia kupunguza vichocheo vya umaskini kwenye jamii, wizi, rushwa, kuongeza ufanisi wa kazi na kuwafanya watu kuwa na matumizi yanayoendana na kipato.

Alisema upangaji huo wa bajeti utasaidia kufahamu unatumia shilingi ngapi kwa siku, shughuli unayoifanya inakuingizie shilingi ngapi na kukidhi mahitaji yako.

Alisema ili kuhakikisha familia na jamii inaondokana na changamoto ya matumizi mabaya ya fedha kwa kutokufuata bajeti, Shirika la Elimisha kwa kushirikiana na serikali linasaidia masuala ya kimkakati na linazingatia malengo na shabaha ya dira ya maendeleo ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.





# Jamii yaaswa utelekezaji watoto wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuacha tabia ya kuwatelekeza watoto wenye ulemavu kwenye vituo badala yake wajumuike nao katika shughuli mbalimbali ili na wao wajione kuwa ni sehemu ya jamii inayowazunguka.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Endles Success Foundation, inayojihusisha na masuala ya kusaidia makundi ya watu wenye uhitaji katika jamii, Amina Feruz, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya maandalizi ya tamasha litakalowajumuisha watoto wenye ulemavu na wasiokuwa walemavu.

Alisema tamasha hilo linalotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu, litajumuisha watoto kutoka Shule ya Antonia's Day Care pamoja na wale wa kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu wa akili cha Miyuji Cheshire Home.

**Sisi kwetu tunawashukuru sana kwani pamoja na ulemavu wetu bado tunahitaji kuwa pamoja na jamii yetu sio kuwa watu wa kutengwa pekee yetu.**

Alisema lengo la tamasha hilo ni kuwajumuisha watoto wote kushiriki mambo mbalimbali kwa pamoja ili kuondoa unyanyapa uliopo katika jamii juu ya watu wenye ulemavu.

Aidha, alisema jamii inapaswa kubadili mitazamo iliyonayo hivi kwa watu wenye ulemavu na kuacha tabia ya kuwatenga kwa kuwaweka katika maeneo ambayo watashindwa kushirikina na watu wengine wasio walemavu.

"Jamii yetu sasa inatakiwa kubadilika na kuacha tabia ya kuwatenga watoto wenye ulemavu kwani na wao ni sehemu ya jamii kinachotakiwa kufanywa ni kuhakikisha kuwa wanapatiwa ushirikiano kutoka katika jamii badala ya kuwatenga katika maeneo yao pekee yao," alisema Feruzi.

Pia alisema pamoja na kuwashirikisha katika mambo mbalimbali watoto hao wenye ulemavu wa akili pamoja na wale walio wazima pia watatoa misaada mbalimbali kwa ajili ya kuwaweze kuendelea kupata mahitaji yao muhimu ya kila siku.

Aliyataja makundi yenye uhitaji ambayo taasisi hiyo imekuwa ikiyasaidia katika jamii kuwa ni pamoja na yatima, wazee, wanawake watoto wa mitaani pamoja na vijana.

Msimamizi wa kituo hicho, Sister Bertha Ligoha, alisema wanashukuru kwa taasisi hiyo kuwapatia fursa hiyo kwani itawasaidia watoto wao kupata nafasi ya kushiriki na wenzao kutoka katika eneo jingine.

"Sisi kwetu tunawashukuru sana kwani pamoja na ulemavu wetu bado tunahitaji kuwa pamoja na jamii yetu sio kuwa watu wa kutengwa pekee yetu," alisema Sister Ligoha.

Alisema kituo hicho bado pia kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo gharama kubwa za dawa kwa ajili ya matibabu ya watoto hao.

Mkurugenzi wa Shule ya Antonia's Day Care, Antinia Mkunya, alisema kujumuika na watoto wenye ulemavu kutasaidia kuwapa faraja na kuwapatia matumaini kuwa jamii inayowazunguka inawajali.



Wafagiaji wakifanya usafi barabarani, katika eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam juzi, bila kuweka alama zinazowatambulisha kuwa wako kazini, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Askofu aomba serikali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la International Evangelism Tanzania, Dk. Eliud Issangya, ameiomba serikali kuhakikisha inawasaka na kuwatia mbaroni watu wote wanaojihusisha na vitendo vya ukatili na utekaji wanawake na watoto.

Dk. Issangya alitoa kauli hiyo baada ya kumalizika kwa ufunguzi wa mkutano mkuu wa wanawake katika Kanisa la International Sinai Ipagala jijini hapa.

Alisema kuwapo watu ambao wanajitokeza na kufanya vitendo vya ukatili, na utekaji pamoja na mauaji kwa wanawake na watoto kunalenga kulichafua taifa na kuliondolea sifa iliyopo ya upendo, amani na mshikamano.

Alisema kanisa linaitaka serikali kuwasaka na kuwachukulia hatua za kisheria wanaojitokeza kufanya vitendo hivyo kwa kuwa wanalitia doa na kuichafua amani iliyopo nchini.

Mwenyekiti wa wanawake wa kanisa hilo taifa, Martha Mbise, alisema semina hiyo imewajenga katika kutunza familia zao kwa kuweza kufanya kazi kwa lengo la kuwaongezea kipato.

Martha alibainisha kuwa semina ya akina mama ambayo ufanyika kitaifa kila mwaka uwajengea uwezo kinamama hao katika kutambua wajibu wao ikiwamo wa kiroho na kimwili.

Naye Askofu wa Mkoa wa Dodoma wa kanisa hilo, Sleyvesta Thadey, alisema semina ya wanawake inalenga kuwajenga kiroho, kimwili na kiuchumi pamoja na kuwajengea ujasiri wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Katika hatua nyingine askofu huyo amewahimiza wanawake hapa nchini kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kwa wale wenye sifa kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi ujao.

Alisema kuwa kanisa linatambua umuhimu wa kazi za kinamama, hivyo ni wajibu wao kutumia fursa waliyonayo kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa pamoja na za kiroho.

# Watakiwa kubuni vyanzo uhakika fedha za Mwenge

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watendaji wengine kuhakikisha wanabuni mbinu za kutafuta vyanzo vya uhakika vya fedha kwa ajili ya shughuli za Mwenge wa Uhuru.

Amesema lengo ni kuondokana na usumbufu ambao wamekuwa wakiupata kila mwaka.

Akizungumza baada ya kufanya tathmini ya mbio za Mwenge kwa mwaka 2019 jijini Dodoma, Dk. Mahenge alisema umefika wakati wa kuwa na chanzo cha uhakika kwa ajili ya zoezi hilo ikiwamo kupanga bajeti ya kila mwaka.

"Hakuna sababu ya kusema mbio za Mwenge ni dharura, kila mwaka unakuwapo, hivyo watendaji wa halmashauri mnatakiwa kujiandaa na kupanga bajeti kuhusu mbio za Mwenge," alisema Dk. Mahenge.

Dk. Mahenge alifafanua kuwa viongozi wa mkoa kwa upande wao wakiongozwa na Katibu Tawala nao wanao wajibu wa kuandaa bajeti ya kupokea na kukabidhi Mwenge katika mkoa mwingine na wasitegemee wilaya kufanya hilo.

Alisema kila mmoja anapaswa kujua wajibu wake kulingana na nafasi aliyokuwa nayo ili kuhakikisha zoezi hilo linakamilika.

"Tunapaswa kuweka mikakati hiyo katika mipango yetu, ikifika muda tunatekeleza ipasavyo," alisema Dk. Mahenge.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema mbio za Mwenge katika kila halmashauri hazina bajeti, hivyo ni wakati mwafaka madiwani katika halmashauri mbalimbali kufikiria kuingiza vifungu vya bajeti kwa ajili ya shughuli hiyo ambayo ni endelevu.

Alisema kutokana na Mwenge kutokuwa na bajeti, imekuwa vigumu kwa wilaya kutekeleza baadhi ya majukumu na hivyo kufanya maandalizi kutokuwa ya kiwango cha juu inapofika wakati wa kupokea.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema wakimbiza Mwenge wanataka wakuu wa idara na wahusika wa miradi wakiwamo makandarasi wanatakiwa kuwa na nyaraka husika, kabla ya kukagua miradi hiyo, hivyo ni vema wanapokabidhiwa kazi wajiandae na vitu ambavyo wanatakiwa kuvifanya.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, alisema, halmashauri yake ilifanya vema katika mapokezi ya Mwenge, na kuongeza kuwa amekubaliana na maagizo ya wakimbiza Mwenge kitaifa kwamba katika ranchi ya Narco wanatakiwa kuweka vibao vya kuonyesha faini kwa watu wanaoingia kinyume cha utaratibu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema wakati umefika sasa kuhakikisha kwamba viongozi wa kisiasa pamoja na wabunge, madiwani wanakuwapo katika mbio za Mwenge husussani katika mapokezi na kukabidhi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bahi, Danford Chisoma, alisema, kunatakiwa kuwapo na maandalizi ya kutosha hasa katika kukagua miradi ya sekta binafsi kabla ya Mwenge kupita na kujiridhisha maandalizi yake ili kukwepa kufanya udanganyifu.



## Mbunge ataka Rais Shein apewe tuzo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Jimbo la Chumbuni, Ussi Salum Pondeza, amesema Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein anapaswa kutunukiwa tuzo ya taifa kwa maendeleo makubwa yaliyoshuhudiwa tangu kushika wadhifa huo mwaka 2010.

Pondeza alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari eneo la Maruhubi kuhusu maendeleo yaliyotekelezwa na Rais Dk. Shein tangu aliposhika wadhifa katika sekta mbalimbali visiwani Zanzibar.

Alisema chini ya uongozi wake maendeleo makubwa yameendelea kushuhudiwa katika sekta ya nishati, usafirishaji na uchukuzi, miradi mikubwa ya maji mjini pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi za wananchi kupitia mradi wa mji mpya wa Kwahani.

"Umefika wakati kwa chama na serikali kumpatia tuzo maalum ya taifa kabla ya kumaliza muda wake, ameleta mabadiliko makubwa ya maendeleo kwa Zanzibar.

Alisema kitendo cha Rais Shein kununua meli ya abiria ya MV Mapinduzi II na meli ya mafuta ya Mkombozi II kimeweka historia kubwa Zanzibar kwa kuimarisha sekta ya usafirishaji na uchukuzi na kuondoa uhaba wa mafuta uliokuwa ukijitokeza Zanzibar.

Alisema sasa Zanzibar tatizo la nyumba za makazi kuvamiwa na mafuriko kila mvua za masika limemalizika baada ya kujengwa mitaro ya kupitisha maji machafu katika maeneo mbalimbali ya mji huo na kumwagwa baharini.

"Hivi sasa tunaendelea kushuhudia mradi mkubwa wa maji katika manispaa ya mji wa Zanzibar na tatizo la upungufu wa maji nalo litabakia historia muda sio mrefu kwanini asipewe tuzo ya nishani ya taifa kwa kazi nzuri Kamanda wetu Rais Dk. Shein," alisema.

Alisema Zanzibar inaendelea na utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia kutokana na juhudi zake baada ya kusimamia mabadiliko makubwa ya sheria ya mafuta na gesi na hatimaye kuyaondoa katika orodha ya mambo ya Muungano.

Alisema chini ya uongozi wa Dk. Shein sekta ya elimu imeendelea kuimarika baada ya kujenga shule nyingi za ghorofa pamoja na kuondoa tatizo la upungufu wa madawati kwa wanafunzi tangu alipounda kamati maalum ya kuratibu tatizo hilo.

# Wanafunzi vyuo vikuu watakiwa kuwa wabunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema ili ujenzi wa uchumi wa viwanda ufanikiwe unahitaji wataalamu wa aina mbalimbali wakiwamo wahandisi wa umeme, mitambo, kompyuta na miundombinu mingine.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania zinatambua umuhimu na nafasi ya vyuo vikuu katika kufanikisha azma za serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Akifungua maonyesho ya teknolojia zilizobuniwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph University Tanzania katika mnara wa Mapinduzi Square, Michenzani, alisema sekta binafsi ina nafasi kubwa katika kuinua uchumi wa taifa na kuimarisha maisha ya Watanzania.

Alisema, serikali inatambua mchango mkubwa wa sekta binafsi hususan kupitia taasisi na mashirika ya dini katika kuisaidia serikali kuinua kiwango cha elimu kwa Watanzania bila kubagua mtu kwa misingi ya dini, kabila na hata taifa ambalo ni lengo la baba wa taifa.

**Serikali inatambua kuwa kuna umuhimu wa kuongeza kiwango cha udahili ili kutoa fursa za kutosha kwa Watanzania wengi zaidi kupata elimu ya juu nchini.**

Vile vile alisema ubunifu wa chuo hicho una mchango mkubwa katika kuzalisha wahitimu katika fani za uhandisi, teknolojia, ualimu wa sayansi na udaktari.

Alieleza kwamba, katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, jitihada zaidi inahitajika katika kuelimisha watu zaidi na kupata rasilimali watu ya kutosha kufikia lengo hilo.

"Serikali inatambua kuwa kuna umuhimu wa kuongeza kiwango cha udahili ili kutoa fursa za kutosha kwa Watanzania wengi zaidi kupata elimu ya juu nchini," alisema.

Alihimiza vyuo vikuu kuendelea kuboresha miundombinu yao ili wanafunzi wengi waweze kudahiliwa na kupata elimu hasa ya masomo ya sayansi, uhandisi na utabibu ambayo yanahitajika wakati huu.

Alivitaka vyuo vikuu na taasisi zote zinazojishughulisha na utoaji wa elimu ya juu kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia utoaji wa elimu ya juu nchini.

Katika hatua nyingine, aliupongeza uongozi wa chuo hicho, walimu na wanajumuiya kwa kazi kubwa walioifanya katika kuwaandaa wanafunzi hao na kufikia hatua hiyo muhimu ya kubuni teknolojia mbalimbali.

Aliwaasa wanafunzi kuwa elimu waliyoipata chuoni ya kubuni teknolojia kuitumikia kwenye jamii kwa weledi na kuiendeleza ili kufikia hatua ya kuanzisha viwanda na kuchangia katika uchumi wa viwanda nchini.

"Mwendelee kuwa wabunifu na kutumia ujuzi mlioupata chuoni katika kufanikisha kauli mbiu ya serikali ya uchumi wa viwanda kwa kufanya kazi katika sekta rasmi au sekta isiyo rasmi," alisema.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo cha St. Joseph, Professa Innocent Ngalinda, alisema ipo dhana potofu kwa baadhi ya wanafunzi kuogopa masomo ya sayansi na hesabu.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Usalama Barabarani nchini, Mhandisi Hamad Masauni (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya mafuta ya Puma Tanzania, Dominic Dhanah (wa tatu kushoto) na Mrajisi wa Jumuiya sisizo za Kiserikali Zanzibar, Ahmed Khalid Abdullah (wa tatu kulia), wakikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni nne kwa uongozi wa Shule ya Msingi Mkunazini, baada ya mwanafunzi Raya Zubeir Hemed (kulia), kuibuka mshindi wa kwanza kwenye shindano la uchoraji michoro ya elimu ya usalama barabarani katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar jana. **PICHA: WMNN**

# Taasisi za fedha zatakiwa kuwafikia wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameziitaka taasisi za fedha kukumbuka dhamana ya kuendelea kusogeza huduma za kibenki karibu zaidi ya wananchi na hasa wale walio vijijini.

Alisema kuna maeneo ambayo wananchi wana kiasi kikubwa cha fedha ambazo hutunzwa sehemu ambazo siyo salama kwa kukosa njia bora za kutunza.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa tawi la Amana Bank, Darajani mjini Unguja, alisema hali hiyo ya wananchi kutunza fedha zao sehemu isiyo salama inatoa mchango mdogo katika kukuza uchumi wa nchi.

"Kutokana na hali hiyo ninatoa rai kwa benki zote nchini kuongeza jitihada za kufungua matawi yake katika maeneo mbalimbali nchini hasa vijijini," alisema.

Alisema mahitaji ya huduma za kifedha nchini ni makubwa na bado taasisi za fedha zina nafasi nzuri ya kupanua wigo wake wa huduma kwa wananchi.

Balozi Iddi alisema benki ya Amana ilianzishwa na Watanzania wazalendo baada ya kuona haja ya kuziba pengo la kukosekana kwa huduma za kibenki zinazozingatia misingi ya sheria za dini ya Kiislamu.

"Huduma hizi zitatoa fursa kwa wananchi ambao walikuwa hawatumii huduma za kibenki za kawaida kutokana na imani zao za kidini," alisema.

Alisema kuanzishwa kwa tawi la Amana ni kichocheo muhimu cha kuvutia uwekezaji na kukuza uchumi wa wananchi wa Zanzibar.

Balozi Iddi alisema ziko fikra kwa baadhi ya wananchi kwamba benki na taasisi za kifedha ni kwa ajili ya matajiri na watu wenye kipato kikubwa ambazo hizo sio fikra sahihi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa benki ya Amana, Dk. Muhsin Salim Masoud, alisema benki hiyo inatoa huduma za kisasa na kipekee kwa kutumia maadili na teknolojia za kisasa.

Alisema benki hiyo inazingatia misingi mitano mikuu ikiwamo uadilifu, uaminifu, uwazi na usikivu. Pia alisema benki hiyo inatoa huduma kwa watu wote bila kujali itikadi zao za kidini.

Aliiomba serikali kutunga sheria maalum kwa benki zinazoongoza misingi ya kiislamu ili kukuza huduma za kibenki ambazo zitatoa ajira.

# Wahitimu 400 elimu ya juu wachangamkia usajili ajira

**Na Silvanus Kigomba,** IRINGA

ZAIDI ya vijana 400 waliohitimu shahada ya kwanza na stashahada katika fani mbalimbali wamejitokeza katika usaili ulioitishwa na serikali wilayani Iringa kwa ajili ya kuwasaidia kupata nafasi za kufanya kazi za kujitolea katika taasisi na kampuni mbalimbali.

Wakizungumza kwenye mahojiano na Nipashe, baadhi ya vijana waliojitokeza akiwamo Silvenia Mathew na Nyota Maulaga walisema wamefarijika na kurejesha matumaini ya kupata ajira kwani utaratibu huo utawapa uzoefu ambao umekuwa kikwazo kila wanapojaribu kuomba ajira katika kampuni, mashirika na serikalini.

"Zoezi hili ni faraja sana kwetu kama wahitimu kwani nimejaribu kuomba kazi katika shule mbalimbali za watu binafsi lakini kila ninapopeleka "CV" zangu wananikataa na kusema hawahitaji mtu wa aina yangu, lakini mimi ndiyo kwanza nimetoka kumaliza chuo napata wapi uzoefu!" Alisema Silvenia.

**Naishukuru serikali ya Rais John Magufuli kwa ubunifu huu maana licha ya kupata uzoefu, pia tumeambiwa tutalipwa nauli kila mwezi, hii itatusaidia wengine kuongeza ubunifu kwenye miradi yetu binafsi.**

Maulaga alisema amefurahi na anaishukuru serikali kwa ubunifu huo ambao utakuwa msaada kwa vijana wengi kwani kwa kupata nafasi ya kujitolea, huku serikali ikilipia nauli na posho itawasaidia vijana kujiamini kwa kupata uzoefu kazini na kipato ambacho baadhi yao wanaweza kukitumia kubuni shughuli nyingine za ujasiriamali na kuondokana na kutegemea kuajiriwa.

"Naishukuru serikali ya Rais John Magufuli kwa ubunifu huu maana licha ya kupata uzoefu, pia tumeambiwa tutalipwa nauli kila mwezi, hii itatusaidia wengine kuongeza ubunifu kwenye miradi yetu binafsi na kuimarisha ili kuondokana kutegemea ajira," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alisema walitegemea kupata vijana kati ya 150, lakini kwa umati huo inaonyesha namna gani tatizo la ukosefu wa ajira lilivyo kubwa kutokana na vijana wengi waliohitimu elimu ya juu katika fani mbalimbali wapo mtaani bila kazi.

"Hii inatuonyesha ni jinsi gani hali ilivyo mbaya, vijana wamesoma wapo mtaani bila kazi. Tunafanya hivi ili tuwape uzoefu na wengine watajiajiri wenyewe kwa uzoefu watakaoupata huko tutakapowapeleka. Wingi wa wahitimu wasio na kazi mtaani ni sawa na kuzalisha matapeli wasomi ambao ni hatari mno kwa ustawi wa jamii yetu," aliongeza Kasesela.

Ofisa Kazi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu- kitengo cha Huduma za Ajira), Theresia Muhanza, alisema mfumo huo umeanzishwa kwa lengo la kuwasaidia wahitimu kupata uzoefu ili waweze kushindana na kuajirika katika mashirika na taasisi mbalimbali bila kukwamishwa na kigezo cha kukosa uzoefu.

Kwa mujibu wa Theresia Muhanza, vijana watakaopata nafasi za kujitolea katika kampuni na mashirika watalipiwa na serikali Sh. 150,000 kila mwezi kwa kipindi cha miezi sita hadi mwaka mmoja, huku serikali ikiendelea kuwashawishi waajiri kuongeza malipo hayo kwa kadiri watakavyoweza.



Mwendesha baiskeli akiwa ameisheheni madumu matupu ya plastiki katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, yanayomfanya ashindwe kuona magari yanayokuja nyuma kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wake barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Fursa ya elimu vijana visiwani

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHUO Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinatarajia kufungua tawi lake Kisiwani Pemba ili kuwapa fursa vijana wa kisiwa hicho kujiendeleza kielimu.

Uamuzi huo umetokana na vijana wengi ambao wanajiunga katika chuo hicho tawi la Unguja pamoja na makao makuu ya chuo hicho, Dar- es- Salaam ni kutoka Kisiwa cha Pemba.

Akizungumza na Masheha wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mkuu wa chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema kuwa wako tayari kufungua tawi hilo mapema mwakani.

Mwakalila aliwataka wazazi na walezi wa kisiwa hicho kuitumia vyema fursa hiyo kwa kuwapeleka vijana wao katika chuo hicho kwa kujipatia elimu.

Mkuu huyo wa chuo aliwapongeza wazazi na walezi Pemba kutokana na mwamko mkubwa walionao kwa kuwapeleka vijana wao katika chuo hicho kwa Unguja na Tanzania Bara.

Alisema wamekuwa wakitoa kozi aina mbalimbali kwa ngazi za cheti, stashahada na shahada bila kuangalia itikadi za kisiasa, dini na hata kabila.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Elimu ya Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakih, alisema kuwa mkutano huo ni mwendelezo wa mikutano mengine iliyopita kwani tayari uongozi huo umeshaonana na viongozi wa mikoa yote miwili ya Pemba pamoja na wilaya zake ili kujadili jambo hilo.

Kuhusu kuanzishwa kwa chuo hicho alisema: "Yote hayo ni juhudi za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwapelekea wananchi wake maendeleo muhimu popote pale walipo, hivyo ni wajibu wetu kuunga mkono jitihada hizo."

# Wanawake 100 kunufaika na mafunzo haki za ardhi

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

SHIRIKA la KAPs Foundation la mjini Iringa, limeanza kutoa mafunzo kwa wanawake 100 na wanaume 20 juu ya Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 ya mwaka 1999.

Mafunzo hayo yanakwenda sambamba na uratibu wa kupata haki za ardhi kwa wanawake kwa vijiji vitano vya Kata ya Sadani, wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa.

Akizungumza jana wakati kutambulisha na kuzindua mradi wa haki za ardhi kwa wanawake Wilaya ya Mufindi, mratibu wa mradi huo, Amos Msambala, amesema mradi huo utatoa mafunzo kwa wanawake 100 na wanaume 20 wa kata ya Sadani.

Aliongeza mradi huo umelenga kuongeza uelewa wa wanawake juu ya haki za ardhi kwa wanawake.

Msambala pia alisema mafunzo yatahusisha viongozi wa serikali, viongozi wa dini, watu maarufu, baraza la kata pamoja na mabaraza ya ardhi ya vijiji juu ya sera ya ardhi ya mwaka 1995, sheria ya ardhi namba 4 na 5 ya mwaka 1999, sheria ya mpango bora wa matumizi ya ardhi, namba 6 ya mwaka 2007.

Naye mwezeshaji wa KAPs Foundation, Renatus Mpiluka, alisema mradi huo unatarajia kuona angalau wanawake100 na wanaume 20 wanakuwa na uelewa juu ya haki za wanawake kumiliki ardhi na mali nyinginezo.

Pia baraza la kata, mabaraza ya ardhi ya vijiji yanawajibika na kushiriki ipasavyo katika kutatua kesi na migogoro kuhusu masuala ya ardhi kwa wanawake.

"Tunatarajia kuona angalau kesi 20 zilizotokana na migogoro ya ardhi zimetatuliwa ifikapo mwezi wa tatu mwaka 2020," alielezea Mpiluka.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Mufindi, Joseph Sylvester Mchina, alilishuru Shirika la KAPs kwa kuamua kutekeleza mradi ambao utasaidia wanawake wengi kupata elimu ya umiliki wa ardhi.

Alisema kuwa ilikuendana na mpango wa serikali shirika hilo, halinabudi kutekeleza mradi huo kufuatana na malengo ya serikali.

## HABARI KIMATAIFA

# Wakenya waanza kuhesabiwa

**NAIROBI, Kenya**

ZOEZI la sensa la kuwahesabu watu na makazi nchini Kenya limeanza na litaendelea kwa wiki moja zaidi.

Maeneo ya burudani yalifungwa mapema Jumamosi baada ya serikali kuwaagiza wananchi kwenda nyumbani ili kuhesabiwa.

Hii ni sensa ya sita tangu Kenya ipate uhuru wake kutoka kwa Mwingereza mwaka 1963, na hufanyika kila baada ya miaka 10, kupata idadi ya watu wanaoishi katika taifa hilo la Afrika Mashariki kwa ajili ya kuisaidia serikali kufanya mipango ya kiuchumi na maendeleo.

Kwa mara ya kwanza, watu wenye jinsia tata, ile ya kiume na kike wanahesabiwa, baada ya kuwapo kwa shinikizo kubwa kutoka kwa wanaharakati na Mahakama kuamuru watambuliwe.

Hata hivyo, zoezi hilo pia hutumiwa na wanasiasa ili kuangazia wingi wa wafuasi wao katika ngome zao kwa sababu siasa za Kenya zimeendelea kuegemea katika mrengo wa ukabila na ukanda.

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta ametoa wito kwa Wakenya kushirikiana na makarani wanaoshughulikia zoezi hilo ili serikali ifahamu hali zao ya maisha.

"Tungependa kufahamu wewe ni nani, una kitu gani ili kama serikali, tuweze kugawa rasilimali tulizopewa na mwenyezi Mungu kwa usawa ili kumfikia kila mwananchi," alisema Rais Kenyatta.

Mbali na sehemu za makazi, zoezi hilo linafanyika hospitalini, hotelini na hata katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi.

Mara ya mwisho kufanyika kwa zoezi hili ilikuwa ni mwaka 2009, na idadi ya Wakenya ilikuwa ni watu milioni 50.

**RFI**

# Kim Jong Un asimamia urushwaji makombora

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

KOREA Kusini imesema majirani zao Korea Kaskazini wamerusha makombora mawili ya masafa mafupi baharini.

Jaribio hilo ni la saba kutekelezwa tangu Korea Kaskazini ilipomaliza mpango wake wa miezi 17 wa kusitisha majaribio yoyote ya silaha zake.

Jaribio hilo lilisimamiwa na Rais wa taifa hilo, Kim Jong Un kulingana na chombo cha habari cha taifa hilo KCNA.

Chombo hicho kilisema kwamba lilikuwa jaribio la kombora kubwa ambalo liliundwa hivi karibuni.

Kim Jong Un alilitaja kombora hilo kuwa silaha nzuri, huku akilishukuru kundi la wataalamu waliounda makombora hayo.

Maofisa wa kijeshi wanasema kwamba makombora hayo yalirushwa saa 12:45 lingine saa 1:02 kwa muda wa Korea Kaskazini kutoka mji wa Mashariki wa Sondok Kusini mwa mkoa wa Hamgyong.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa makombora hayo yaliruka umbali wa kilomita 380 na urefu wa kilomita 97 kabla ya kuanguka katika bahari ya Japan, pia ikijulikana kama bahari ya mashariki.

"Jeshi letu linachunguza hali ilivyo iwapo majaribio zaidi yatafanyika huku tukujiandaa," alisema Mkuu wa Jeshi wa Korea Kusini.

Waziri wa Ulinzi wa Japan, Takeshi Iwaya alithibitisha kombora hilo halikuanguka katika maji ya Japan lakini akataja kuwa ni ukiukaji wa wazi wa maazimio ya Umoja wa Mataifa (UN).

Pyongyang tayari imeonyesha kukasirishwa na mazoezi ya kijeshi ya pamoja ya Marekani na Korea Kusini ambayo yamekuwa yakiendelea.

Korea Kaskazini imeyataja kuwa maandalizi ya vita na kusema kwamba yanakiuka makubaliano walioafikiana na Rais wa Marekani, Donald Trump na Rais wa Korea Kusini, Moon Jae-in.

Marekani na Korea Kusini zimekataa kufutilia mbali mazoezi hayo na kwamba wameyafanya kuwa ya kiwango cha juu.

Katika taarifa iliyotolewa na Rais wa Korea Kusini siku ya Jumamosi, ilitoa wito kwa Korea Kaskazini kutoongeza wasiwasi wa kijeshi uliopo huku akisisitiza mpango wao wa mazungumzo na Marekani kwamba utaendelea.

Mazungumzo ya kutounda silaha za kinyuklia yamekwama tangu mkutano wa ana kwa ana kati ya Rais Trump na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Mjong Un kugonga mwamba mnamo Februari, mwaka huu.

Juni viongozi hao wawili walikutana katika eneo la mpakani kati ya mataifa hayo ya Korea na kukubaliana kuendelea na mazungumzo.

Akizungumza baada ya majaribio hayo mawili, Rais Trump alisisitiza kwamba ana uhusiano mzuri sana na Kim ambaye anasema kuwa amekuwa mkweli kwake.

***BBC***




Waziri wa Fedha wa Kenya, Ukur Yakatani (katikati), akizungumza na waandishi habari kuhusu zoezi la sensa lililoanza juzi na kumalizika jana. **PICHA: REUTERS**

# Viongozi G7 wajadili uchumi, hali ya hewa

**PARIS, Ufaransa**

MKUTANO wa kilele wa viongozi wa nchi za G7 umeanza vikao vyake vya mwanzo jana.

Viongozi kutoka nchi zinazoongoza kwa demokrasia na uchumi duniani wanakutana mjini Biarritz, Ufaransa.

Mkutano huo wa kilele wa mwaka huu hata hivyo utakwenda kinyume na utamaduni wake kwa kutokuwa na taarifa ya pamoja baada ya kumalizika kwake.

Mwenyeji wa mkutano huo, Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alisema hatua hiyo inalenga kuwaepushia wakuu wa nchi na serikali kujiepusha na mivutano itakayotokana na kutokubaliana, kuepusha kuzianika wazi tofauti zitakazojitokeza baina yao.

Marekani haikubaliani na Rais Macron na viongozi wengine juu ya masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa, na wakati huo huo maoni ya Rais wa Marekani, Donald Trump juu ya biashara ya kimataifa.

Maamuzi yake ya kuzitoza ushuru zaidi bidhaa kutoka nchi washirika wa Marekani sawa na maadui zake yamesababisha mkwaruzano na washirika wake wa karibu.

Rais Trump jana alifanya kikao na Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, kabla ya ufunguzi rasmi wa mkutano huo.

Rais Trump na Johnson walikutana kwa mara ya kwanza kama viongozi, na wanatarajiwa kuzungumzia mpango wa biashara kati ya nchi zao baada ya Uingereza kujiondoa Umoja wa Ulaya (EU).

Inaelezwa kuwa macho yote yatakuwa kwa Boris Johnson ambaye anahudhuria mkutano wa kwanza wa kimataifa tangu alipoingia madarakani Julai kwa ahadi ya kuiondoa Uingereza kutoka EU na kurudisha hadhi ya taifa lake.

Mazungumzo ya waziri mkuu huyo wa Uingereza na Rais wa Tume wa Ulaya, Donald Tusk, baadaye yanaweza kuwa ya mvutano baada ya viongozi hao kukwaruzana juu ya nani atakaye laumiwa ikiwa Uingereza itaondoka kutoka Umoja wa Ulaya bila ya makubaliano.

Kikao cha kwanza cha G7 kinatarajiwa kuangalia masuala ya uchumi wa kimataifa, biashara na usalama.

Baada ya chakula cha mchana, marais, mawaziri wakuu na viongozi wa mashirika ya kimataifa waliohudhuria mkutano huo walijadili juu ya ukosefu wa usawa ulimwenguni.

Washindi wa Tuzo ya Amani Nobel, Denis Mukwege na Nadia Murad waliwasilisha mada juu ya masuala ya usawa wa kijinsia.

Viongozi waliohudhuria kutoka Bara la Afrika walihutubia masuala kuhusiana na eneo la Sahel yaliyokubaliwa na wingi wa makundi ya kijihadi yaliopewa kipaumbele maalumu.

***DW***

# Siku ya Lishe yatangazwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetangaza kila Agosti 7 kuwa na maadhimisho ya Siku ya Lishe ambayo yataenda sambamba na Sikukuu ya Wakulima (Nanenane).

Tangazo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, katika kikao cha kutathmini utekelezaji wa afua za lishe kilichowakutanisha wakuu wa mikoa, makatibu tawala na waganga wakuu wa mikoa.

Jafo alisema siku hiyo imechaguliwa ili iende sambamba na maonyesho ya wakulima na wafugaji ambayo yanaendana na masuala ya lishe.

"Tutaunganisha na maadhimisho ya Nanenane, kwa kufanya hivyo tutapeleka taifa mbele katika masuala ya lishe, jamii itapata taarifa sahihi kuhusu masuala ya lishe kwa kuwa taasisi za kilimo na ufugaji zitakuwapo," alisema.

Aliongeza: "Mikoa itaadhimisha siku moja kabla ya kilele cha maadhimisho ya Nanenane."

Kadhalika, aliwataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala kuhakikisha halmashauri zinasainiana mikataba ya lishe na vijiji na kata zote nchini ifikapo Septemba 30, mwaka huu.

Alisema agizo hilo limekuja kutokana na kuwapo kwa taarifa kuwa baadhi ya halmashauri hazijatiliana saini mikataba ya lishe na vijiji au kata.

"Hakikisheni mnasimamia utekelezaji wa afua za lishe kwenye mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ili jamii iweze kupata huduma bora na kuondokana na hali duni ya lishe nchini," alisema.

Aidha, alisema utekelezaji wa mkataba na usimamizi wa shughuli za lishe unahitaji kusimamiwa na mikoa ili halmashauri ziweze kutekeleza na kuboresha huduma za lishe kwa wananchi wote.

"Nawaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha mnasimamia watoto wenye utapiamlo nchini, ili wapatiwe chakula dawa kwa ajili ya matibabu ili kunusuru maisha ya watoto," alisema.

Awali, akiwasilisha mada katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Dk. Germana Leyna, alisema kwa mujibu wa utafiti wa hali ya lishe uliofanyika mwaka 2018 nchini, Mkoa wa Kilimanjaro unaongoza kwa kuwa na wanawake wanene wenye viribatumbo.

Pia alisema mkoa wa pili ni Dar es Salaam huku akiitaja mikoa ya Kagera, Geita, Simiyu, Kigoma, Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza ina watoto zaidi ya 150,000 wenye udumavu ambao wapo chini ya miaka mitano.

"Huu utafiti umeshirikisha watoto 17,524 wenye umri wa chini ya miaka 5 na wanawake 9,426 wenye umri wa miaka 15-49, na tumefanya kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitano kutoka Zanzibar," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Uratibu wa shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Paul Sangawe, alisema mkataba wa lishe umeongeza uwajibikaji wa masuala ya lishe nchini.

Alifafanua kuwa umechangia utapiamlo aina ya udumavu wa kuendelea kushuka kutoka asilimia 34.7 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018.

# Wawekezaji waonyeshwa fursa ya zabibu Dodoma

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WIZARA ya Viwanda na Biashara imewataka wawekezaji kujenga kwa wingi viwanda vya kuchakata zabibu kwa kuwa hutumika kutengeneza malighafi nyingi.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alitoa kauli hiyo juzi katika ziara ya kutembelea mashamba ya zabibu yaliyopo eneo la Mpunguzi jijini hapa.

Alisema wawekezaji wanatakiwa kuangalia fursa ya uwekezaji katika viwanda vya zao la zabibu kutokana na kutumika kutengeneza malighafi nyingi nchini na nje.

"Jambo ambalo litawapa faida kubwa kwenu na taifa kwa ujumla kwa kuwa zao la zabibu hutumika kutengeneza vitu mbalimbali kwa hiyo ni vema wawekezaji kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya zao hili," alisema Manyanya.

Manyanya alisema hivi sasa Taifa linaelekea katika uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ni vema wawekezaji wakawekeza katika viwanda hivyo ili kusaidia zao hilo kupata soko kubwa.

"Zao la zabibu linatoa faida nyingi kutokana na kwamba hutumika kutengeneza aina nyingi ya vimimika ambavyo hutumiwa na jamii katika nchi mbalimbali," alisema.

Aliwataka wamiliki wa viwanda washirikiane na wakulima ili wasiwanyonye kipindi wanapokwenda kununua zao hilo. "Nawaomba wenye viwanda mjenge utaratibu wa kushirikiana na wakulima wa mazao haya, ninachotaka msiwapunje haki yao na nyie simamieni kwenye haki yenu inayostahili wakati wa ununuzi," alisema Manyanya.

Alisema lengo la serikali ni kuona sekta ya viwanda inakua na kufanya vizuri, lakini pia wakulima wa mazao mbalimbali nao wananufaika kupitia viwanda.

Naye mkulima Samwel Mombo alisema viwanda vingi vya uongezaji thamani ya zao hilo vikijengwa vitawasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa soko la zao hilo hapa nchini kutokana na uwepo wa changamoto ya masoko.


United Nations Development Programme

U N D P
Empowered lives.
Resilient nations.

**ADVERTISEMENT**

**CALL FOR PROPOSALS FOR PROVISION OF LEGAL AID IN ZANZIBAR**

UNDP in collaboration with the Ministry of Constitution and Legal Affairs (MoCLA) - Zanzibar is soliciting proposals from Legal Aid providers with proven experience and track record in providing legal assistance in Zanzibar.

Interested and competent Legal Aid providers with proven experience and track record in providing legal assistance and support are therefore invited to submit Technical and Financial proposals on or before Monday, 23 September 2019 at 14.00 hours (EAT) to:

**United Nations Development Programme (UNDP)**
**UN Compound**
**182 Mzinga Way, Osterbay**
**P.O. Box 9182**
**Dar Es Salaam, Tanzania**

**Attn: UNDP Registry**

The Terms for Reference (ToR) may be downloaded from the following link:
**http://procurement-notices.undp.org/view_notice.cfm?notice_id=58605**

Requests for clarification should be sought in writing from the following e-mail address:
**paul.turay@undp.org** or **fridah.mwakasyuka@undp.org**

Proposals in one original plus four copies, duly completed and marked **"Call for Proposal for provision of Aid in the Criminal Justice Sector, DO NOT OPEN BEFORE MONDAY, 23 September 2019 at 14.00 hours (EAT)"** must be submitted before closing time.

All proposals must be delivered by hand/courier services and reach UNDP Tanzania before the deadline as indicated above.

**Late proposals will not be accepted.**

Plot No.182, Mzinga Way, Oysterbay. P. O. Box 9182, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255-22-2112576 Fax: +255-22-21111668 Website: http://www.tz.undp.org/ Email: registry.tz@undp.org



RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


(Substituted Service)
**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**
**FOR KAHAMA**
**AT KAHAMA**
**LAND APPLICATION NO. 52/2019**

**ZABELA THADEO BUHAGA** **APPLICANT**

**VERSUS**

1. JOHN KAGUNILA
2. **PETER JOSEPHAT NGUMA**
3. **MUSA WIBONELA** **RESPONDENTS**

**TO:**
1. **JOHN KAGUNILA**
2. **PETER JOSEPHAT NGUMA**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for Mention on 30th day of August 2019 at 09:00am before **Hon. PAULOS L.S LEKAMOI** Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be **mentioned.**

**TAKE FURTHER NOTICE** that, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and the **SEAL** of this tribunal this 30th day of July 2019.

CHAIRMAN

215387802

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**Juma Selemani** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji aina ya WANHOO yenye namba za usajili **MC917 BMG** Yenye chassis no **LW8HD-MZ41GW005585** NA Engine na **WH160800056** Kwa yeyote atakayeiona atoe Taarifa kituo chochote cha polisi **Taarifa ya polisi KAH /RB/629/2019**

215388101

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Samson Mwijarubi Ndaro** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 720 DCJ.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **NML/RB/19900/19**

215388002

### KUPOTEA KWA KADI

**Said Mohamed Said** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Isuzu tipper yenye namba za usajili T 607 ARF Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya Polisi: **KAH /RB/539/2019**

215387902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMI NA: 195/2018**

**TITUS MUGUNYA A. KAGASHE ...............MDAI**
**@ ABDU MUGUMYA KAGASHE**
**DHIDI YA**
**DEUSDEDITH KAIJAGE ........................... MDAIWA**

KWA DEUSDEDITH KAIJAGE
(POPOTE PALE MLIPO)
Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na. 195/2018 yamepangwa kutajwa tarehe 30.09.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 23.08.2019

215387602


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# LICHA YA KIPIGO EMERY AONA MWANGA ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery alikatishwa tamaa kwa kichapo cha mabao 3-1 na Liverpool, lakini ana matumaini kuhusu majaliwa mazuri ya baadaye kutokana na kiwango kilichonyeshwa na timu hiyo.

'Washika Bunduki' hao ndoto zao za kuanza msimu bila kufungwa zilimalizwa pale Anfield, wakati wekundu hao walipopata mabao matatu kupitia Joel Matip na Mohamed Salah.

Bao la kufutia machozi kwa Arsenal lilifungwa na Lucas Torreira na akizungumza baada ya mchezo huo Emery alisema anaona dalili chanya kwa siku za usoni kwa kikosi hicho licha ya kufungwa.

Arsenal ilipoteza mchezo wake wa kwanza msimu huu baada ya kupata ushindi dhidi ya Newcastle na Burnley.

"Nimekatishwa tamaa na matokeo. Ni kitu cha kwanza unachoweza kuelezea baada ya dakika 90, tulifanya kitu tofauti na wachezaji," alisema Emery.

"Tulitaka kumiliki mpira vizuri, lakini pasi zao zilikuwa imara na tulishindwa kuzivunja kama tulivyotaka."

Arsenal walikuwa bado kwenye mchezo hadi David Luiz aliposababisha penalti kwa kumvuta jezi, Mohamed Salah, kitendo ambacho Emery anadhani hakikuwa sawa.

"Katika kipindi cha pili nguzo kuu ilikuwa ni penalti. Nafikiri ilikuwa laini na nafikiri haikutosha, lakini iliamuliwa hivyo na tukaendelea."

# PSG KUTUMIA MIL. 100 KUMSAJILI ZAHA

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain inapanga kutoa kiasi cha pauni milioni 100 kwa ajili ya usajili wa mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha kama ndiye mrithi wa Neymar, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mirror.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, tayari wametuma wawakilishi wao jijini London kuanza mazungumzo na Palace wakati Barcelona na Real Madrid wakishindana kusaka saini ya Neymar.

Miamba hao wa soka la Hispania wapo kwenye mbio moja kutaka kukamilisha usajili wa pauni milioni 200 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili La Liga Septemba 2, mwaka huu.

Crystal Palace ilitangaza dau la pauni milioni 100 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 wakati timu za Ligi Kuu ya England, Arsenal na Everton zilipoonyesha nia ya kutaka kumsajili.

PSG pia inahusishwa na mpango wa kutaka kumsajili nyota wa Juventus, Paulo Dybala kama wakimpoteza Neymar, na kama atatua Ufaransa miamba hao wa Serie A watakuwa kwenye wakati mzuri kumsajili Christian Eriksen kutoka Tottenham.



Lakini usajili wa Dybala hautazuiwa kusajiliwa kwa Zaha.

Zaha alisaini mkataba wa miaka mitano unaofanya kulipwa kiasi cha pauni 130,000 kwa wiki pale kwenye dimba la Selhurst Park kipindi cha majira ya joto kilichopita.

# FIORENTINA YAMNYATIA DUNCAN WA LIVERPOOL

**ROME, Italia**

KLABU ya Fiorentina imejiunga kwenye mbio za kuwania kumsajili 'dogo' wa Liverpool, Bobby Duncan na kinda huyo yupo tayari kuondoka Anfield.

Timu hiyo ya Italia imetoa ofa ya mkopo kumsajili mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 18, hadi mwishoni mwa msimu.

Gazeti la Daily Mail limebainisha kwamba, Duncan anataka kujiunga na Fiorentina kutokana na kutopata nafasi ya kucheza katika kikosi cha wakubwa.



Kinda huyo ameondoa nembo ya Liverpool kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii kuonyesha ishara kwamba anaondoka klabuni hapo.


Ofa ya Fiorentina imekuja baada ya klabu ya nchini Denmark, FC Nordsjaelland kutoa ofa ya mkopo wa muda mrefu kwa kinda huyo.

Duncan anatazamwa kama mmoja wa vijana wenye vipaji vikubwa zaidi akiwa ni zao kutoka akademi ya Liverpool na alikuwa sehemu ya mipango ya kocha, Jurgen Klopp kipindi cha maandalizi ya msimu mpya.

Lakini sasa Duncan ameamua kuonyesha wazi mpango wake wa kutaka kuondoka Liverpool kwani anajua wazi kwamba hataweza kupata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Kinda huyo ambaye ni binamu yake na Steven Gerrard, aliingia kwenye akademi ya Anfield msimu uliopita akitokea Manchester City.

Lakini Duncan, ambaye amefunga mabao 32 kwa timu ya akademi ya 'Wekundu' hao mwaka jana, alikuwa akitajwa kuwa na nafasi katika kikosi cha kwanza cha Klopp.



# SOLSKJAER

## AKOSA NENO KUBAGULIWA RASHFORD

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesema "amepoteza maneno" baada ya mchezaji wa pili wa Manchester United kubaguliwa kwa rangi yake katika mitandao ya kijamii.

Marcus Rashford alitumiwa maneno mazito ya ubaguzi kupitia mtandao wa Twitter baada ya kukosa penalti wakati Man United wakifungwa 2-1 na Crystal Palace katika dimba la Old Trafford Jumamosi, ikiwa ni siku tano baada ya tukio kama hilo kumkumba Paul Pogba.

"Ni sawa na tulivyozungumza kabla ya wikendi; inahitaji kuzuiwa," alisema Solskjaer wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Nimepoteza maneno ya kuzungumza. Wanajificha kwa kutumia majina bandia na hilo ni jambo la kipuuzi kulizungumzia mwaka 2019."

Rashford alikosa penalti katika kipindi cha pili baada ya Jordan Ayew alipofunga baada ya dakika 32 na kuwafanya Palace kupata bao la kwanza katika dimba la Old Trafford kwa kipindi cha miaka 15.

Daniel James alisawazisha dakika mbilli kabla ya mpira kumalizika na Patrick van Aanholt akafunga la ushindi kwenye dakika ya tatu ya nyongeza kwa kumtungua golikipa, David De Gea.

"Nafikiri tulifanya kazi kubwa ya kujaribu kupenya," alisema Solskjaer.

## Sare ya Real Madrid yamkasirisha Zidane

**MADRID, Hispania**

MATUMAINI ya Real Madrid yalivunjwa nguvu na bao la kusawazisha la dakika ya 88 kutoka kwa nyota wa Real Valladolid, Sergi Guardiola wakati kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane kikilazimishwa sare ya 1-1 kwenye mchezo wao wa kwanza nyumbani wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu huu juzi, Jumamosi.

Karim Benzema alionekana ameipa ushindi wa pili mfululizo Madrid akitoka kufunga pia wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Celta Vigo wiki iliyopita, wakati alipofunga dakika ya 82.

Mfaransa huyo ambaye msimu uliopita alikuwa mfungaji bora wa kikosi hicho, alitumia vizuri pasi aliyopewa na kufunga kwa shuti la mbali na kuipa timu yake uongozi.

Mshambuliaji wa kimataifa wa Serbia, Luka Jovic alikaribia kufunga, lakini shuti lake kali liligonga mwamba, huku pia Gareth Bale na James Rodriguez wakikosa nafasi za wazi.

Valladolid hawakupata nafasi nyingi za kufunga, lakini walitumia nafasi pekee aliyoipata Guardiola ambaye alisawazisha kwa kumfunga golikipa, Thibaut Courtois.

"Nimeachwa na ladha mbaya kwa sababu tulifanya kitu kigumu ambacho ni kufunga kipindi cha pili ambacho hatukucheza kwa kiwango chetu," kocha wa Madrid, Zidane aliwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Ni hisia mbaya wakati timu inaposawazisha dakika chache baada ya wewe kufunga. Tulicheza vizuri kipindi cha kwanza, lakini tulishindwa kutikisa nyavu."

# Coutinho aanza kwa 'shoo' kali Bayern

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski alifunga mabao matatu 'hat-trick' na Philippe Coutinho alianza kuwachezea kwa mara ya kwanza mabingwa Bayern Munich wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Schalke juzi Jumamosi na kupata ushindi wao wa kwanza wa Bundesliga msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 31, alifunga bao la kwanza dakika ya 20 kwa mkwaju wa penalti na akaongeza la pili kwa shuti la adhabu ndogo baada ya kuanza kwa kipindi cha pili.

Alifikisha hat-trick yake ya tisa kwenye Bundesliga wakati alipofunga bao la tatu dakika ya 75 na kumfanya afikishe mabao matano katika mechi mbili msimu huu.

Bayern, ambao walianza kwa sare ya 2-2 kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Hertha Berlin, kwa sasa wamefikisha pointi nne, mbili nyuma ya vinara Borussia Dortmund, ambao walishinda mabao 3-1 dhidi ya Cologne Ijumaa.

"Naweza kucheza kwa ubora zaidi. Ni nafasi ya kuimarika zaidi," alisema Lewandowski, ambaye anakaribia kuongeza mkataba wake na miamba hao wa Bavaria, wakati akizungumza na waandishi wa habari.



"Unaweza kushinda baadhi ya mechi peke yako, lakini ukiwa na timu unashinda mataji."

"Bundesliga si ligi rahisi na mara zote tutatakiwa kuwa tayari. Nilikuwa tayari na nina furaha kuisaidia timu yangu," alisema.

Mshambuliaji huyo sasa amefunga penalti 24 kati ya 27 kwenye Bundesliga, huku akifunga mabao 16 katika mechi 19 za Ligi Kuu dhidi ya Schalke.

Coutinho, usajili mkubwa wa Bayern kipindi hiki cha majira ya joto, pia aliingia kwenye mchezo huo kipindi cha pili na kucheza kwa mara ya kwanza katika ardhi ya Ujerumani baada ya kujiunga kwa mkopo akitokea Barcelona na aliwaambia waandishi wa habari kwamba amepewa heshima kucheza mbele ya "gwiji" kama Lewandowski.

"Inavutia kucheza pamoja naye. Yeye ni gwiji," alisema Coutinho. "Yeye ni mchezaji mkubwa, mtu mzuri. Nimekuwa hapa kwa siku tatu au nne, na niliona ubora wake tukiwa mazoezini. Na leo (juzi) amefunga hat-trick."

Ndani ya dakika 30 kwenye soka la Bundesliga, Coutinho aligusa mpira mara 36 na kutoa pasi 28 akicheza kwenye nafasi ya kiungo wa kati.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LUIZ AHOJI PENALTI, KLOPP AKIKUNWA

●●●Sikutumia nguvu, nilimuuliza Mo (Salah) na alisema hakuhisi chochote, na ndio maana hakuanguka chini, lakini…

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesifia "nguvu, kasi na hamasa" ya Liverpool kwenye mchezo wao wa ushindi dhidi ya Arsenal huku, David Luiz akihoji kuvuta kwake jezi kama ni penalti.

Liverpool ilijivuta kwa pointi tatu zaidi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England wakati bao la kichwa la Joel Matip la dakika za mwisho za kipindi cha kwanza lilipowapa uongozi, kabla ya Mohamed Salah kufunga mabao mawili kipindi cha pili ndani ya dakika 10.

Klopp alivutiwa na namna kikosi chake kilivyocheza wakati kikiibuka na ushindi huo wa mabao 3-1.

"Tulikuwa na nguvu kubwa, kasi na hamasa ikiwa ndio kitu pekee unachohitaji unapocheza na timu nzuri kama Arsenal," alisema akiambia Sky Sports.

"Tulishangaza na mfumo waliocheza, walicheza na tulizoea haraka. Sisi tuna hamasa kubwa, lakini yote kwa yote tulikuwa kwenye wakati mzuri na tulicheza soka la kuvutia zaidi.

"Tulikaa na mpira vizuri kwa sababu hawakutushambulia mara kwa mara. Lakini Arsenal ni timu nzuri ambayo ilionyesha kiwango cha kuvutia, ingawa sisi tuliwashinda."

Wakati matokeo yalikuwa bado 1-0 na mpira kuonekana kuwa sawa kwa pande zote mbili, mambo yalibadilika wakati David Luiz alipomvuta Salah nyuma ili asiifikie krosi ya Roberto Firmino. Kitendo cha Luiz kumvuta Salah jezi yake kilitosha kupewa adhabu ya penalti. Lakini baadaye akaiambia Sky Sports: "Sikutumia nguvu, nilimuuliza Mo (Salah) na alisema hakuhisi chochote, na ndio maana hakuanguka chini.

"Lakini sasa tuna VAR, na huwezi kuona nguvu yake na ni ngumu kwa waamuzi. Aliona jezi imevutwa, siwezi kulalamika, ni ngumu kwa upande wao.

"Kama unamvuta mtu kwa kutumia nguvu, lazima atadondoka, lakini kwangu ilikuwa ni tofauti kabisa.

"Alinipa kadi ya njano na sikumfanyia faulo Salah kwa bao la tatu na kuiweka timu yangu kwenye matatizo. Mchezo wangu ulikuwa mgumu baada ya pale."

Baada ya kuangalia Manchester City wakitawala mchezo dhidi ya Tottenham wiki iliyopita na Liverpool ikiwa hivyo hivyo kwa Arsenal, mchambuzi wa soka wa Sky Sports, Jamie Carragher ndivyo anavyofikiri.

Alisema: "Nafikiri Arsenal walicheza vizuri mno kipindi cha kwanza. Waliweza kutawala mchezo kwa dakika 10 hadi 15, lakini Liverpool walibadilika kipindi cha pili na Arsenal walishindwa kuwazuia.

"Ilionyesha jinsi gani wako mbali na Manchester City na Liverpool. Ni ukweli kwamba wapinzani wao wamekuwa wakubwa zaidi kwao."

## KWA UFUPI

**ZAHA KUSHTUKIZWA PSG**
Paris St-Germain inapanga kushtukiza kwa kutoa pauni milioni 100 kuinasa saini ya winga wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26, kama mbadala wa mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27. ***(Sunday Mirror)***

**UNITED KUMFUATA MADDISON**
Manchester United inatazama uwezekano kwa Januari kwenda kumsajili kiungo wa Leicester City, Muingereza James Maddison, ambaye atawagharimu pauni milioni 80. ***(Sunday Mirror)***

**FIFA KUGEUKIA REFA ROBOTI**
Fifa inachunguza kama roboti linaweza kuwa msaidizi wa refa kwa upande wa kutoa maamuzi ya mchezaji kuotea (offside'), wakati huu ikiwa tayari kukiwa na msaada wa video. ***(Sunday Mirror)***

**GRACIA ANUKIA KUTIMULIWA WATFORD**
Watford inazingatia mustakabali wa baadaye wa kocha Javi Gracia baada ya kuanza msimu wa Ligi Kuu England kwa kipigo cha mechi tatu mfululizo na kufanya kupoteza saba mfululizo kuanzia za mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Mail on Sunday)***

**NAVAS KUIPELEKA MADRID EVERTON**
Real Madrid itatoa ofa ya kushtukiza kwa kipa wa Everton, Mholanzi Maarten Stekelenburg, 36, kama Mchile Keylor Navas, 32, ataachana na miamba hiyo ya Hispania na kujiunga na PSG. ***(Football Insider)***

**SANCHEZ ARUDIWA INTER**
Manchester United na Inter Milan zitarejea tena mazungumzo leo kuhusu dili la mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30. ***(Observer)***

**LIVAKOVIC KUMRITHI DE GEA**
MANCHESTER United itatazama uwezekano wa kuinasa saini ya kipa Mcroatia Dominik Livakovic, 24, kutoka Dinamo Zagreb kwa dau ambalo litafikia hadi pauni milioni 20 kama Mhispania David de Gea, 28, hatatia saini mkataba mpya hapo Old Trafford. ***(Sun on Sunday)***

**NACHO KUTIMKIA REAL SOCIEDAD**
Real Sociedad imekubali dili la kuinasa saini ya beki wa Arsenal, Mhispania Nacho Monreal, 33. ***(Marca - in Spanish)***

**SPURS YAJIAMINI KWA ALDERWEIRELD**
Tottenham imeongeza kujiamini kwa beki Mbelgiji Toby Alderweireld, 30, kutia saini mkataba mpya. ***(Sun on Sunday)***

**FIORENTINA YATUA LIVERPOOL**
Fiorentina imejiunga katika mbio ya kuisaka saini ya mshambuliaji wa Liverpool, Muingereza Bobby Duncan, 18, kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu. ***(Mail on Sunday)***

**DYBALA AIKETISHA CHINI PSG**
Paris St-Germain inajaribu kutatua suala la haki za matangazo kwa Paulo Dybala wakati huu ikitazama uwezekano wa kuinasa huduma ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina anayeichezea Juventus.***(Calciomercato)***

**EZE AWINDWA SOUTHAMPTON**
Southampton inamfuatilia mshambuliaji wa QPR, Eberechi Eze, 21, kabla ya kutoa ofa kwa mchezaji huyo hapo Januari. ***(Sun on Sunday)***

**SAMPDORIA KUIBOMOA ASTON VILLA**
Sampdoria inavutiwa kuipata huduma ya kipa wa Aston Villa, Mcroatia Lovre Kalinic, 29. ***(Il Secolo XIX - in Italian)***

HABARI MICHEZO

# UDHAMINI VODACOM LIGI KUU KUANZA KUINOGESHA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kampuni ya Vodacom Tanzania ikiingia mkataba wa miaka mitatu na Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa ajili ya kuidhamini Ligi Kuu Tanzania Bara, Klabu ya Simba itakuwa mnufaika wa kwanza kwa kumegewa mamilioni kadhaa kutoka Sh. bilioni tisa za udhamini huo, imeelezwa.

Ijumaa iliyopita, TFF na Vodacom zilisainishana rasmi mkataba wa miaka mitatu wenye thamani ya Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kudhamini ligi hiyo inayoshirikisha timu 20, ambazo kwa msimu ujao zitapungua na kuwa 18 kabla ya msimu unaofuata kubaki 16.

Alipoulizwa kuhusu hatima ya zawadi ya bingwa wa Ligi Kuu kwa msimu uliopita, Simba, Rais wa TFF, Wallace Karia alisema kwa kuwa tayari wamepata mdhamini, ndani ya wiki mbili itafahamika zawadi atakayepewa bingwa huyo.

Katika hafla hiyo ya kutangaza mdhamini iliyofanyika jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, mkataba huo umehusisha pande zote ambazo ni Kampuni ya Vodacom Tanzania, TFF na Bodi ya Ligi, ambapo sasa Ligi Kuu Tanzania itaitwa Ligi kuu ya Vodacom , ikitarajiwa kushuhudia jumla ya michezo 380 ikichezwa katika viwanja mbalimbali.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mwakyembe alisema serikali imepiga hatua kubwa katika kuwezesha vijana wenye vipaji mbalimbali nchini na alisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika vijana ili kuleta maendeleo nchini huku akiitaka TFF kuheshimu makubaliano yaliyopo katika mkataba huo.

"Ukweli ni kwamba tupo katika wakati ambao tunahitaji kushirikiana na vijana katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, nawapongeza sana Kampuni ya Vodacom kwa kuiona fursa hii, pia nawataka TFF kuheshimu sana makubaliano yaliyopo katika mkataba huu," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Hisham Hendi, alisema kampuni hiyo iko mstari wa mbele katika kuunga mkono maendeleo na shughuli za mpira wa mguu hapa nchini, hivyo ni siku ya furaha sana kwao.

"Tumedhamini ligi hii kwa zaidi ya miaka tisa na tumeona vipaji vingi vikiibuka na ligi kuongezeka umaarufu nchini na nje ya nchi ikufuatiliwa na mamilioni ya mashabiki. Wote tumekubali kuwa wanamichezo ni mabalozi wazuri wa nchi yetu kama tulivyoona katika michuano ya AFCON iliyoisha hivi karibuni. Ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa tunawaunga mkono katika kutambua na kukuza vipaji vyao kadri tutakavyo weza," alisema Hisham.



Mchezaji wa Ukonga Warriors, Karimu Seleman (mwenye mpira), akipata upinzani mkali wa kupenya ngome ya ulinzi ya Mbagala Hard Core kwenye mechi ya mtoano ya michuano ya Sprite Bball Kings 2019 iliyopigwa katika viwanja vya JK Park jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ni vita mtoano Sprite Bball Kings 2019

**Na Sabato Kasika**

MASHINDANO ya Sprite Bball Kings 2019 yameanza rasmi kwa hatua ya mtoano kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park, jijini Dar es Salaam kwa 43 kushuka dimbani jana.

Timu zilizofungua pazia ni Ukonga Warriors dhidi ya Mbagala Hard Core na Kigamboni City dhidi ya Ukonga Hitmen huku nyingine zikifuatia.

Katika ufunguzi huo, Ukonga Warriors iliifunga Mbagala Hard Core vikapu 37 kwa 25, huku Ukonga Hitmen ikipata vikapu 51 kwa 21 dhidi ya Kigamboni City.

Akizungumzia ufunguzi huo, Mratibu wa Mashindano hayo, Barnabas Mkingwe, alisema baada ya timu zote 43 kushiriki mtoano huo, leo Jumatatu watafanya droo ya kupata jinsi timu 16-bora zitakavyocheza.

"Mtoano huu ni wa kupata timu 16 bora ambazo baada ya kuzipata itabidi tukae tupange timu ipi itacheza na ipi kisha mchuano utaendelea Jumamosi na hatimaye tutapata zitakazoingia fainali," alisema Mkingwe.

Alisema michuano ya Sprite Bball Kings inajumuisha hatua mbalimbali kuanzia usaili, mtoano, hatua ya 16 bora, hatua ya robo fainali, kisha hatua ya nusu fainali na mwisho fainali.

"Lakini pia usishangae kusikia timu zilizofungua pazi zisiwamo kwenye 16-bora, kutokana na ukweli kwamba timu ni nyingi na zinaweza kuwapo zenye vikapu vingi zaidi kuliko hizo zilizoanza," alisema.

Alisema mashindano hayo yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite kwa lengo la kuibua vipaji vya mpira wa kikapu na kuburudisha.

"East Africa Televisheni na East Africa Radio ni chombo cha habari kinachoziunganisha nchi za Afrika Mashariki kikiwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarikisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali," alisema na kuongeza kuwa mshindi wa michuano hiyo atajinyakulia Sh. milioni 10 na kombe la Sprite Bball Kings 2019.

Kwa upande wa mshindi wa pili, alisema atazawadiwa Sh. milioni tatu wakati mchezaji bora ataibuka na kitita cha Sh. milioni mbili na kikombe.

# Soka bwerere, DStv yafyeka bei vifurushi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msimu wa Ligi Kuu barani Ulaya na kwingineko ukiwa ndiyo kwanza umeanza, Kampuni ya DStv Tanzania imethibitisha rasmi kupunguza kiasi kikubwa cha ada ya mwezi ya vifurushi vyake kuanzia Septemba Mosi, mwaka huu ili kumfanya kila mtu afurahia burudani hiyo.

Akithibitisha punguzo hilo la bei jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso alisema muda wote wamekuwa wakisikiliza maoni ya wateja wao na moja ya mambo waliyoshauri ni kupunguzwa kwa bei za vifurushi.

**"Wateja ndiyo moyo wa biashara yetu na muda wote tunawasikiliza na kutekeleza maoni yao pale inapoweze kana. Kwa msingi huu, tumeamua kupunguza bei ili wateja wetu waendelee kufurahia burudani kabambe kwa bei nafuu zaidi," alisema Jacqueline.**

Amezitaja bei hizo mpya kuwa kifurushi cha DStv Premium kitakuwa na punguzo la Sh. 40,000 kutoka bei ya sasa ya Sh. 169,000 hadi 129,000; Kifurushi cha DStv Compact+ punguzo la Sh. 25,000 kutoka Sh. 109,000 hadi Sh. 84,000; Kifurushi cha DStv Compact punguzo la Sh. 25,000 kutoka Sh. 69,000 hadi Sh. 44,000; na kifurushi cha DStv Family punguzo la Sh 10,000 kutoka Sh. 39,000 hadi Sh. 29,000.

Kuhusu vifurushi maalum, Jacqueline alisema kifurushi chenye nyongeza maalum ya chaneli za Asia - DStv Premium+Asia Addon kitapungua kwa shilingi 40,000 kutoka 220,050 hadi 170,050 wakati kile chenye chaneli za ziada za Kifaransa DStv Premium+French addon nacho pia kitapungua kwa Sh. 40,000 kutoka Sh. 259,000 hadi 2019,000.

Mkurugenzi huyo amewahakikishia wateja wa DStv kuwa kushuka huko kwa bei hakutasababisha mabadiliko ya chaneli katika vifurushi hivyo na kwamba mteja ataendelea kupata chaneli zilezile alizokuwa akipata awali ila sasa atakuwa analipa bei ndogo zaidi.

Michezo
Jumatatu Agosti 26, 2019
Nipashe




## Luiz ahoji penalti, Klopp akikunwa

HABARI UK 30

PENALTI!...



Beki wa Arsenal, David Luiz akimvuta jezi mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, kitendo ambacho kilisababisha mwamuzi kutoa penalti iliyozaa bao la pili katika mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield na kumalizika kwa wenyeji kushinda 3-1. **HABARI UK. 30**

# KILICHOIUA SIMBA TAIFA, KAZI KWA YANGA, AZAM

### Kiungo mkabaji shida, Zahera kuelekeza hesabu kwa Lwandamina huku Ndayiragije akipiga hesabu...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameshindwa kumalizia kuutafuna mfupa waliouanza kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya wageni zao, UD Songo ya Msumbiji, hivyo sasa matumaini pekee kwa Tanzania Bara yakibaki kwa Yanga na Azam FC.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa, Simba ilikuwa ikihitaji ushindi wowote ili kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), kufuatia mechi ya kwanza ugenini kutoka suluhu.

Hivyo kwa matokeo hayo, UD Songo inasonga mbele kwa faida ya bao la ugenini ambapo sasa itakutana na mshindi wa jumla kati FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi.

Bao la mpira wa faulo ndogo la dakika ya 13 uliopigwa na kujaa nyavuni moja kwa moja nahodha wa UD Songo, Luis Misquissone lilidumu hadi dakika ya 86 kufuatia Simba kusawazisha kwa mkwaju wa penalti kupitia kwa Erasto Nyoni.

Simba ilipata penalti hiyo baada ya mtokea benchi Miraji Athuman aliyeingia kuchukua nafasi ya Sharaf Eldin Shaiboub, kuangushwa ndani ya eneo la hatari wakati akielekea kufunga.

Kwa ujumla kipindi cha kwanza hususan dakika 20 Simba ilizidiwa nguvu na UD Songo ilitawala mchezo zaidi kutokana na mfumo wao wa kukabia katikati ya uwanja jambo ambalo liliwafanya kutawala kiungo cha kati.

Simba ilijaza viungo wengi, lakini kiungo mkabaji alikuwa ni Jonas Mkude, huku wengine wakiwa viungo washambuliaji jambo ambalo ni wazi liliwafanya UD Songo kutawala dimba la kati na kutimiza malengo yao ya kupata bao la ugenini lililowabeba.

Kipindi cha pili Simba ilitawala mchezo zaidi hususan dakika 25 za mwisho, lakini umakini wa safu ya ulinzi ya UD Songo ndiyo iliyowawezesha kuweza kuokoa mipira mingi ya kupenyeza ya kutoka safu ya ushambuliaji ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao.

Macho na maombi yote kwa Watanzania sasa yanaelekezwa kwa Yanga na Azam FC ambazo zimetinga raundi ya kwanza katika michuano hiyo ya Caf, ili zifike mbali na kuweza kulinda nafasi ya Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo msimu ujao kufuatia KMC nayo kutolewa na AS Kigali kwa jumla ya mabao 2-1.

Kwa Yanga hesabu zake sasa ni namna ya kuikabili Zesco ya Zambia inayonolewa na kocha wao wa zamani, Mzambia George Lwandamina aliyeachana nayo kwa kile kilichodaiwa kutolipwa stahiki zake.

Yanga ambayo imetinga raundi ya kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1, italazimika kujipanga ipasavyo kutokana na ubora wa Zesco.

Zesco imesonga mbele baada ya kuitoa Green Mamba ya Eswatini kwa mabao 3-0 kufuatia ushindi wa mabao 2-0 ugenini kabla ya juzi, Jumamosi kushinda 1-0 nyumbani, Zambia.

Tayari Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera ameeleza kuwa hatua hiyo imemalizika na atafanya maandalizi kulingana na mechi iliyopo mbele yao.

Zahera amesema anahitaji kuendelea kufanyia marekebisho kikosi chake hususan safu ya ushambuliaji ili kuweza kuwa makini kutumia nafasi wanazozipata.

Yanga itahitaji kupata matokeo katika mechi hizo mbili dhidi ya Zesco ili kutinga hatua ya makundi na hata kama itashindwa kupata matokeo katika mechi hizo mbili nyumbani na ugenini dhidi ya Zesco itaangukia mechi za mchujo kwenye Kombe la Shirikisho Africa na kama itapita itaingia hatua ya makundi.

Kwa upande wa Azam FC kwenye Kombe la Shirikisho iliyofanikiwa kutinga raundi ya kwanza kufuatia ushindi wa jumla wa mabao 3-2 dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia, italazimika kujipanga vilivyo ili kuweza kupata matokeo dhidi ya Triangle United ya Zimbabwe iliyoitoa Rukinzo ya Burundi kwa jumla ya mabao 5-0.

Ikiwa katika Uwanja wao wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Azam FC ilipata ushindi wa mabao 3-1 hivyo kuitoa Fasil Kenema kwa jumla ya mabao 3-2 kufuatia mechi ya awali ugenini kuchapwa bao 1-0.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >